

**14 SEPTEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Pili – Tarehe 14 Septemba, 2022**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*).

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2022*).

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Kuwarudisha Wanafunzi Waliokatisha Masomo Shulenii**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya sintofahamu ya utaratibu wa kuwapata wanafunzi wanaorudishwa masomoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI MITAA  
(MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoea Mwongozo wa Februari, 2022 wa kuwarejesha wanafunzi waliokatisha masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali ili waweze kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii pamoja na mwongozo uliotolewa na Serikali lakini bado utekelezaji wake ni mdogo kwenye halmashauri zetu zote.

Je, Serikali ina mkakati wa kusimamia mwongozo huu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali haioni haja sasa ya kutunga sheria ya kuhusu jambo ili basi kuwanusuru wanafunzi wetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba huu mwongozo unasimamiwa na jukumu letu sisi kama Ofisi ya Rais-TAMISEMI, ni kufuatatilia utekelezaji wa mwongozo huu na tathmini yake. Kwa hiyo, niseme tu tutarudi tena tutawaagiza Maafisa Elimu kuhakikisha kwamba agizo la Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu la wanafunzi wote waliokatishwa masomo wanarudi shulenii linatekelezwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu sheria, tumelipokea wazo hili ni jema, na sisi kama Serikali tukishirikiana na Bunge tutafanya mchakato kuhakikisha kwamba sheria hiyo inaletwa Bungeni ili tuweze kuwalinda Watoto hao ambao wameacha shule. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swalii lake.

Na. 22

**Urejeshaji Mikopo Inayotengwa na Halmashauri Nchini**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 ni fedha kiasi gani kwa ajili ya vijana, akinamama na watu wenye ulemavu zimekopeshwa na kurejeshwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa mikopo inayotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2020 Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ilitoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 133. Katika kipindi hicho jumla ya shilingi bilioni 92.21 sawa na asilimia 69.32 zilirejeshwa kutoka kwa vikundi vya wanufaika.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBA**S: Mheshimiwa Spika, kwanza kutokana na majibu haya naomba nimpongeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Hanifa Suleman Hamza ambapo mwaka jana yeye amefanikisha kupeleka mikopo ya asilimia mia moja ya shilingi bilioni 3.1 kwa watu wa Kinondoni, nimpongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, swali langu, kwa kuwa marejesho yanaonekana hayakuwa asilimia mia moja kuna asilimia 31 ya fedha za mikopo hazijarejeshwa. Je, Serikali ipo tayari kufanya *performance audit* ili kuweza kujua kama fedha hizi kweli ziliwafikia walengwa na sababu ya kutokurudishwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali iko tayari kufanya utafiti kujua kwamba fedha hizi zinapopelekwa kwa walengwa hakika zinawafikia na zinabadilisha Maisha yao kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano marejesho yalikuwa asilimia 69.32 na Serikali ilifanya *performance audit* kwa kuhakikisha kwamba tunaita halmashauri zote 184 na kuona mtiririko wa mikopo kwa miaka yote mitano.

Mheshimiwa Spika, maelekezo tuliyoyatao Serikali ni kuhakikisha tunabainisha vikundi vyote ambavyo vilikopeshwa na vilikuwa havikurejesha marejesho hayo na virejeshe marejesho hayo. Naomba nimhakikishie

**14 SEPTEMBER, 2022**

Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari marejesho yanakwenda vizuri, kwa vikundi vyote ambavyo vilikopa na vilikuwa havijarejesha.

Mheshimiwa Spika, pili, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwanza tumeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kikopeshaji wa mikopo wa asilimia kumi, na halmashauri zote zimelekezwa kuingiza vikundi vyote vilivyokopeshwa na ambavyo havijarejesha kwenye mfumo wa kielektroniki ambao tutaufutilia kila siku na kuona kila hatua ya marejesho ya fedha hizo. Kwa hiyo, mpango huu wa asilimia kumi umeboreshwa kwa kiasi kikubwa na marejesho yanakwenda vizuri. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Samwelii HHayuma Xaday, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Regina Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Samwelii HHayuma naomba swali la lipatiwe majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Swali namba Mheshimiwa, Mheshimiwa Regina Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, swali namba 23.

Na. 23

**Serikali kufanya Utafiti Ziwa Bassotu**

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti wa kujua sababu za kusambaa kwa maji ya Ziwa Bassuto na kuhama kwa samaki kwenye Ziwa Eyasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibeni swali la Mheshimiwa Samwelii Hhayuma, Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeona hakuna haja ya kufanya utafiti wakujua sababu ya kusambaa kwa maji na kuhama kwa samaki ziwa Bassuto. Sababu kuu ni kujaa maji wakati wa mvua nyingi, ziwa hilo ni dogo halina uwezo wa kuhifadhi maji mengi yanayosababishwa na mvua nyingi. Aidha, maji hayo hutawanyika na kuingia Ziwa Eyasi na kwa kuwa Ziwa Bassuto lina viumbe mbalimbali ikiwemo samaki, maji hayo yanapoingia kwenye Ziwa Eyasi huingiza na viumbe mbalimbali wanaoishi kwenye Ziwa Bassuto ikiwemo samaki. Hali hii inasababisha wananchi wanaotegemea samaki wa Ziwa Bassuto inawabidi kupata samaki hao kwenye Ziwa Eyasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa viongozi wa Wilaya ya Hanang kuendelea kuhamasisha wananchi kuhifadhi vyanzo vyta maji ikiwemo Maziwa ya Bassuto na Ziwa Eyasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, mwaka 2020 Mheshimiwa Waziri wa Mazingira alifanya ziara kule Ziwa Bassuto na aliahidi kwamba atatumia timu ya wataalam ili waje kufanya tathmini kuona namna gani wanaweza kudhibiti madhara yanayoendelea kuwapata wananchi wa eneo hilo. Lakini kwa majibu haya ya Serikali sasa wananchi wategemee nini?

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili, ni lini Serikali sasa itatafuta fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya Ziwa Bassuto kwa sababu wananchi wale wanaendelea kupata madhara makubwa ili kuepuka yale madhara yasiendelee kuwapata wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibeni swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge Regina Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina kauli mbili, kauli ya Serikali ni kauli moja, sasa katika hili namuomba Mheshimiwa Mbunge, twende na hii kauli ya kwamba kwa sasa hivi Serikali hatujawa na mpango wa kufanya kama vile

Mheshimiwa anavyosema kwa sababu kama ambavyo tumeeleza katika jibu la msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wa fedha nadhani hili sasa atupe muda tuona namna ya kukaa na kushirikiana na baadhi ya Wizara zingine za kisekta, ikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Wizara yetu ya Mazingira ili kuona namna ambavyo tunaweza kujadili kwa pamoja na baadaye tukatafuta fedha kwa ajili ya ziwa hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresto, Mbunge wa Viti Maalum sasa ulize swalii lake.

Na. 24

### **Serikali Kutatua Changamoto ya Matukio ya Mauaji**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali katika kutatua changamoto ya wimbi kubwa la mauaji hapa nchini?

**SPIKA:** sioni nani yupo au wewe ndio una..., haya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA  
K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresto, Mbunge Wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na ongezeko la matukio ya mauaji hapa nchini. Matukio mengi yanababishwa na wananchi kwanza kujichukulia sheria mikononi mwao, lakini pili ni vivu wa mapenzi, lakini zaidi migogoro ya ardhi, ulevi na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti wimbi hili tuliunda tume maalum ya kuchunguza na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua, pamoja na kuchukua hatua za kisheria kama zilivyopendekewa na tume tuliyoienda,

Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa kuwashirikisha viongozi wa siasa, dini, wazee wa mila na watu wanaoheshimika kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi, katika kutatua migogoro na migongano katika jamii. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini sasa taarifa hiyo ya tume itawekwa wazi kwa wadau na wananchi wote kuifahamu na kuijua?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, migongano na migogoro hii imesababisha wananchi kujichukulia sheria mkononi, na je, Serikali haioni haja ya kuja na mkakati wa pamoja kama Serikali mkakati wa haraka kuhakikisha namna gani tunakabiliana na hii changamoto ya watu kujichukulia sheria mkononi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ambavyo tumesema katika jibu letu la msingi kwamba kufuatia kuongezeka kwa matukio haya tayari Serikali imeunda tume ama timu maalum kwa ajili ya kuchunguza na kuweza kuleta majibu.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli timu iliundwa na taarifa zimekuja, majibu yamekuja lakini bado Serikali tunaangalia kama kutakuwa kuna haja ya namna ya kuweza kutoa hizi taarifa kwa jamii basi zitatolewa. Kama hatuna namna basi tutaona namna nyingine ya busara zaidi ya kuwafikishia majibu wananchi ya tume hii iliyoundwa kwa ajili ya kuchunguza hayo matukio.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusiana na mkakati, ama bila ya shaka kuna haja ya kuwa na mkakati na mkakati upo, na mkakati wa kwanza katika hili ni kuendelea kuwaelimisha watu. Moja kuhusiana na masuala haya ya kishirikiana, kwamba si kila ambaye anakuwa na sababu hizo maana yake auliwe. Lakini kingine ni kushurutisha sheria kwamba watu lazima wafuate sheria na wasijichukulie sheria ama hatua mikononi mwao. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini hili tatizo pamoja na hatua mnazozichukua bado linaendelea kukua. Sasa sijui ni kwa sababu polisi ndio wanaoviambia vyombo vya habari, kwa hiyo, inakuwa ni habari nzito fulani hivi halafu mwingine ambaye hajui kama hilo jambo linawezekana anafikiri pengine na mimi naweza kufanya.

Sasa hebu mjaribu kuangalia zile hatua za kawaida kabisa, pengine haya matangazo nayo yanaleta hizo changamoto, yaani hata ambaye hajui anajua sasa pengine kama limetokea kule basi na mimi, kwa sababu mnaeleza namna liliwyotokea na nini na sababu, sasa tukitumia tu sababu ya wivu wa mapenzi na nini.

Mimi nafikiri mtafute hizi sababu za kawaida kabisa na mtuulize sisi watu wa kawaida kabisa, tunafikiri hilo jambo linaweza kumalizwa namna gani. Kwa sababu kadri linavozidi kuzungumzwa utasikia leo huku, kesho, huenda linatembea kwa sababu linazungumzwa na watu wazito, naona Waziri wa Nchi anataka kusimama pale. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**  
Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Naiibuu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi tumezungumza umuhimu wa wadau wote kushiriki katika kutafakari juu ya jambo hili, kwa sababu utafiti umeonesha kwamba sababu kubwa ni hizi zilizosemwa, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina, ugomvi wa masuala ya mipaka ya ardhi, lakini eneo kubwa sana ni kugombea mali na uhalifu mwingine wa kawaida unasababisha mauaji.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane sana na maoni yako kwamba kwa kweli hili jambo liko haja ya kushirikisha wadau wote. Law enforcers na wao wajiuulize au tuijuulize tumetimiza wajibu wetu sawasawa? Kama kunatokea hasira kwa wananchi kuchukua hatua mkononi, kwa nini wanachukua hatua mkononi, ni wapi hapako sawa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli nikubaliane sana pamoja na maoni haya mazuri uliyoyatoa kwamba Serikali inayohaja wa kulichukua hili suala kwa uzito wake mkubwa. Niongeze kwamba pia maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano imekuwa chachu kubwa inayochochea upashanaji habari umekuwa mkubwa na ushabiki ni mkubwa sana wa matukio mabaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunalichukua hili pia na kuona kwamba ni lazima pia tutafute mfumo rasmi na tushirikishane kweli kabisa mpaka kwa

kiwango cha chini kama ulivyosema kuhakikisha kwamba tunapunguza au kutatua tatizo la mauaji yasiyokuwa na sababu. Ni kweli mauaji yanakuwa kama yameongezeka kwa kiasi fulani. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi tunakushukuru kwa majibu hayo. Kwa hiyo mimi naamini kwamba Polisi eeh Waziri Polisi muwaambie walitazame hili jambo kama wanahaja ya kuwatangazia wananchi kila haya mambo yanapotokea kama kuna hiyo haja na je, ni habari au siyo habari.

Sisi tunajua mnafanya mambo mengi ili nchi yetu iwe salama na hamtuambii. Sasa hili tujue kama ni muhimu kuambiwa au siyo muhimu, kama siyo muhimu basi tuachenii tuwe tu yaani wawe wanajua wale wanaohusika hilo eneo lao basi, sisi wengine fusijue kwa sababu yaani muwe na taarifa hizo, lakini mnapoendelea kuwaambia wananchi pengine inaleta changamoto kubwa kama ulivyosema.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri umeenda kukaa lakini kuna swali lingine la Wizara yako bado. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

Na. 25

### **Kesi za Wakulima Zilizofanyiwa Kazi**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, ni kesi ngapi za wakulima kulishiwa mazao yao zimeripotiwa na ngapi zimepelekwa mahakamani katika Wilaya ya Kilosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA  
K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kesi zilizoripotiwa polisi za wakulima kulishiwa mazao yao Wilayani Kilosa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 ni kesi 1,403. Katika kesi hizo zilizofikishwa mahakamani ni 1,037 na zilizotolewa hukumu na mahakama ni kesi 540.

Mheshimiwa Spika, vilevile kesi 356 ziliondolewa ama kufutwa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nikiri kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana Wilayani Kilosa na nimpongeze DC wa Wilaya Kilosa Alhaji Majid Ahmed Mwanga kwa kazi kubwa ya kupunguza na kuondoa kabisa katika baadhi ya maeneo migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo kwa namba hizi ambazo naziona na ripoti nyingi za matatizo ya wakulima kulishiwa mazao yao katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza matatizo haya?

Pili, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kulichukulia jambo hili kama janga la kitaifa Wizara ya Mambo ya Ndani ikae na Ofisi ya Waziri Mkuu kuona namna bora ya kulichukulia suala hili kama janga? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi na vyombo vingine vikiwemo vya Mahakama kwa kweli tumechukua hatua nyingi na tofauti, moja tumegundua kwamba bado kuna watu uelewa wao ni mdogo katika hili. Kwa hiyo cha kwanza ni kuendelea kuwapa taaluma wananchi juu ya suala hili, lakini kingine tunaendelea kutoa maelekezo kwa baadhi ama kwenye vyombo mbalimbali ikiwemo watu wa halmashauri, watu wa mijji na majiji ili kuendelea kutusaidia kulilea suala hili ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanaondoka kabisa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwengine nikiri kwamba kweli hili suala ni janga na kwa sababu linalrudisha nyuma hali za wananchi zikiwemo hali za kiuchumi na mambo mengine kwa hiyo kutokana na hali hii ndiyo maana sasa tukaona pia bado kuna haja ya kuchukua baadhi ya mikakati na hatua

hizi. Kwa hiyo nikiri kwamba hili ni janga na kwa sababu linawaathiri sana wananchi.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge huyu anajibu kwa niaba ya Wizara husika kwa hiyo nawaona mliosimama. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Barabara ya Dar Es Salaam - Morogoro**

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa kiwango cha lami njia nane barabara ya Dar es Salaam hadi Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imetangaza zabuni kwa ajili ya *Expression of Interest* kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka Kibaha – Mlandizi – Chalinze hadi Morogoro yenye urefu wa kilometra 205 kwa utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construct and Finance (EPC + F)*. Gharama za ujenzi wake zitatolewa na Serikali au na sekta binafsi (PPP) kwa utaratibu wa Jenga, Endesha, Rudisha (*Build Operate and Transfer*) ambapo sekta binafsi itajenga barabara hii kwa fedha zake na kuiendesha hadi pale itakaporejesha fedha zake kuititia tozo za magari. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, swali la nyongeza

**MHE. SYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya TAMCO - Mapinga - Kibaha inayojengwa kiwango cha lami imekuwa inasuasua kwa muda mrefu, lakini pamoja na hilo wale wananchi waliopisha ujenzi wa barabara hii hawajalipwa fidia hadi leo kwa maana ya wananchi wa kata ya Tangini na Pangani. Je, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia kama kwa mujibu wa sheria ulivyo?

Swali la pili barabara ya zamani kwa maana ya Dar es Salaam - Morogoro inayoanzia sasa Picha ya Ndege mpaka Mlandizi ni barabara ambayo ni kimbilio la wasafiri na wasafirishaji hasa barabara hii kubwa inapopata tatizo la ajali na kufunga barabara.

Sasa kwa umuhimu huo ni lini Serikali itaweka nguvu kurekebisha barabara hii ili iweze kupidika na kusaidia kutokuondoa msongamano wa barabara kubwa wakati kunapokuwa na ajali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya TAMCO - Mapinga kumekuwa na ujenzi wa kusuasua na pia baadhi ya watu hawakulipwa fidia. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifahamu jambo hili na inalifanya kazi kuhakikisha kwamba hawa watu wanalipwa na ujenzi huu unakamilika kwa muda kwa hii barabara ya TAMCO - Mapinga ambayo ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu barabara aliyosema ambayo itakuwa ni msaada mkubwa sana kwa ajili ya kusaidia panapotokea changamoto kwenye eneo hili la picha ya ndege naomba nichukue suala la Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa maana ya Wizara kupitia TANROADS tutalifanya kazi kuhakikisha kwamba barabara hii inaboreshwa iwe ni msaada pale ambapo barabara kuu inapopata changamoto inatusaidia kuhakikisha kwamba hatupati changamoto kubwa kwa maana ya kukwama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Bujela -Masukulu na kuekelea Matebe na kutokea Kyela ni barabara muhimu sana kiuchumi kwa maana kokoa, chai inatoka maeneo hayo. Serikali haioni umuhimu wa kuijenga angalau kwa lami ili kuweza kusaidia uchumi wa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara zote tungependa tuzijenge kwa kiwango cha lami, lakini hatuwezi kuzijenga zote kwa wakati mmoja kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italichukua na ni mpango kwamba hizi barabara ikiwemo na hii barabara aliyoitaja kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini kikubwa itategemea tu na uwezo wa bajeti ya Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava samahani.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Ndala kwenda Mwawaza kuliko na Hospitali ya Rufaa. Je, ni lini itaanza kutekeleza mpango huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii itaanza kujengwa pale tu ambapo fedha itapatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hiyo barabara muhimu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi.

Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Namanyere - Kilando mpaka Kipili kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Namanyere hadi Kipili ambayo inaenda bandarini ni barabara muhimu na barabara hii iko kwenye usanifu, kwa hiyo baada ya kukamilisha usanifu wa kina Serikali itatafuta fedha ili ianze kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga swalii la nyongeza

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swalii.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kuuliza barabara ya kutoka Masumbwe kwenda Geita Makao Makuu ya mkoa ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masumbwe kwenda Geita imeshafanyiwa usanifu wa kina na sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, swalii la nyongeza

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri ni lini barabara ya Bonyokwa - Kimara itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bonnah, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba amefika mara kadhaa Wizarani na Mheshimiwa Waziri pamoja na

**14 SEPTEMBER, 2022**

TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam wamemuhidi na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo kutoka Bonyokwa kwenda Kimara ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga Mbunge wa Itilima swalii lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

Na. 27

**Ujenzi wa Barabara ya kutoka Sibiti – Kisesa – Itilima – Bariadi – Salama – Sayaka hadi Kisamba**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO K.n.y. MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Sibiti – Kisesa – Itilima – Bariadi – Salama - Sayaka hadi Kisamba kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Sibiti hadi Mwandoya Junction ama Loboko ni sehemu ya barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilometa 389 ambayo imepangwa kujengwa kupitia utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction & Financing (EPC + F)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Mwandoya Junction hadi Kisesa – Itilima – Bariadi yenye urefu wa kilometa 100, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea na sehemu ya kutoka Bariadi – Salama hadi Magu kupitia Ng’ haya (kilometa 76) ipo katika hatua ya manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swalii la nyongeza

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, mimi nishukuru tu kwamba majibu ni mazuri, lakini siyo majibu ya swalii la msingi.

Swali la msingi linauliza ni lini barabara hii inaanza kujengwa?

Kwa hiyo swali langu mimi la kwanza la nyongeza ni lini barabara hii inaanza kujengwa? Na swali la pili ni lini barabara hii inaanza kujengwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la msingi ni lini Serikali itajenga barabara kutoka Sibiti hadi Salama, Sayaka, Kisamba nimejibu kwamba ili uanze kuijenga barabara lazima ifanyiwe upembusi yakinifu na usanifu wa kina, na katika hiyo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge kuna eneo ambalo tumesema kilometra 71 ipo kwenye mpango wa EPC na tayari taratibu zimeshaanza.

Kwa hiyo, ni kwa maandalizi ya kuijenga na vipande ambavyo vimebaki kutoka Mwandoya Junction ambapo ni Goboko kwenda Kisesa hadi Itilima mkandarasi ameshapatikana kwa ajili ya kuanza kuifanya usanifu, hayo yote ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami na baada ya kuikamilisha ndipo sasa barabara hiyo tutajua gharama za ujenzi na tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nami naomba niulize swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inayotokea Duto kuelekea Nyashimo kupitia Shigala, Malili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Duto - Nyashimo itajengwa tu pale ambapo fedha na bajeti itaruhusu kwa sababu tayari ipo kwenye mpango kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela swali la nyongeza

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ni lini barabara ya Mnivata kwenda Masasi itajengwa ni kwa nini haijengwi wakati pesa bado ipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote ambaa barabara hii inapita Mnivata - Newala hadi Masasi yenye urefu wa kilometra 160 kwamba tayari taratibu zote zimeshakamilika kwa maana ya maandalizi ya zabuni na barabara itakuwa na loti mbili na katika ujenzi huu pia Daraja la Mwiti limeunganishwa na tayari tunachosubiri ni wenzetu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika watupe no objection kwa sababu ndiyo wanaojenga hii barabara. Kwa hiyo, muda si mrefu barabara hii itatangazwa kwa ajili ya kujenga yote kilometra 160. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amekuwa akiniahidi sana kila mara kwamba pesa ya upembuzi yakinifu itakapopatikana barabara ya kutoka Kahama - Nyang'hwale itawekwa ndani ya mpango.

Je, ni lini pesa hiyo itapatikana na kuwekwa ndani ya mpango hiyo barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, swali lake sijalisikia vizuri barabara alizozitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Barabara kutoka Kahama - Nyang'hwale - Busisi umekuwa ukiniahidi kwamba itakapopatikana pesa barabara hiyo itawekwa ndani ya mpango wa upembuzi yakinifu.

Je, ni lini pesa hiyo itapatikana na barabara hiyo kuwekwa ndani ya mpango wa upembuzi yakinifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Nassor Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuweze kuangalia kitabu cha bajeti ili tuone. Naamini kwamba hii barabara itakuwa imetengewa fedha kwa ajili ya mpango kwa mwaka huu. Na kama kutakuwa haijatengwa basi tuangalie Wizara nini cha kufanya ili kuiwekea kwenye mpango wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hii. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi swalii la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwakuwa Serikali imetangaza zabuni ya ujenzi wa barabara ya Morogoro, Njombe boda walau kwa kilometra 100 route one na route two. Je ni lini kazi hii itaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ipo kwenye hatua za manunuzi. Najua Mheshimiwa Mbunge anaifuatilia; ipo kwenye hatua za manunuzi kwa ajili ya kuanza kujengwa hiyo barabara kwa hivyo ipo kwenye hatua mbalimbali za manunuzi ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swalii la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto Munze Mwingunge yenyeki kilometra 63 imekuwepo kwenye mpango wa utekelezaji kwa maana ya ujenzi katika kiwango cha lami kwa mwaka

2021/2022. Mwaka 2021/2022 haikuweza kutekelezwa. Je, nini mpango wa Serikali kwa mwaka 2022/2023 kuhakikisha kwamba unatekelezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto hadi Lalago kama alivyotaja hizo kilometra 62 imepewa Bajeti kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango hiki; kwa hiyo tusubiri tutakapoanza utekelezaji wa bajeti ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 28

**Miundombinu kwa watu wenyewe Ulemavu katika vyombo vyatofauti**

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenyewe ulemavu katika vyombo vyatofauti ikiwemo mabasi ya mwendokasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisimamia upatikanaji wa huduma bora na salama kwa watumiaji wa usafiri kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wenyewe ulemavu. Serikali imekuwa ikizingatia mahitaji ya makundi maalum hasa wenyewe ulemavu katika ujenzi wa miundombinu ya usafiri ikiwemo miundombinu ya mabasi ya mwendokasi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya mabasi ya mwendokasi inayotumika sasa na inayoendelea kujengwa imezingatia watu wenyewe mahitaji maalumu. Aidha, mabasi yote ya mwendo kasi yamezingatia watu wenyewe mahitaji maalumu hususan wenyewe ulemavu, wazee na wajawazito. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis swali la nyongeza.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Hata hivyo, pamoja na majibu hayo mazuri pia napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, ni maeneo gani mahsusи ambayo Serikali imeyazingatia katika utumiaji watu wenyе ulemavu katika mabasi hayo?

(ii) Kwakuwa mmesema mmezingatia; je, ni kwanini hakuna utaratibu maalum ambao umezingatia watu wenyе ulemavu wakati wanapofika vituoni na wanapotaka kutumia usafiri huo kwa kupanda mabasi hayo? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza tukiri kwamba hapо awali miundombinu mingi ambayo ilikuwa ikijengwa ilikuwa haizingatii sana mahitaji ya watu wenyе ulemavu ikiwa ni pamoja na kwenye hospitali, shule na majengo mengi. Hata hivyo, sasa imekuwa ni utaratibu wa Serikali kwamba miundombinu yote inayojengwa, iwe majengo iwe wapi lazima izingatie watu wote wenyе mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala la usafiri; na tumetoa mfano wa mwendokasi; Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba hata ujenzi wa barabara na hasa kwenye vituo mtu ye yeyote mwenye mahitaji maalum, na hasa watu wenyе ulemavu, yale mabasi yamejengwa na yametengenezwa kiasi kwamba yapо kwenye usawa. Kwamba anatoka anaingia, na hata kama ana Wheelchairs ana uwezo wa kuingia kwenye mabasi hayo katika vituo vyote. Lakini pia kwenye mabasi kumekuwa na nafasi na kumekuwa na viti maalum vya watu wenyе mahitaji hayo; kwa maana ya watu wenyе ulemavu wazee na hata wajawazito; na hata rangi ya viti imekuwa ni tofauti. Pia kumekuwa na utaratibu wa watu kuingia kwa foleni

Mheshimiwa Spika, pengine nitumie nafasi hii kusema kwamba, kunapokuwa na watu wenyе ulemavu wanaposafiri wanatakiwa wawe na mstari wao na wawe wa kwanza kuingia, na viti vyao visikaliwe na watu wengine. Sasa, suala hili tunataka pia liende kwenye mabasi mengine ya umma, kwa mfano daladala na hata yanayokwenda mikoani. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry William Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwakuwa Serikali sasa inaandaa kanuni za ujenzi, kwa maana ya *Billing regulation*, nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha majengo yote yanayojengwa kwenye nchi yetu yanazingatia mahitaji wa watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali, kwa sasa majengo na ujenzi wowote unajengwa wa Serikali lazima uzingatie watu wenye mahitaji maalum. Na kwa suala la hizo *regulation* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lipo na linaendelea kufanyiwa kazi. Lakini hadi sasa hivi hakuna ujenzi wowote unaojengwa bila kuzingatia hayo mahitaji maalum. Ahsante (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe Mbunge wa Mombasa sasa aulize swali lake.

Na. 29

#### **Kuwawezesha wanawake wanaozalisha pombe za kienyeji**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwanunulia mitambo ya kisasa na kuwapa mikopo wanawake ambao wanazalisha pombe za kienyeji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushuru. Kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe Mbunge wa Jimbo la Mombasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uzalishaji na uuzaji wa pombe za kienyeji unaofanyika vijiji na katika baadhi ya maeneo ya mijini. Kwa sasa Serikali haijaanzisha mpango wa kuwanunulia mitambo ya kisasa na kuwapa mikopo wanawake wanaozalisha pombe za kienyeji. Hata hivyo, wanawake

wajasiriamali wataendelea kupata mikopo kuitia mifuko na programu za uvezeshaji wananchi kiuchumi, nakushukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa wenye maswali unasi mama haraka ili nikuone la sivyo nakupita ninamwita Mbunge mwingine maana sitajua kama unalo swali. Mheshimiwa Condester Sichalwe swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER MICHAEL SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nimesikiliza majibu ya Serikali siyo mbaya, ni hivyo hivyo. naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba na kwamba wanatambua uzalishaji ambao upo vijiji Je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kubadilisha Sheria ya Vilevi na Vilevo (The intoxication Liquors Act) ambayo ni ya mwaka 1968 na marekebisho yake ya mwaka 1978. Hauni kuna haja; kwamba, sheria hii ikibadilishwa inaweza ikaendana na mazingira tuliyonayo sasa kwa ajili ya kuendelea kuwasaidia wananchi waliopo kule vijiji? Kwasababu Sheria iliyopo sasa hivi inaongelea sana mambo ya leseni.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kulingana na llani yetu ya Chama cha Mapinduzi kusitiza uchumi wa viwanda Je, Wizara hii haioni sasa ipo haja kabisa ya kuwapa SIDO jukumu la kuwasaidia wananchi hawa wanawake wa vijiji na sehemu zote, kuwapa elimu, kupata takwimu halisi ili waweze kuwasaidia kuboresha hizo pombe zao za kienyeji na ziweze kuwa kwenye viwango na ziweze kuuzwa nje ya nchi? Ahsante. (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester Sichalwe Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, na ninadhani ni mawazo mazuri, kwamba tuangalie namna ya kuitia sheria zetu za vileo na vilevi ili iweze kuendana na uhalisia wa sasa. Nadhani hii kama Serikali tuichukue. Na kwasababu ni wajibu wetu kama Wabunge kutunga sheria hizi basi na sisi tutalifanyia mchakato ili tuweze kuona uhalisia kama kuna uhitaji wa kubadilisha sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kuitia SIDO Serikali inaboresha baadhi ya mitambo lakini pia na kuboresha mikopo kwa ajili ya wajasili amali mbalimbali ikiwemo wanawake. Na sasa labda tutaangalia mahsus kwa ajili ya hawa wazalishaji wa pombe za kienyeji ambao huenda watataka teknolojia

mahsus au mfuko maalum ili waweze kuwezeshwa kuzalisha pombe ambazo zina viwando badala ya kuendelea kuzalisha hizi pombe ambazo tunaita ni za kienyeji. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Uingizaji na utengenezaji wa vipodozi fake**

**MHE. JULIANA D. MASABURI** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kufanya ukaguzi wa kudhibiti uingizaji na utengenezaji wa vipodozi fake nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania yaani TBS imeendelea kudhibiti uingizaji na utengenezaji wa vipodozi visivyokidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Na. 2 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka 2019. Pia Serikali imeendelea kudhibiti bidhaa *fake* kupitia Tume ya Ushindani (FCC) kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu hayo ya Serikali ambayo bado hayaridhishi napenda kuiuliza Serikali; tangu nimeandika hili swali najua kuna shirika la TBS najua kuna Tume ya Ushindani; lakini bidhaa *fake* hasa vipodozi, vyakula vimezidi kuzalishwa nchini na kuingizwa kwa kasi ya juu. Naomba majibu sahihi ya Serikali nini wanapanga kudhibiti bidhaa *fake*? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli changamoto ya bidhaa *fake* ni ya kudumu. Na kwa namna ambavyo tunajua lazima tuendelee kudhibiti. Serikali inaendelea kufanya juhudhi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya changamoto tuliyonayo ni upungufu wa watumishi katika taasisi zetu hizi za TBS na FCC. Hata hivyo tunaendelea kuboresha ili kupata watumishi wa kutosha. vilevile tunaweka nguvu au mkazo kwenye elimu kwa umma, kwasababu bidhaa *fake* au bidhaa *hizo* au vipodozi hivi vinavyoingizwa ni kwasababu ya mahitaji ambayo Watanzania wanahitaji. Kwa hiyo, tukiwapa elimu sahihi maana yake vitakosa soko au uhitaji wa bidhaa *hizo*. Kwa hiyo tutaendelea kutoa elimu pamoja kuimarisha zaidi kwa kuhakikisha tunapata watumishi wa kutosha ili wasaidie kudhibiti mianya ambayo inatumika kuingiza bidhaa hivi *fake* na vipodozi ambavyo vinakosa sifa za kutumika kwa ajili ya kudhibiti soko la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la msingi la vipodozi *fake* kweli ni janga la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba vipodozi vinapendezesa (beautifying) lakin kazi kubwa ya vipodozi ni za kiafya katika ngozi na mwili. Swali langu la msingi ni kwamba, ni lini Serikali itahamisha bidhaa za vipodozi kutoka Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara kwenda Wizara ya Afya ambapo kuna wataalam wa vipodozi hivyo ili tuweze kulinda afya ya jamii? Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Florent Kyombo (Mb) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika ni kweli vipodozi ni sehemu ya bidhaa ambayo ipo kwenye kundi la dawa. Sasa, kwasababu ni ushauri Serikali tunalichukua ili tuweze kuona namna gani tutaliweka hili suala liweze kutumiwa kwenye sehemu sahihi kama sio Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwakuwa tumekuwa tukishuhudia kila mara vitu hivyo au vipondozi hivyo, vyakula hivyo vikichomwa katika maghara na kwa gharama kubwa sana. Je, ni nani anayegharamia, kwasababu yule aliyenyang'anywa tayari ameshafilisika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond (Mb) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwamba kwa utaratibu anayetakiwa kugharamia uharibifu wa bidhaa hizo fake au vipodozi ni yule ambaye ameingiza, kwa maana ya aliyejuki sheria ya uingizaji wa bidhaa, kwasababu zidhaa zote ambazo zinaruhusiwa kuuzwa katika masoko ya Tanzania hasa vipodozi lazima viwe vimesajiliwa. Kwamba, kama vimeingizwa kinyume na sheria hiyo yeye ndiye atakayetakiwa kulipa ili kuhakikisha anafidia gharama hizo za kuharibu vipodozi, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Felista Deogratius Njau Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Kuwezesha Mradi wa Kilimo cha Mpunga Chita JKT**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kifedha JKT ili iweze kutekeleza kwa ufanisi mradi mkubwa wa kilimo cha mpunga Chita JKT – Morogoro na Shamba la Mngeta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA  
K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kifedha kila mwaka ili liweze kutekeleza kwa ufanisi shughuli zake, ikiwa ni pamoja na miradi ya kilimo, ikiwemo mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika shamba la mpunga lililopo Chita mkoani Morogoro na Shamba la Mngeta. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilitoa Shilingi 4,000,000,000 ambazo zimetumika kununulia zana na vifaa vya kilimo kwa ajili ya shamba la Chita. Aidha, katika Mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi 4,000,000,000 katika bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kumalizia awamu ya kwanza ya ujenzi wa skimu ya umwagiliaji wa ekari 2,500 huko Chita.

Mheshimiwa Spika, Katika kuliendeleza shamba la Mngeta lenye ekari 12,000, kiasi cha Shilingi 11.5 zinahitajika kwa ajili ya ununuzi wa zana, matengenezo na maboresho ya miundombinu ya uzalishaji, na gharama za uendeshaji. Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na Wizara ya kilimo ili kuona uwezekano wa shamba hili la Mngeta, kuwa sehemu ya mpango wa skimu za umwagiliaji. Taratibu za ndani zinaendelea ili kuwasilisha maombi ya fedha Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau swalii la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwakuwa eneo hili kuna baadhi ya maeneo tayari yana miundombinu ya umwagiliaji na miundombinu hii ipo ardhini na ikikaa kwa muda mrefu inaweza kuharibika nataka kujua;

Je, ni lini hasa Serikali itatenga kiasi hichi cha Shilingi bilioni 11.5 ili kunusuru miundombinu hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwakuwa maeneo mengi nchini katika mikoa yetu yana madhari yanayofanana na Mngeta na maeneo ya Chita.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati sasa wa kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji kwa pamoja ili kupambana na uhaba wa chakula pamoja na kuendeleza usalama wa chakula nchini? (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana kwa kazi nzuri anayoifanya katika mkoa wake, lakini pia kwa hamu aliyonayo ya kuona kwamba siku moja jeshi hili linazidi kusonga mbele hasa katika shughuli za sekta hizi za kilimo. Hongera sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza mchakato na ukweli huu unapatikana katika jibu langu la msingi; ukiangalia kwenye mstari wa mwisho, utaratibu wa ndani unaendelea ili kuwasilisha maombi ya fedha Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa hiyo, suala hilo la upatikanaji wa hizi Shilingi bilioni 11 tayari utaratibu tumeshauanza na muda wowote tunategemea kupata hizi fedha na tukizipata tutakwenda kufanya kile ambacho Mheshimiwa ameshauri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kweli tumegundua na utafiti unaonesha kwamba shughuli za kibinadamu zikiwemo za kilimo, mifugo, uvuvi, madini na nyingine, kwa kweli zimekuwa zinaathiri sana vyanzo vya maji, athari ambazo mwisho wa siku zinakwenda kuharibu shughuli za kilimo na kufanya shughuli hizi zisiende vizuri.

Mheshimiwa Spioka, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba tumeshakaa na tutaendelea kukaa kufanya stadi mbalimbali kwa kushirikiana na wenzetu wa Tawala za Mikoa kwa maana ya wa Halmashauri, Vijiji na wale wa Mamlaka ya Mabonde ili kuona namna ambavyo tunahuisha vyanzo vya maji kwa ajili ya kuboresha shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Hitaji la Kituo cha Kupoza Umeme – Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka Kituo cha kupoza umeme Igunga?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANESCO imebaini uhitaji wa vituo vya kupoza umeme katika Wilaya zote Tanzania Bara zenyet uhitaji huo. Aidha, imeweka mpango wa ujenzi wa vituo hivyo kulingana na uhitaji kuanzia mwaka huu wa fedha 2022/2023. Kituo cha Kupoza umeme cha Igunga kitawekwa katika mpango wa ujenzi wa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha huduma ya umeme katika maeneo ya Wilaya ya Igunga na Nzega, Serikali inaendelea na mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lusu kilichopo Wilayani Nzega kutoka MVA 15 132/33kV hadi MVA 60 132/33kV. Upanuzi huu, utakamilika ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Wizara ya Nishati kwa kituo hiki cha kupoza umeme ambacho kinatarajiwa kujengwa kwenye Kata ya Mbutu iliyopo Jimbo la Igunga ilikuwa ifanyike kwa mwaka huu wa fedha, lakini naona Serikali wameamua kuisogeza tena mwakani; ukiangalia imekuwa na changamoto kubwa kwa sababu tunapata umeme kutoka Lusu, Nzega ambayo ni kilometra

100. Sasa je, Serikali haioni kuchelewa kujenga kituo hiki ni kudumaza uchumi wa wananchi wa Jimbo la Igunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa George Ngassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatilaji wake wa mara kwa mara. Ni kweli Serikali ilikuwa imetoa ahadi ya kukijenga kituo hiki, lakini mwaka 2021 na mwaka huu wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia TANESCO imefanya upembuzi yakinifu katika maeneo yote Tanzania Bara kuona uhitaji halisi wa ujenzi wa vituo vya kupooza umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niseme kwamba upembuzi yakinifu ulipokamilika, tukabaini mahitaji kutoka maeneo mbalimbali na uhitaji wa haraka zaidi kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Kwa hiyo, Kituo cha Igunga hakijachelewa ila imeonekana kijengwe mwakani kwa sababu kuna wenyewe uhitaji mkubwa zaidi kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nivitaje vile vituo ambavyo vitajengwa mwaka huu ambavyo tayari vimepatiwa fedha katika ule mradi wetu wa grid stabilization project.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wewe taja kile cha kwake, hivyo vingine Wabunge watauliza na wenyewe kila mtu kwenye eneo lake. Tutajie cha kwake.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kitajengwa mwakani.

**SPIKA:** Mwakani kwa maana ya 2023/2024 au ni mwaka huu wa fedha? Sasa ili Mbunge aelewe, maana anaona imesogezwa mwaka, ni mwaka upi? Mwaka wa fedha au mwaka wa Januari – Desemba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni mwaka wa fedha wa 2023/2024.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Assa Makani, swalii la nyongeza.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa hali ya umeme ya Igunga, Julai 19, Mheshimiwa Waziri akiwa Biharamulo alieleza kwamba mnamo mwezi Septemba umeme wa gridi ya Taifa utakuwa umefika Kigoma. Sasa tupo mwezi Septemba, tunataka kujua hali ya umeme wa gridi ya Taifa: Je, umeshawasili Kigoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Assa Makanika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme wa gridi utafika Mkoani Kigoma mwezi huu Septemba kwa sababu ipo njia ya msongo kv 33 ambayo inakamilishwa mwishoni mwa mwezi huu inayotokea Nyakanazi kupita Kakonko – Kibondo Kwenda mpaka Kasulu. Kwa hiyo, umeme wa gridi kwa kuanzia utaingia mwezi Septemba katika Mkoa wetu wa Kigoma.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, swalii la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kumekuwa na changamoto ya katikakatika ya umeme katika Jimbo la Igalula lakini ukiuliza, unaambiwa changamoto hiyo inasababishwa na kusafiri kwa umbali mrefu wa nishati hii ya umeme: Je, Serikali haioni haja ya kujenga vituo vya kupooza umeme katika Kata ya Kigwa na Kizengi ili kupunguza adha ya kusafiri umeme na kupunguza changamoto ya katikakatika hii ya umeme?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Venant, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika huu mpango wa *grid stabilization project* kwa mwaka huu wa fedha, Tabora inavyo vituo viwili vya kupooza umeme ambacho kitajengwa pale Uhuru katika Wilaya ya Urambo na kingine kitajengwa Ipole katika Wilaya ya Sikonge. Kwa Mheshimiwa Venant kule Igalula nitaenda kuangalia kwenye mpango wetu wa ujenzi wa vituo vya kupooza umeme katika wilaya zenyehi mahitaji na nitamfahamisha ni lini Serikali imejipanga kukijenga katika eneo lake. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swalii la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwmaba amekitaja kituo cha kupoozea umeme Urambo: Je, anawahakikishiaje wananchi wa Urambo kwamba lini kituo hicho kinakamilika? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Margaret Sitta na wananchi wa Jimbo lake kwamba katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 kutoka katika Shilingi bilioni 500 ambazo zimewekwa kwa ajili ya uendelezaji wa gridi, vile vituo 15 vitakavyojengwa, na cha kwake cha pale Uhuru kitakamilika bila matatizo yoyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 33

### ***Migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji Mlimba***

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua migogoro ya wakulima na wafugaji katika Jimbo la Mlimba?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa changamoto mbalimbali zinazosabisha migogoro ya matumizi ya ardhi ikiwemo hiyo ya wakulima na wafugaji. Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha migogoro ya matumizi ya ardhi katika Mkoa wa Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero inatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kumilikisha ardhi kuitia Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi (*LTSP*) ambapo jumla ya vijiji 58 viliandalistiwa mipango ya matumizi ya ardhi na Hakimiliki za Kimila 150,006 zilisajiliwa. Kati ya vijiji hivyo 58, vijiji 32 vipo katika Halmashauri ya Mlimba ambapo jumla ya Hakimiliki za Kimila 41,797 zimesajiliwa na 30,699 zimechukuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza Serikali za Halmashauri kuhakikisha zinasimamia mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandalistiwa ili kupunguza uwezekano wa kuibuka au kuendelea kwa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni kudhibiti na kuimarisha mbinu za utatuzi wa migogoro kwa kutoa elimu kuitia mikutano ya wananchi kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi iliyowekwa kwa pamoja, kutungwa kwa Kanuni za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi na kuhimiza matumizi ya ardhi yenye tija.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta zitaendelea kudhibiti na kushughulikia migogoro na kuitafutia ufumbuzi iliyopo ili kuimarisha ustawi wa jamii baina ya wakulima na wafugaji. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali langu la kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ina vijiji 62; na katika mpango wa *Land Tenure Support Programme*, vijiji 30 tu vilifanyiwa kazi: Je, ni lini Serikali inakwenda kukamilisha kazi hii ya vijiji 32 vilivyobaki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari mara baada ya Bunge hili kuambatana nami kwenda kufanya ziara ndani ya Jimbo langu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kunambi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba kukiri mbele ya Bunge lako kwamba kweli ule mkakati ulipofanyika mara ya kwanza, yaani ile programme ya LSTP ulipita katika vijiji 32 ndani ya Halmashauri ya Mlimba ambayo ina vijiji 62. Nataka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumeshatenga fedha, basi tutakwenda kwa ajili ya kumalizia vijiji hivyo vilivyobakia kwa sababu programme hii ili kuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge kwisha tutakwenda pamoja katika Halmashauri yake ili Kwenda kujadili siyo tu matatizo haya ya mipango ya matumizi bora ya ardhi, lakini pia na kutatua kero nyingine zinazoendelea katika maeneo ya matumizi ya ardhi. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ni ukweli usiopingika kwamba migogoro ya ardhi imekuwa ikileta changamoto kubwa ikiwemo maafa na pia udumavu wa uchumi wa Taifa letu: Je, Serikali haioni sasa ni wakati umefika wa kuitambua kwamba hii ni ardhi ya kilimo, hii ni ardhi ya mifugo na matumizi mengine kwa Taifa letu? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kunti Majala, swali lake la nyongeza juu ya utaratibu wa kutambua ardhi za Tanzania. Naomba kwanza nimrudishe Mheshimiwa Mbunge katika Sheria zetu zinazoongoza usimamizi yaani Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ambazo zinatambua uwepo wa mgawanyo huu ambao yeye ameusema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, pia Wizara imeendelea kufanya semina mbalimbali na elimu mbalimbali kwa wananchi ili kuweza kuwatambulisha. Pia ziko hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na ufahamu juu ya mgawanyiko wa maeneo ya ardhi ikiwemo kufanya hatua kubwa za kuelewesha Umma wetu kwa jumla yake. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa ni ukweli pamekuwa na migogoro mingi sana kwenye Jimbo la Kibamba kuhusiana na kutokamilika kwa urasimishaji, sasa je, Serikali ina mkakati gani kumaliza kabisa migogoro hii inayohusiana na urasilimishaji kwenye Jimbo la Kimbamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mtemvu kwamba kama ambavyo nimeeleza katika swali la msingi kutoka kwa Mbunge Kunambi, hatua hizo ambazo zimechukuliwa kule Mlimba ndiyo ambazo pia zinaendelea kuchukuliwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kama nilivyoeleza; kuendelea kutoa elimu na kuendelea kuhakikisha Halmashauri zetu zinaendelea kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi ikiwemo mipango iliyowekwa na kushirikisha wananchi katika kuweka taratibu za ardhi katika maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini Wizara yake itaridhia upanuzi wa Mji wa Moshi kufikia kilometra za mraba 142 ukizingatia sasa hivi tuna kilometra za mraba 58 na maombi yako ofisini kwao; na hata damp tumenunua Moshi Vijijini na makaburi yanajaa, tutahitajika tena kununua pia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli maombi ya Mheshimiwa Priscus yalifika katika Ofisi zetu, lakini kama inavyofahamika mwenye mamlaka ya kuongeza maeneo ya kiutawala ni Mheshimiwa Rais. Hivyo, maombi yake tuliyapeleka katika ngazi

husika na majibu yatakapokuwa yametolewa tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa jicho lako kuniona. Naomba katika Halmashauri yangu ya Mkalama, Kata ya Matongo Kijiji cha Mnung'una yuko mwananchi mmoja ambaye amechukua ardhi ya wananchi karibu ekari 400; na hata baada ya matumizi bora ya ardhi ameendelea kukaidi: Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kama yuko tayari kufuatana nami ili kwenda kuondoa tatizo hili ambalo ni kubwa sana kwa wananchi wangu wa Matongo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Francis kwamba niko tayari kuongozana naye kwenda kuzungumza juu ya mgogoro huu ambao unakabili vijiji vyake katika eneo hilo la Kata ya Matongo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi unaohusu wananchi wa Kata ya Malula na Majengo walioko katika eneo linalozunguka uwanja wa KIA?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Pallangyo, Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutakapokuwa tumemaliza Bunge hili, nitaomba kuongozana pia na Mheshimiwa Pallangyo ili twende tukazungumze na wananchi wale tuweze kujua undani wa tatizo lenyewe na baada ya hapo tuweze kutafuta suluhu ya pamoja katika kuleta maendeleo katika maeneo yetu ya Arumeru. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kata za Jangwani na  
Mtawanya – Mtwara Mikindani**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu Kata ya Jangwani na Mtawanya Manispaa ya Mtwara Mikindani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Jangwani iliyopo katika Manispaa ya Mtwara Mikindani inapata huduma za mawasiliano kutoka kwa Kampuni za Tigo, Airtel na Vodacom. Vile vile maeneo ya Kata ya Mtawanya yanapata huduma hafifu za mawasiliano kutoka kwa watoa huduma wa Airtel, Vodacom na Tigo kuititia minara iliyojengwa katika Kata ya Likombe juu ya Mlima wa Lilungu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itavifanyia tathmini na uhakiki wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano maeneo yote yaliyopo katika Kata za Jangwani na Mtawanya na kuchukua hatua stahiki mara moja ili kuimarisha na kuboresha huduma endapo utatuzi hautahitaji ujenzi wa minara mipya.

Mheshimiwa Spika, endapo tathmini hiyo itabaini utatuzi wa changamoto zilizopo unahitaji ujenzi wa minara mipya, maeneo husika katika kata hizi yataainishwa na kuingizwa katika zabuni za kufikisha huduma ya mawasiliano zitakazotangazwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri niliongozana naye mwaka jana kwenda Mtwara kuangalia maeneo ambayo yana matatizo ya mawasiliano ikiwepo bandarini pale Mtwara, pale Mitengo kwenye Hospitali ya Rufaa.

Sasa nahitaji *commitment* ya Serikali, kwa kuwa tulishawahi kwenda na mwenyewe ukaangalia uhalisia. Ni lini sasa minara hii itapatikana kwenye maeneo husika? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tuliongozana na Mheshimiwa Mbunge kuangalia changamoto ya mawasiliano katika maeneo haya. Lakini tulitoa maelekezo kwa operator wote ambao wanatoa huduma ya mawasiliano katika maeneo haya ili kuweza kufanya *optimization* ili kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Mbunge bado anaonesha kuna changamoto pale, basi tutatuma wataalam wetu ili waweze kufanya tathimini ili tujirizishe kama kuna uhitaji wa ujenzi wa minara katika maeneo hayo. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kasim Iddi swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Naibu Waziri alifanya ziara jimboni Kata ya Jana na alipokuwa pale aliahidi ujenzi wa minara sita ambayo itajengwa Kata ya Mwakata, Kata ya Mwaluguru, Kata ya Chela, Kata ya Mega na Kata ya Runguya, Kijiji cha Nyangarata.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni lini utekelezaji huu utaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika kata hizo tuliahidi na tayari zimeingizwa katika mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo, na katika miradi ambayo inaongozwa na Mradi wa Tanzania Kidigitali ambao ni miradi 763 na katika minara hiyo 763 na maeneo ya Mheshimiwa Kassim Iddi yatakuwemo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aendelee kusubiri ilimradi tu mchakato wa utangazaji wa tender utakapokamilika, ujenzi wa minara utanza mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawaona wengi mmesimama lakini namna mnavyouila maswali mnasababisha ninyi wenyewe mnajipunguzia muda. Kwa hiyo, na mimi kuongea muwe mnaambiana hata ninyi wenyewe. Maana mnaanza na hadithi ndiyo unafuata swali. Sasa hiyo hadithi sijui unamuambia nani? Unamwambia Waziri au unatuambia Bunge ili tuje.

Mheshimiwa Masache Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuweza kuniona.

Kijiji cha Shoga kilichopo Kata ya Sangambi, Kijiji cha Sipa Kata ya Kambekatoto na maeneo karibu yote ya Kata ya Upendo yana changamoto kubwa sana ya mawasiliano ya simu za mkononi; je, ni lini sasa Serikali itapeleka minara ili kumaliza changamoto hii? Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunatatu changamoto ya mawasiliano ili Watanzania waendelee kutumia huduma ya mawasiliano katika biashara na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo ya Mheshimiwa Masache ni kwamba yameingizwa pia katika utekelezaji wa Tanzania Kidigitali katika miradi 763. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hali ya kukosekana mawasiliano ya simu katika Kata ya Jangwani, Manispaa ya Mtwara Mikindani inafanana kabisa na hali ya Kata ya Dutumi na Kwala kwa Kijiji cha Kimalamisale, Wilayani Kibaha, Mkoani Pwani.

Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri utafanya ziara katika maeneo hayo ili kujiona hali halisi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu, Mbunge Viti Maalum - Pwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alinijulisha siku mbili zilizopita kuhusu maeneo haya na mimi nikaenda kufuatilia katika utekelezaji wa miradi yetu kwa bahati nzuri maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge tayari yako kwenye utekelezaji katika ile miradi 763.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio, kama kutakuwa na uhitaji wa kwenda kufanya ziara basi sisi kama Serikali tuko tayari kufika katika maeneo yenye changamoto. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 35

### **Vifaa Tiba Hospitali ya Rufaa Tumbi na Hospitali za Wilaya Mkoa wa Pwani**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, ni lini Hospitali ya Rufaa Tumbi na Hospitali za Wilaya za Mkoa wa Pwani zitapokea vifaa tiba ikiwa ni sehemu ya fedha za kupambana na UVIKO-19?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu majibu.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi imeshapokea vifaa tiba 74 kati ya 77 vilivyoagizwa kwa fedha za kupambana na UVIKO-19, hii ni sawa na asilimia 94 ya vifaa vyote vilivyoagizwa ikiwemo mashine ya CT Scan. Kazi ya kusimika vifaa hivi inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa Hospitali za Wilaya, ujenzi wa majengo ya huduma za dharura yaani EMD na majengo ya huduma za wagonjwa waliopo kwenye uangalizi maalum yaani ICU unaendelea. Hivyo vifaa tiba kwa ajili ya hospitali hizi vitafikisha mara baada ya ujenzi kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalo swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya kupitia fedha hizi za UVIKO na naishukuru sana Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye jibu la msingi ameeleza vifaa hivi vimefika zaidi ya asilimia 94 katika Hospitali ya Tumbi; je, Mheshimiwa Waziri anatuahidi ndani ya mwezi Oktoba kwamba CT Scan itafanya kazi, yupo tayari kuwaelekeza wataalam wake kuhakikisha kweli mwezi Oktoba vifaa hivi vitafanya kazi kwa kuwa ni jambo la kihistoria na halijawahi kutokea kuwa na CT Scan ngazi ya hospitali za rufaa za mkoa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa kazi kubwa imefanywa ya ujenzi ya miundombinu ya afya ikiwemo vituo vyta afya Mkwakwani tuna vituo vyta afya 10 kutokana na tozo na hospitali za wilaya na zahanati.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kupunguza ujenzi wa miundombinu mipyta ili ijielekeze kuhakikisha miundombinu hii ambayo imejengwa kwa kasi inapata vifaa tiba kwa kuwa pia inakuja na mpango wa bima ya afya ili mpango huu ukianza kutekelezeka hospitali zote na vituo vyta afya viweze kuwa na vifaa tiba? Ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Subira Mgalo kwa maswali yake mazuri na hususan kusema kwamba suala la ununuzi wa vifaa tiba ni jambo la kihistoria ambalo limefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan haijapata kutokea. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa CT Scan kama nilivyosema itafungwa by October, 2022 lakini kabla ya kuanza kufanya kazi lazima pia tufanye *testing* (tufanye majoribio) na watu wa Tume ya Atomic Energy lazima pia watoe kibali cha kuanza kutumika. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Subira Mgali kwamba suala hili kwetu ni la kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu je, kwa nini sasa Serikali isijielekeze katika kuimarisha huduma za afya? Nakubaliana nawe Mheshimiwa Subira na mimi nilishatoa maelekezo kwa wenzangu Wizara ya Afya, lakini kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Tumejenga zahanati nyingi, tumejenga vituo vya afya vingi, tumejenga hospitali za wilaya nyingi. Sasa hivi tujikite kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa zenye ubora katika hospitali tulizojenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kipaumbele cha Wizara ya Afya au kwa sekta ya afya sasa hivi ni mambo mawili; ubora wa huduma, kuhakikisha huduma zinapatikana, dawa zinapatikana, tunao watumishi wa kutosha lakini pamoja na lugha ambazo wataalam wetu wa afya wanawahudumia wananchi. Kwa hiyo, hiki ndiyo kipaumbele cha sekta ya afya katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba hatutajenga zahanati na vituo vya afya kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi mnataka, lakini tutajikita katika maeneo ya kipaumbele ambayo tunadhani labda kuna umbali mrefu, kuna idadi kubwa ya wananchi, lakini pia mzigo wa magonjwa bado ni mkubwa katika eneo hilo husika. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Ziddu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Kuwalinda watumiaji dhidi ya madhara ya cyanide**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda watumiaji wa cyanide kama mbadala wa zebaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya majibu.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Ziddu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia njia mbalimbali kuwalinda watumiaji wa cyanide kuzuia athari za kiafya zisitokee wakati wa kutumia kemikali hizi ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuelimisha wachimbaji juu ya madhara yanayotokana na matumizi ya cyanide na namna ya kujikinga na madhara yake. Pia kuwaelimisha kufika vituo vya kutolea huduma za afya mapema kupata matibabu wanapopata madhara.

(b) Kufanya upimaji wa afya za wafanyakazi maeneo ya migodini.

(c) Kutumia njia nyingine katika uzalishaji wa dhahabu katika migodi iliyopo hapa nchini kama *direct smelting* na njia nyingine mbadala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ziddu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, cyanide na mercury ni kemikali ambazo zote zina athari kubwa kwa maisha ya watumiaji. Lakini pia cyanide ndiyo ina gesi ambayo inatoa sumu kali ambayo inaweza kusababisha vifo kwa watumiaji ukilinganisha na zebaki.

Je, Serikali imetoa elimu kiasi gani kwa watumiaji wale ili kuepukana na madhara ambayo yanaweza kupelekea vifo kwa wachimbaji wadogo? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa upatikanaji wa cyanide ni mchakato mkubwa na unahitaji mtaji mkubwa lakini pia unahitaji kuwa kibali ili uweze kununua cyanide jambo ambalo linapelekea wachimbaji wadogo wakashindwa kuipata hiyo kemikali ya cyanide.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kuipata kwa gharama nafuu ambapo sasa waweze kufanya shughuli zao za kila siku kama walivyokuwa wanaitumia mercury ambayo ilikuwa inaweza kukamata kwa 0.1 ambapo kwa kila siku wanakuwa wanazalisha na kuweza kupata chakula chao cha kila siku kulinganisha na cyanide? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Hassan Zidetu Kungu kwa maswali yake mawili mazuri hususan katika kuhakikisha tunawalinda wachimbaji wadogo wa madini na madhara ya matumizi ya kemikali hatarishi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wachimbaji wadogo huko nyuma na wengine hadi sasa wanatumia madini au mercury kwa Kiswahili zebaki ili waweze kuchenjua dhahabu ambayo wanatenganisha dhahabu, udogo na madini mengine. Lakini kimataifa nchi yetu inawajibika kusitisha matumizi ya zebaki kwa mujibu wa Mkataba wa Minamata. Kwa hiyo, ndomana saizi tunasisitiza matumizi ya cyanide.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba cyanide ni ghali ukilinganisha na zebaki, kwa hiyo wachimbaji wengi wadogo hawana uwezo wa kumudu. Tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Madini kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya matumizi ya cyanide na namna ya kujikinga na madhara na watu wa madini wako hapa.

Mheshimiwa Spika, pia tumeshajenga vituo vya mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo kujifunza jinsi gani ya kutumia madini haya ya cyanide kwa wachimbaji wadogo, kwa mfano pale Rwanagasa, Mkoani Geita tumeweka kituo hicho, Katente pia Mkoani Geita na Itumbi, Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nikiri bado tunayo kazi kubwa ya kufanya kwa sababu bado wachimbaji wetu wadogo hawana elimu, lakini pia vifaa kinga vya kujikinga na madhara yatokanayo na madini haya hatari ya cyanide.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kwa kutumia mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Madini pamoja na wenzetu wa OSHA kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanapata elimu pamoja na kujikinga na madhara ya madini haya.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa David Kihenzile.

Na. 37

#### **Hitaji la maji Kata ya Mwabuki – Misungwi**

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI K.n.y. MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata ya Mwabuki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti Mbunge wa Jimbo la Misungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mwabuki ina jumla ya vijiji sita vya Lubuga, Mhungwe, Mabuki, Mwagagala, Mwanangwa na Ndinga. Kwa sasa vijiji hivyo vinapata huduma ya maji kuitia visima vya pampu za mkono ambapo hali ya huduma ya maji ni asilimia 39.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji Kata ya Mwabuki katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imekamilisha usanifu wa mradi wa maji kutoka bomba kuu la KASHWASA kupeleka katika vijiji vyote vya Kata ya Mwabuki. Kwa sasa taratibu za manunuzi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2022 na kukamilika mwezi Desemba, 2023. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza huduma ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 39 hadi kufikia asilimia 100.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu mazuri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, moja, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Mtambula, Luhunga na Mninga kule Mufindi Kusini?

Mheshimiwa Spika, pili, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya maji ya Malangali, Nambalamaziwa na Igohole ambayo tayari Serikali imeshaanza kutenga fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali imejipanga hivi sasa katika kata zile tatu alizozitaja inafanya utafiti wa kupata vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, la pili, tayari taratibu za manunuzi zimekwisha kukamilika na mnano mwezi Desemba utekelezaji wa mradi utaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Miradi mingi ya maji ikiwemo ya Jimbo la Ukerewe...

**SPIKA:** Nenda moja kwa moja kwenye swalii.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ...inasuasua kukamilika kwa sababu ya mchakato mrefu wa kupata msamaha wa kodi. Nini mkakati wa Serikali kupunguza urasimu kwenye kupata misamaha ya kodi ili miradi hii ya maji iweze kukamilika haraka? Nashukuru. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli na hivi sasa Serikali inaendelea na jitihada, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba misamaha yote ya kodi inayohusu sekta ya maji iweze kupitiwa na kupatikana suluhu mapema ili kuweza kuwanufaisha wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, mkakati wa kutoa maji Ziwa Tanganyika ni mkakati wa muda mrefu. Nataka kujua mkakati wa muda mfupi wa kuwasaidia zile kata tano za Wilaya ya Nkasi, Kata ya Namanyele, Nkomoro, Majengo pamoja na Isunta kuepusha hiki kipindi ambacho wanakipitia kigumu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha shilingi bilioni 657 zimetengwa na iko miradi 381 mipyä. Ninayo imani kwamba katika hii miradi 381, miradi hii ya Nkasi ni mionganî mwao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aida uendelee kufuatilia katika kuhakikisha kuwa wananchi wa Nkasi na wenyewe wanapata faida hii ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Idadi ya wanafunzi kutoka Zanzibar waliopatiwa mikopo ya elimu ya juu mwaka 2020/2021**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza:-

Je, wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar wamepata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2020/2021?

**SPIKA:** Nadhani kisemeo chako hakijakaa vizuri, hebu zungumza tena.

Na. 38

**Idadi ya wanafunzi kutoka Zanzibar waliopatiwa mikopo ya elimu ya juu mwaka 2020/2021**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza:-

Je, wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar wamepata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2020/2021?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wote wa Kitanzania wenyе uhitaji bila kuangalia mwombaji anatoka upande upi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, takwimu za mwaka 2020/2021 zinaonesha kuwa wanafunzi Watanzania wapatao 1,492 wanaosoma katika taasisi sita za elimu ya juu zilizopo Zanzibar walipangiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.3. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 jumla ya wanafunzi wa Tanzania 1,929 wanaosoma katika taasisi za elimu ya juu Zanzibar walipangiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Omar swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kati ya wanafunzi 1,492 ni wanafunzi wangapi wenyе mahitaji maalum ambao walipatiwa mkopo huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali linataka takwimu hilo kama unazo takwimu umpe Mheshimiwa Mbunge kama huna kanuni zinakuruhusu kutoa baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda sasa kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Omar Ali Omar Mbunge wa Wetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa vigezo ambavyo vinatumia na Bodi ya Mikopo yetu ya Elimu ya Juu ni pamoja na ulemavu, kwa maana ya wenzetu wenyе mahitaji maalum pamoja ya uyatima. Kwa hiyo nitatoa takwimu tu za jumla za wenzetu hao kwenye makundi hayo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2021 wanufaika wote wa Bodi ya Mikopo walikuwa ni 149,389; kwa upande wa Zanzibar wale waliokuwa na mahitaji maalum walikuwa ni 100; na mwaka 2021/2022 yaani mwaka huu tunaoendelea nao jumla ya wanufaika wote ni 177,892 na wale wenyе mahitaji maalum kwa upande wa Zanzibar peke yake walikuwa ni 181, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa Serikali isione haja ya kushirikisha taasisi binafsi za fedha ili ziweze kutanua wigo wa kupata fedha zaidi kwa ajili ya kutoa mikopo na yenyewe ibaki ku-regulate tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hivi sasa tunaendelea na mazungumzo na taasisi mbalimbali za fedha, lakini katika bajeti yetu ya mwaka 2022/2023 tayari wenzetu wa NMB wameweza kuongeza bajeti yetu ya mikopo kwa ajili ya vijana wetu wa elimu ya juu pamoja na elimu ya kati zaidi ya shilingi bilioni 200. Kwa hiyo kama Serikali tunalifanya hilo na tutaendelea kulifanya.

**SPIKA:** Umesema zaidi ya milioni 200 au bilioni 200?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni shilingi bilioni 200.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu ya maswali yenu ambayo yanajibiwa na Serikali, niwashukuru sana kwa maswali mafupi kwa wale wachache walioweza kuuliza mafupi na wale waliouliza marefu tumeendelea na uvumilivu kidogo, lakini tuendelee sisi wenyewe kujifunza kwa sababu tunabana kidogo ule muda ukianza na hadithi ambayo kimsingi swali lako litajibiwa hata bila hiyo hadithi. Ukienda moja kwa moja hawa Mawaziri wako tayari kabisa kukujibu maswali yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni hapa ndani tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika; ni wageni wawili wa Bunge ambao ni ndugu Gerald Musabila Kusaya ambaye ni Kamishina wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini, karibu sana. (Makofii)

**14 SEPTEMBA, 2022**

Waheshimwa Wabunge, hapo mmesikia sio madawa ya kulevyta, ni dawa za kulevyta. Kwa hiyo tunaendelea na kujifunza Kiswahili maadamu tumeanza kupidisha sheria za Kiswahili humu ndani. (Makofi)

Tunaye pia Ndugu Seraphin Lusala ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo wa Serena Hotel, karibu sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wako humu ndani wamekuja kutembelea Bunge; wageni wa Waheshimiwa Wabunge wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Tunao wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 164 na walimu sita wa *Kitungwa Adventist Secondary School* kutoka Mkoani Morogoro, karibuni sana watoto wetu na walimu wenu kutoka Morogoro (Makofi)

Tunao pia waimbaji wa muziki wa injili kutoka sehemu mbalimbali za Jiji la Dodoma karibu sana waimbaji Dodoma. (Makofi)

Lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Benki ya *Diamond Trust*, Benki ya *Azania Bank Limited* pamoja na Kampuni ya *Kilimanjaro Leather Industries Limited* ziko kwenye viwanja vya Bunge kuanzia tarehe 12 Septemba, 2022 hadi tarehe 16 Septemba 2022 ili kuonesha huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi hizo. Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kwenda kuzitembelea.

Baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali (Na. 2) ya Mwaka 2022  
(The Written Laws Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill 2022**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu ameshatusomea shughuli inayofuata na sasa nimwite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, karibu sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu muswada, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Bunge lako tukufu, Serikali yote chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri wote na viongozi wote kwa ujumla katika nyanja mbalimbali kwa ushirikiano mkubwa milionipa kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja tangu niteuliwe kushika wadhifa wa kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamasisha na kutoa miongozo iliyowezesha kufanikisha vema zoezi zima la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. (Makofii)

Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkoo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kusimamia na kufanikisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa weledi na umahiri mkubwa. Hongereni sana na washiriki wa Bunge wote kwa ujumla. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kusimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, ndc na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaopatia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, ikiwemo kuandaa

muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bwana Onorius J. Njole, Mwandishi Mkoo wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo kwa kuishauri Serikali kuboresha muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2020, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2022, (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*) sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*) unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitekeza wakati wa kutumia masharti ya sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyoko katika sheria nyingine zilizopo. Baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika muswada huu ni kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuvianidika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipyta.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia muswada huu kama ulivyowasilishwa Bungeni kwa mara ya kwanza mnamo tarehe 23 Juni, 2022 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya kwanza Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (*The Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432*); sheria ya pili, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevy, Sura ya 95 (*The Drug Control and Enforcement Act, Cap. 95*); na sheria ya tatu ni Sheria ya

Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 (*The Public Leadership Code of Ethics Act, Cap. 398*).

Mheshimiwa Spika, muswada huu umegawanyika katika sehemu nne; sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya muswada inapendekeza kufanya marekebisco katika Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 ambapo vifungu vya 4, 5, 6, 7, 8A na 13 vinarekebishwa kwa lengo la kuongeza adhabu zilizoanishwa katika vifungu hivyo. Marekebisco haya yanakusudia kuimarisha jitihada za Serikali za kupambana dhidi ya ongezeko la vitendo vya uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu kutokana na madhara yake kwa nchi na kwa wananchi kwa ujumla. Hatua hii itasaidia kudhibiti uwezekano wa kuongezeka kwa makosa mengine ambayo huenda sambamba na makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Makosa hayo ni kama vile usafirishaji wa dawa za kulevyaa na biashara ya ngono.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisco haya, pamoja na mambo mengine, yanaongeza adhabu ya faini ili kuwianisha adhabu hizo na adhabu zinazotolewa kwenye makosa hayo katika nchi nyingine hususani nchi jirani na Tanzania.

Suala la mapambano dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu ni suala la kimataifa na hivyo mifumo ya sheria inapaswa kuzingatia viwango vya kimataifa. Vilevile, mapendekezo ya marekebisco yanakusudia kuweka masharti ya ulazima wa kifungo na faini kuwa adhabu ya nyongeza. Lengo la marekebisco haya ni kuiwezesha Tanzania kupambana ipasavyo na biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya muswada inakusudia kufanya marekebisco katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevyaa Sura ya 95 ambapo kifungu cha 2 kinafanyiwa marekebisco ili kujumuisha kemikali bashirifu au mchanganyiko wake katika orodha ya dawa zilizokatazwa kuingizwa nchini bila kibali chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisco haya ni kudhibiti madawa ambayo matumizi yake yanaweza kuchepushwa na hatimaye kutengeneza dawa za kulevyaa ambayo yamekatazwa na sheria hii. Hata hivyo, baada ya majadiliano kati ya Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba na Serikali, Serikali imeongeza misamiati mipyaa inayotoa tafsiri ya Kamishna Mkuu na Mkuu wa

Kituo cha Polisi kwa mujibu wa sheria hiyo. marekebisho hayo yamefanywa kupitia Jedwali la Marekebisho litakalowasilishwa kwenu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 32 kinafutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuwawezesha Maafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevy ya kuwa na nguvu za kisheria sawa na mamlaka waliyonayo Maafisa wa Polisi chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 au mamlaka waliyonayo Maafisa Forodha chini ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha, Sura ya 403.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa Afisa wa Mamlaka anaweza kuwasiliana na kushirikiana na mamlaka nyingine pale panapokuwa na uhitaji wa kufanya hivyo. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuboresha utendaji wa maafisa wa Mamlaka kwa kuwapa mamlaka toshelezi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 32A cha Sheria kinapendekezwa kurekebishiwa ili kumpatia mamlaka Mkurugenzi Mkuu au Afisa aliyeidhinishwa na mamlaka uwezo wa kutoa hati za upekuzi. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuiwizesha mamlaka kutekeleza majukumu yake ya kiupelelezi kwa ufanisi zaidi hususani, pale mamlaka inapotakiwa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia kuharibu au kutorosha ushahidi.

Mheshimiwa Spika, sheria hii pia inapendekezwa kufanyiwa marekebisho katika sehemu ya nne kwa kufuta kichwa cha sehemu hiyo na kukiandika upya. Madhumuni ya marekebishiwa haya ni kukifanya kichwa cha sehemu hiyo kiakisi ujumla wa masuala yote yanayotekeliza na mamlaka chini ya sehemu hiyo. Marekebishiwa pia yanapendekezwa kufanywa katika kifungu cha 48 kwa lengo la kuipa Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevy ya nguvu dhidi ya sheria nyingine yoyote pale ambapo kutakuwa na ukinzani na sheria nyingine katika masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevy.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya muswada inapendekeza kufanya marekebishiwa katika Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398. Kifungu cha 9 kinarekebishiwa ili kuweka ukomo wa muda ambao mtu anapaswa kuwasilisha tamko la mali na madeni wakati anapokoma kuwa kiongozi wa umma kuwa ni ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya siku ya kuhitimisha utumishi wake.

Mheshimiwa Spika, marekebishiwa yanayopendekezwa yanalenga kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 9 yanayohusu kiongozi kutoa tamko la mwisho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10 kinachohusu mali zisizopaswa kutamkwa kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa kimsingi sheria inapaswa kubainisha mali zinazopaswa kutolewa tamko ambazo tayari zimebainishwa katika kifungu cha 11.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekeblishwa kwa kuongeza katika orodha ya mali zinazopaswa kutamkwa mali zingine zinazopaswa kutolewa tamko. Marekebiso yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa mkanganyiko uliopo sasa kati ya masharti ya kifungu cha 10 na kifungu cha 11.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya majadiliano kati ya Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba na Serikali, Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na hatimaye imeridhia mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 11 kwa kuongeza aya mpya ya 11(2)(b) inayobainisha samani za ndani na vifaa binafsi vya matumizi kama mali zinazopaswa kutolewa tamko iondolewe. Marekebiso hayo yamefanywa kupitia Jedwali la Marekebiso litakalowasilishwa kwenu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha sheria hiyo kinapendekezwa kurekeblishwa kwa kuongeza majukumu ya Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Majukumu yanayopendekezwa kuongezwa ni pamoja na jukumu la utoaji elimu ya maadili kwa viongozi wa umma, kufanya tafiti mbalimbali zenyé lengo la kuimarisha maadili ya viongozi wa umma na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya maadili ya viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebiso ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebiso yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa

kunipatia fursa hii, kabla sijaanza kusoma na kwa vile nitasoma kwa ufupi, naomba taarifa nzima ya Kamati yetu iingie kwenye Hansard kama ilivyo kwenye kitabu chetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2022 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2022*].

Mheshimiwa Spika, muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Kikao cha Hamsini, Mkutano wa Saba wa Bunge tarehe 23 Juni, 2022 kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni 136(14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa miswada ya sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya muswada ambayo yaliwasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) siku ya Jumatatu tarehe 5 Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada hatua hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau walioalikwa katika mkutano wa kupokea maoni ya wadau (*public hearing*) uliofanyika Jumatano tarehe 7 Septemba, 2022. Katika mkutano huo, Kamati ilipokea maoni kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society*).

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru kwa dhati kabisa wadau waliowasilisha maoni yao ambayo yameongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya muswada huu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa muswada; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2022 umegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi wakati sehemu ya pili hadi ya nne zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

- (a) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (*The Anti-Trafficking in Person Act, Cap. 432*);
- (b) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Sura ya 95 (*The Drug Control and Enforcement Act, Cap 95*); na
- (c) Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 (*The Public Leadership Code of Ethics Act, Cap 398*).

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya tathmini ya kina kuhusu kiwango cha marekebisho yanayofanyika katika pamoja na kufanya upembuzi wa maudhui ya masharti yanayopendekezwa kama ambavyo inafafanuliwa katika aya zifuatazo:-

Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 yanapatikana katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 9 ya Muswada. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwepo kwa dosari chache za kiuandishi na kiuchapaji katika Ibara ya 4, 5, 6 na 7. Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha uandishi wa muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya muswada inafanya marekebisho katika kifungu cha 13 cha sheria kuu (*principal act*) na kuipa uwezo Mahakama wa kutoa adhabu kali (*severe penalty*) kwa mtuhumiwa anayerudia kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu. Ibara hii inapendekeza kuwa pamoja na adhabu nyingine zinazotolewa katika sheria kuu, iwapo mtu atarudia kutenda kosa, Mahakama imtoze faini isiyopungua shilingi milioni 100 na isiyozidi shilingi milioni 200 kwa kosa la pili au makosa yanayojirudia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia aina ya makosa yanayopatikana katika vifungu mbalimbali vya sheria hii, Kamati iliishauri Serikali kuweka adhabu ya juu kabisa kwa mtu anayerudia makosa kuwa kifungo cha maisha. Mapendekezo haya yalilenga kuweka masharti yenyе adhabu kali zaidi kwa wahusika wa makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Hata hivyo, baada ya majadiliano ya kina kuhusu mapendekezo hayo, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba adhabu inayopendekezwa katika muswada ibaki kama ilivyo kwa sababu Mahakama inapewa mamlaka ya kutoa adhabu ya juu zaidi kwa mkosaji wa mara ya pili kama nyongeza ya adhabu iliyotolewa kwenye vifungu vingine vya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Sura ya 95 yanapatikana katika Ibara ya 10 hadi Ibara ya 16 ya muswada. Baadhi ya masuala yaliyobainika katika uchambuzi ni pamoja na kukosekana kwa tafsiri na maana za maneno yaliyotumika katika masharti yanayopendekezwa na hivyo basi Serikali imeshauriwa kufanya marekebisho ya kiuandishi katika Ibara za 11, 14 na 16.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui na kutoa mapendekezo mahsusini katika masharti ya ibara nyingine za muswada zinazofanya marekebisho katika sheria hii. Kwa kiasi kikubwa, Serikali imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na vilevile Kamati imekubaliana na Serikali kwamba baadhi ya masharti yatabaki kama yanavyopendekezwa na muswada.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 13 mathalani, muswada unapendekeza kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 32 cha sheria kuu (*principal act*). Masharti mapya yanyopendekezwa, yanawapa Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevyta, uwezo na madaraka ya kukamata, kupekua na kuchunguza 6 makosa chini ya sheria hiyo. Aidha, masharti mapya yanapendekeza kwamba maafisa wa mamlaka hiyo katika kutekeleza majukumu hayo chini ya sheria hii, watambuliwe kisheria sawa na mamlaka ya Maafisa wa Polisi chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai au mamlaka ya Maafisa Forodha chini ya Sheria ya Forodha.

Mheshimiwa Spika, Ibara 13 pia inaweka masharti katika kifungu kipyta cha 32(4) na kifungu kipyta cha 32(5) ambavyo kwa pamoja, vinaipa mamlaka uwezo wa kuanzisha mahabusu zake, na masharti ya kumuweka mtu kizuizini kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika sheria nyingine kabla ya mtuhumiwa kufikishwa Mahakamani. Katika uchambuzi wake Kamati iliihoji Serikali iwapo kuna ulazima wa kuwa na mahabusu zinazojitegemea kwa mujibu wa sheria hii, na iwapo Serikali ina rasilimali za kutosha za kuendesha mahabusu hizo na hoja hii ilijengwa kwa kuzingatia kuwa, bado Serikali ina changamoto ya kuzihudumia mahabusu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mjadala mrefu na wa kina, Kamati kimsingi imekubaliana na Serikali kwamba masharti hayo yabaki kama ambavyo muswada unapendekeza. Moja kati ya mambo mahsusini ambayo yamezingatiwa na Kamati katika kukubaliana na Serikali katika jambo hili, ni njema iliyooneshwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba mnyororo wa udhibiti wa ushahidi (*the chain of custody*) tangu pale mtuhumiwa anapokamatwa hadi anapofikishwa Mahakamani, haukatiki. Aidha, muafaka baina ya Kamati na Serikali ulijikita katika kuiruhusu Serikali kuwa na namna ya upekee wa kushughulika na watuhumiwa wa makosa ya dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba biashara ya dawa za kulevyo ni haramu na madhara katika jamii ni makubwa. Hivyo mapendekezo ya Serikali iwapo yatasimamiwa kwa weledi na kwa uadilifu yanaweza kuwa njia mojawapo ya kuongeza ufanisi wa mapambano dhidi ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 yanapatikana katika Ibara ya 17 hadi Ibara ya 23 ya muswada. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini mambo kadhaa katika Ibara hizo na Serikali imeshauriwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali, isipokuwa katika maeneo machache. Moja kati ya eneo ambalo imeshauri Serikali kutafakari, ni maudhui yanayopatikana katika Ibara ya 20. Ibara hiyo inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11(2) cha sheria kwa kuongeza mali zinazopaswa kutamkwa katika tamko la mali na madeni ikiwemo vifaa vya nyumbani na vitu binafsi yaani *household goods and personal effects for private use*. Katika kifungu hiki cha 11(2)(b) kwa uchambuzi uliofanywa na Kamati, masharti haya yanaweza kuleta changamoto katika utekelezaji wake kwa sababu ya ugumu wa kubainisha na kuainisha vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba baada ya majadiliano ya kina, Serikali imeona mantiki ya hoja ya Kamati na hivyo basi imekubali kufuta masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa haya ni maoni na mapendekezo ya Kamati; Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba baadhi ya adhabu zinazopendekezwa na muswada pia zina lengo la kuzuia makosa chini ya sheria hii hasa kwa wakosaji wanaorudia makosa. Aidha, kwa kuzingatia kwamba tafiti zinaonesha kwamba waathirika wakubwa wa usafirishaji haramu wa binadamu ni wanawake na watoto, ni vyema Serikali ikafanya tafiti za kina na kupendekeza adhabu kali zaidi kwa lengo la kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu ili kuyalinda makundi haya.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyo, Sura ya 95; kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ipo katika vita vikali dhidi ya mtandao wa biashara ya dawa za kulevyo, mapendekezo mbalimbali yanayoletwa na muswada huu muhimu katika kuchochaea juhudzi za Serikali katika udhibiti wa biashara hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba katika mahabusu ambazo zinaanzishwa kwa mujibu wa mapendekezo ya muswada huu, Serikali ihakikishe inaweka masharti kwamba watuhumiwa watapata haki

zote za msingi, na kupata ulinzi wanaostahili kwa mujibu wa sheria za nchi na hakijinai.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria inayorekebishwa inatumika Tanzania Bara peke yake, Kamati inaendelea kusisitiza na kuishauri Serikali ishirikiane kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jithada za kupambana na biashara ya dawa za kulevyta. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kwamba Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta iendelee kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuongeza ufanisi wa mapambano dhidi ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398; kwa kuwa muswada huu unaweka masharti ambayo yanahu masuala ya maadili ya viongozi wa umma, ni vyema Sekretarieti ya Maadili wa Viongozi wa Umma ikatoa elimu kwa viongozi hao kuhusu masuala yanayowahu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba walichambua na kujadili na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ambavyo yameonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria wakati wa uchambuzi wa muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, hatuna budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya taarifa hii. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nigezo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jiji Dkt. Eliezer Feleshi, akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) Ndugu Onorius Njole kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa muswada. Aidha, nawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wa taasisi

ambazo zinatekeleza sheria mbalimbali zinazorekebishwa na muswada huu, ambao kwa namna moja au nyingine wamehusika katika kuandaa mapendekezo ya Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, ndc, kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Namshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, ndc, akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili, kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wa Bunge ambao wanaunda Sekretarieti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kuratibu vikao vya Kamati na kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa uchambuzi wa muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndugu Elihaika Mtui, Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Thomas Shawa, Ndugu Ludovick Ringia na Ndugu Thuwaiba Jumbe wakisaidiwa na Ndugu Theresia Jacob.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja; baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalmali Na. 2 wa mwaka 2022 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2022* pamoja marekebisho yake, kama uliyowasilishwa na mto hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (Makofij)

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU  
MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 2 WA  
MWAKA 2020 [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 2) ACT,  
2022] – KAMA YALIYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

- 1.0 **UTANGULIZI**
- 1.1 **Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya**

**Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2022].**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika **Kikao cha Hamsini, Mkutano wa Saba** wa Bunge, tarehe **17 Februari, 2022** kwa mujibu wa masharti ya **Kanuni ya 93 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni 136 (14)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ilitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ili Kamati iujadili na kuufanya uchambuzi.

## 1.2 **Namna Kamati Ilivyoteketeza Jukumu la Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha **Nyongeza ya Nane** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), siku ya Jumatatu tarehe 5 Septemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, baada hatua hiyo, kwa mujibu wa **Kanuni ya 97 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau walioalikwa katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau (*Public Hearing*) uliofanyika Jumatano tarehe 7 Septemba, 2022. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea maoni kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati kabisa, wadau waliowasilisha maoni yao, ambayo yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 **UCHAMBUZI WA MUSWADA**

#### 2.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022 umegawanyika katika Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya Kwanza inahusu Msharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi ya Nne zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika Sheria zifuatazo: -

- a) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (*The Anti-Trafficking in Person Act, Cap. 432*);
- b) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Sura ya 95 (*The Drug Control and Enforcement Act, Cap 95*); na
- c) Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 (*The Public Leadership Code of Ethics Act, Cap 398*).

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Kamati ilichambua Mapendeleko hayo kwa kufanya tathmini ya kina kuhusu kiwango cha marekebisho yanayofanyika katika pamoja na kufanya upembuzi wa maudhui ya masharti yanayopendekezwa kama ambavyo inafafanuliwa katika aya zinazofuata.

## 2.2 **Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 yanapatikana katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 9 ya Muswada. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwepo kwa dosari chache za kiuandishi na kiuchapaji katika Ibara ya 4, 5, 6 na 7. Kamati imeishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha uandishi wa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 9 ya Muswada, inafanya marekebisho katika Kifungu cha 13 cha Sheria Kuu (*Principal Act*) kwa kuipa uwezo Mahakama wa kutoa adhabu kali (*severe penalty*) kwa mtuhumiwa anayerudia kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu. Ibara hii inapendekeza kuwa, pamoja na adhabu nyingine zinazotolewa katika Sheria Kuu, iwapo mtu atarudia kutenda kosa, Mahakama imtoze faini isiyopungua shilingi milioni mia moja na isiyozidi shilingi milioni mia mbili kwa kosa la pili au makosa yanayojirudia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia aina ya makosa yanayopatikana katika vifungu mbalimbali vya Sheria hii, Kamati ilishauri Serikali kuweka adhabu ya juu kabisa kwa mtu anayerudia makosa kuwa kifungo cha maisha. Mapendeleko haya yalilenga kuweka masharti yenye adhabu kali zaidi kwa wahusika wa makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Hata hivyo, baada ya majadiliano ya kina kuhusu mapendeleko hayo, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba adhabu inayopendekezwa katika Muswada

ibaki kama ilivyo kwa sababu Mahakama inapewa mamlaka ya kutoa adhabu ya juu zaidi kwa mkosaji wa mara ya pili kama nyongeza ya adhabu iliyotolewa kwenye vifungu vingine vya Sheria hiyo.

## 2.3 **Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Sura ya 95**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Sura ya 95 yanapatikana katika Ibara ya 10 hadi Ibara ya 16 ya Muswada. Baadhi ya masuala yaliyobainika katika uchambuzi ni pamoja na kukosekana kwa tafsiri na maana za maneno yaliyotumika katika masharti yanayopendekezwa, na hivyo basi Serikali imeshauriwa kufanya marekebisho ya kiuandishi katika Ibara ya 11, 14 na 16.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui na kutoa mapendekezo mabsusi katika masharti ya Ibara nyingine za Muswada zinazofanya marekebisho katika Sheria hii. Kwa kiasi kikubwa, Serikali imezingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na vilevile Kamati imekubaliana na Serikali kwamba baadhi ya masharti yatabaki kama yanavyopendekezwa na Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 13 Mathalani, Muswada unapendekeza kukifuta na kukiandika upya Kifungu cha 32 cha Sheria Kuu (*Principal Act*). Masharti mapya yanyopendekezwa, yanawapa Mamlaka ya Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevy, uwezo na madaraka ya kukamata, kupekua na kuchunguza makosa chini ya Sheria hiyo. Aidha, masharti mapya yanapendekeza kwamba, maafisa wa Mamlaka hiyo katika kutekeleza majukumu hayo chini ya Sheria hii, watambuliwe kisheria sawa na mamlaka ya Maafisa wa Polisi chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai au mamlaka ya Maafisa forodha chini ya Sheria ya Forodha.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara 13 pia inaweka masharti katika Kifungu Kipywa cha 32 (4) na Kifungu Kipywa cha 32 (5) ambavyo kwa pamoja, vinaipa Mamlaka uwezo wa kuanzisha mahabusu zake, na masharti ya kumuweka mtu kizuizini kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika sheria nyingine kabla ya mtuhumiwa kufikishwa Mahakamani. Katika uchambuzi wake Kamati ilihoji Serikali iwapo kuna ulazima wa kuwa na mahabusu zinazojitegemea kwa mujibu wa sheria hii, na iwapo Serikali ina rasilimali za kutosha za kuendesha mahabusu hizo. Hoja hii ilijengwa kwa kuzingatia kuwa, bado Serikali ina changamoto ya kuzihudumia mahabusu zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya mjadala mrefu na wa kina, Kamati imekubaliana kimsingi na Serikali kwamba masharti hayo yabaki kama ambavyo Muswada

unapendekeza. Moja kati ya mambo mabsusi ambayo yamezingatiwa na Kamati katika kukubaliana na Serikali katika jambo hili, ni njema ilioonyeshwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba mnyororo wa udhibiti wa ushahidi (*the chain of custody*) tangu pale mtuhumiwa anapokamatwa hadi anapofikishwa Mahakamani, haukatiki. Aidha, muafaka baina ya Kamati na Serikali ulijikita katika kuiruhusu Serikali kuwa na namna ya upekee wa kushughulika na watuhumiwa wa makosa ya dawa za kulevyo.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kwamba biashara ya dawa za kulevyo ni haramu, na madhara katika jamii ni makubwa. Hivyo mapendekezo ya Serikali, iwapo yatasimamiwa kwa weledi na kwa uadilifu, yanaweza kuwa njia mojawapo ya kuongeza ufanisi wa mapambano dhidi ya biashara hiyo.

#### 2.4 **Marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398**

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 yanapatikana katika Ibara ya 17 hadi Ibara ya 23 ya Muswada. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo kadhaa katika Ibara hizo na Serikali imeshauriwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali, isipokuwa katika maeneo machache. Moja kati ya eneo ambalo imeshauri Serikali kutafakari, ni maudhui yanayopatikana katika **Ibara ya 20**. Ibara hiyo inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 11 (2) cha Sheria kwa kuongeza mali zinazopaswa kutamkwa katika tamko la mali na madeni ikiwemo vifaa vya nyumbani na vitu binafsi (*household goods and personal effects for private use*) katika Kifungu cha 11 (2) (b). Kwa uchambuzi uliofanywa na Kamati, masharti haya yanaweza kuleta changamoto katika utekelezaji wake kwa sababu ya ugumu wa kubainisha na kuainisha vitu hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, baada ya majadiliano ya kina, Serikali imeona mantiki ya hoja ya Kamati, na hivyo basi imekubali kufuta masharti hayo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

#### 3.1 Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba baadhi ya adhabu zinazopendekezwa na Muswada pia zina lengo la kuzuia makosa chini ya sheria hii hasa kwa wakosaji wanaorudia makosa. Aidha, kwa kuzingatia kwamba tafiti zinaonesha kwamba waathirika wakubwa wa usafirishaji haramu wa binadamu ni wanawake na watoto, ni vyema Serikali ikafanya tafiti za kina na kupendekeza adhabu kali zaidi kwa lengo la kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu ili kuyalinda makundi haya.

#### 3.2 Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Sura ya 95

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ipo katika vita vikali dhidi ya mtandao wa biashara ya dawa za kulevy, mapendekezo mbalimbali yanayoletwa na Muswada huu muhimu katika kuchochlea juhudzi za Serikali katika udhibiti wa biashara hiyo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, katika mahabusu ambazo zinaanzishwa katika mapendekezo ya Muswada huu, Serikali ihakikishe inaweka masharti kwamba watuhumiwa watapata haki zote za msingi, na kupata ulinzi wanaostahili kwa mujibu wa wa Sheria za nchi na HakiJinai.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa sheria inayorekebishwa inatumika Tanzania Bara peke yake, Kamati inaendelea kusisitiza na kuishauri Serikali ishirikiane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika jitihada za kupambana na biashara ya dawa za kulevy. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kwamba, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy iendelee kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuongeza ufanisi wa mapambano dhidi ya biashara hiyo.

#### 3.3 Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Muswada huu unaweka masharti ambayo yanahu masuala ya maadili ya viongozi wa umma, ni vyema Sekretarieti ya Maadili wa Viongozi wa Umma ikatoa elimu kwa viongozi hao kuhusu masuala yanayowahusu.

## SEHEMU YA NNE

- 4.0 **HITIMISHO**  
 4.1 **Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

1.	Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb.	Makamu
2.	Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.	Mjumbe
3.	Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.	Mjumbe
5.	Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.	Mjumbe
6.	Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb.	Mjumbe
7.	Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.	Mjumbe
8.	Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb.	Mjumbe
9.	Mhe. Omar Ali Omar, Mb.	Mjumbe
10.	Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.	Mjumbe
11.	Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.	Mjumbe
12.	Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.	Mjumbe
13.	Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.	Mjumbe
14.	Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb.	Mjumbe
15.	Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.	Mjumbe
16.	Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.	Mjumbe
17.	Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.	Mjumbe
18.	Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.	Mjumbe
19.	Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.	Mjumbe
20.	Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.	Mjumbe
21.	Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb.	Mjumbe
22.	Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.	Mjumbe
23.	Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb.	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria wakati wa Uchambuzi wa Muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, sina budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya Taarifa hii. Wajumbe hao ni: -

1. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
2. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
3. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb.
4. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) Ndg. Onorius Njohole kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada. Aidha, nawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wa taasisi ambazo zinatekeleza Sheria mbalimbali zinazorekebishwa na Muswada huu, ambao kwa namna moja au nyingine wamehusika katika kuandaa mapendekezo ya Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee niwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, ndc, kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Namshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, ndc, akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili, kwa kusimamia utendaji wa Kamati mbalimbali za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wa Bunge ambao wanaunda Sekretarieti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kuratibu vikao vya Kamati na kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa Uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii. Watumishi hao ni Ndg. Elihaika Mtui, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Thomas Shawa, Ndg. Ludovick Ringia na Ndg. Thuwaiba Jumbe wakisaidiwa na Ndg. Theresia Jacob.

#### 4.2 **Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2022]** pamoja Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mto Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria**

14 Septemba, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshamsikiliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia tumemsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria katika maelezo yaliyosomwa na Makamu Mwenyekiti na sasa ninayo orodha hapa mbele ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii.

Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mheshimiwa Luhaga Joel Mpina, ajandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na Serikali pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia Serikali ilete muswada huu muhimu sana kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wasilisho lake zuri na kwa kushirikiana vizuri sana na Kamati ya Katiba na Sheria katika kuuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya Watanzania na Waheshimiwa Wabunge naomba uniruhusu ninukuu taarifa ya Kamati katika Ibara ya 13 ya muswada. Taarifa ya Kamati inasema; "Katika Ibara ya 13 Muswada unapendekeza kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 32 cha sheria hiyo. Masharti mapya yanayopendekezwa yanawapa maafisa wa mamlaka madaraka ya kukamata, kupekua na kuchunguza makosa chini ya sheria hiyo."

Mheshimiwa Spika, naomba pia uniruhusu ninukuu sehemu ya pili ya taarifa hiyo katika Ibara hiyo hiyo ya 13 inayozungumzia Ibara ya 32 ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia Sura ya 95 ambayo inasema; "Kifungu kipyta cha 30 ambayo inaweka masharti katika kifungu kipyta cha 32(4) na kifungu kipyta cha 32(5) ambavyo kwa pamoja vinaipa mamlaka husika kwa maana ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia uwezo wa kuanzisha mahabusu zake na masharti ya kumuweka mtu kizuijini kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika sheria nyingine kabla ya mtuhumiwa kufikishwa mahakamani."

Mheshimiwa Spika, Bunge lako litakubaliana na mimi kwamba madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevyta ndani ya nchi yetu ni makubwa sana, vijana wengi wa Kitanzania ambao wameanguka kwenye matumizi ya dawa za kulevyta wamekuwa vijana ambao Taifa haliwezi kuwategemea tena na wamekuwa mzigo mkubwa sana kwa Taifa. Nenda Zanzibar, lakini nenda Dar es Salaam, Mikoa mikubwa na midogo kokote utakakokwenda utakuta vijana wengi wameathirika na matumizi ya dawa za kulevyta, lakini pia Serikali imebebehwa mzigo mkubwa sana wa kuhudumia na kuwarudisha kwenye hali ya kawaida, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, Bunge lako litakubaliana na mimi kwamba mtandao wa wauzaji wa dawa za kulevyta ni mkubwa sana ndani ya nchi hii, pia unahusisha nchi za nje, kwa hiyo ni mtandao ambao ni *complex* sana kwa nature yake, siyo mtandao rahisi kuuvunja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu, Bunge lako Tukufu litakubaliana na mimi kwamba kwa sehemu kubwa wanaojihusisha na kunufaika na biashara ya dawa za kulevyta ni wafanyabiashara wakubwa sana, matajiri wakubwa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa hiyo, siyo watu wadogo ambao tunaweza kukabiliana nao kirahisi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia litakubaliana na mimi kwamba njia ambazo zinatumika kusafirisha dawa za kulevyta ni ngumu na ni njia ambazo kimsingi zinahitaji utsalam maalum wa kuweza kukabiliana nazo. Nitatoa mfano. Unajua kwamba baadhi ya dawa za kulevyta zinasafirishwa kwenye tumbo la binadamu, wanaosafirisha wanameza kete zinakaa tumboni kwa saa nyingi, 48 au zaidi. Na hiyo ni moja kati ya njia ngumu ambazo zinatumika kusafirisha dawa za kulevyta. Pia zinasafirishwa kwa njia za meli, njia za boti, kupitia wavuvi kwenye bahari bubu. Kwa hiyo, hizo hoja nne zinadhihirisha kwamba kupambana na biashara ya dawa za kulevyta kunahitaji umahsusii, umakini, utsalam, ujuzi wa kipekee na zaidi kunahitaji nyenzo za kipekee sana.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa, kulitegemea Jeshi la Polisi peke yake kukabiliana na tatizo hili tunafeli. Sayansi, takwimu zimethibitisha kwamba tunafeli kwa kiwango kikubwa sana. Usambazaji wa dawa za kulevyta na uingizaji wake umeendelea kuwa mkubwa ndani ya nchi yetu licha ya Jeshi la Polisi kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ambayo yametolewa na Mamlaka hii ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta ni kwamba sasa wapate mamlaka kamili ya kuweza kukabiliana na jambo hili huku wakisaidiana na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, yapo mazingira ambayo tumeona, mtu ambaye ameshikwa na dawa za kulevy a napelekwa kwenye custody hizi mnasema rumande, anawekwa ndani, anatafutiwa ushahidi, kabla ushahidi haujakamilika ushahidi mtaani umepotea kwa sababu kuna *interaction* kubwa sana kati ya Jeshi letu la Polisi, watu wengine amba wanakaa ndani nao lakini pia wale amba wanashiriki kwenye huo mtandao. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Serikali ni kwamba tuwe na mahabusu maalum ambazo zitatumika kukabiliana na tatizo hili ili yule ambaye amekutwa na dawa za kulevy a chukuliwe awekwe kwenye mahabusu maalum ili pia tupate fursa ya kulinda ushahidi amba upo mtaani amba mara nydingi umekuwa unapotea kwa sababu watu hawa wakiachiwa au wakiwa na *interaction* na watu wengine amba wamekosa uadilifu au watu wengine amba wapo kwenye mahabusu amba hawana kesi kama hizo basi ushahidi huo unapotea na tunashindwa kulimaliza tatizo hili. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na pendelekezo la Serikali kuunga mkono hoja hii kwamba Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy ipewe sasa kibali cha kuwa na mahabusu yao waweze kupambana na jambo hili kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofij*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ajijandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuchangia katika Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka huu 2022.

Mheshimiwa Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati amba tulichakata Muswada huu kwa weledi mkubwa na niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kuitia wewe mwenyewe Spika wetu, muweze kuupitisha Muswada huu kwa sababu umezingatia maslahi mapana ya nchi yetu na watu wetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anazozifanya, hasa katika Majimbo yetu huku. Wabunge hawa ni mashahidi wa jinsi Serikali inavyoelekeza pesa kule kwa wananchi wetu amba wametuleta katika nyumba hii, anatutendea vizuri sana. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze pia wewe mwenyewe kwa jinsi unavyoliendesha Bunge letu hili Tukufu kwa weledi mkubwa sana, na umekuwa ukifanya kazi ambazo kwa hakika unatosha kwa kiwango cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yamekuja yakiwa katika sehemu tatu kama alivyosema, upande wa biashara haramu ya binadamu. Nianzie hapo tu kwa kifupi. Tumekuwa mashahidi hapo nyuma, watu wetu wanaovuka mipaka ya nchi yetu bila kutumia utaratibu, kuna mawakala ambao wanawavusha. Hao ndiyo waliokusudiwa humu hasa vijana wa kike ambao wanakwenda kufanya kazi ambazo hazina utu katika baadhi ya nchi, hasa nchi za Asia.

Mheshimiwa Spika, watu hawa wamekuwa wakitumia namna nzuri na urafiki wa mipaka yetu ambayo imepakana na nchi nyingi kupitia bahari zetu, maziwa na kuwavusha katika nchi nyingine hatimae wanaondoka kwa njia ambazo siyo sahihi. Ndiyo maana sheria hii inakuja kuweka adhabu kali sana, na hasa wale wanaorudia makosa yale.

Mheshimiwa Spika, wengine wamekuwa wakikamatwa lakini kumekuwa na tabia za kurudiarudia, wanakuwa ni wazoefu. Adhabu zimekuwa kali, kama alivyosema Makamu Mwenyekiti wetu wakati anasoma hapa, ni adhabu kubwa kwelikweli na lengo hasa ni kuhakikisha matukio haya hayatokei.

Mheshimiwa Spika, wewe ulikuwa shahidi, Bunge la Kumi na Moja kulikuwa na malalamiko makubwa sana ya watu wetu wanaopelekwa nchi za Kiarabu kufanya kazi wakidhani wanakwenda kufanya kazi kumbe wameuzwa. Sasa yule aliyenunua anajua amenunua mtu kumbe yule aliyepelekwa anajua amekwenda kufanya kazi. Ule utu wake unapotwezwa anafika mahali anajitupa hadi kwenye maghorofa.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia watu wetu na hasa mikoa hii ya katikati, Mkoo wa Singida ukiwa kati ya Mikoa iliyothirika, Mkoo wa Dodoma, kuna mabinti walijirusha huko nchi za Kiarabu, hatuwezi kuzitaja kwa sababu ni marafiki zetu. Lakini sheria hii inakwenda kupunguza kama siyo kutibu kabisa changamoto hii ambayo imekuwepo.

Mheshimiwa Spika, hapahapa tumeona watu wanaotoka nje wanapita hapa kwetu, wanaipa gharama kubwa Serikali yetu kwenye magereza yetu. Wale hawapiti peke yao, kuna watu ambao wanawavusha kutoka mpaka mmoja wa nchi kupitia nchi yetu na kwenda nchi nyingine. Adhabu hizi zitakwenda kuwfanya na kuwatia hofu wale ambao ni mawakala wa hii kazi waweze kuacha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Bunge lako likubaliane na kupidisha Muswada huu wa Marekebisho haya kwa maslahi mapana sana ya nchi yetu kwa sababu AG ambaye ni mtu msikivu sana kwa kipindi hiki tumefanya naye kazi kwa takribani mwaka mmoja, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana, nasi kama Kamati anatupa ushirikiano mzuri na pale ambapo anaona pana ugumu na Kamati inaona ugumu hasiti kukubali na kuondoa hiyo hoja ambayo alikuja nayo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Dawa za Kulevy, mamlaka imetaka tuingize kemikali bashirifu mionganoni mwa vitu hatari. Kemikali bashirifu ni dawa za kawaida ambazo baada ya kushepushwa kwa matumizi ambayo siyo ya kawaida ambayo yalitegemewa kupelekwa katika hospitali zetu, hasa hizi hospitali kubwa ambazo zinafanya operesheni kutumia dawa fulani za kupumbaza na kufanya ili mtu aweze kufanyiwa matibabu mengine, sasa watu huzitumia hizi kuzitengenezea pia dawa za kulevy.

Mheshimiwa Spika, ni kitu ambacho ni muhimu sana sisi kama Kamati tumeona madhara yake. Bahati nzuri mimi ni mionganoni mwa Wajumbe wa Kamati ile ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevy, kule pia tunakutana na hali hii. Kwa hiyo ilipokuja kwenye Kamati ya Katiba na Sheria kwa kweli tumeshiriki kwa kiasi cha kutosha na kulishawishi Bunge lako Tukufu likubaliane na hii hali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nafasi hii ya kukamata na hasa kutoa hati ya ku-search ambayo mamlaka inakwenda kupewa lilikuwa ni gumu na kabla haijatoka ile hati tayari watu walikuwa wanapata taarifa. Kwa sababu mtandao wa hawa watu, kama alivyosema mchangiaji aliyepita ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Kamati, ni kwamba wana nguvu sana za kiuchumi na kwa kuwa wana nguvu za kiuchumi wana ushawishi kwa Watumishi wa Umma wakiwemo Polisi na Taasisi nyingine ambao wanaweza kutoa hivi vibali vya upekuzi, inapofika mezani kwake anaweza aka-delay kwa dakika chache tu na taarifa hii ikawa imefika kwa wale ambao wanakusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakipewa mamlaka maana yake sasa suala hili linakwenda kufanya kwa usiri mkubwa kiasi kwamba tunaweza tukakamata mapapa wengine wengi zaidi kama ilivyotokea hapa nyuma.

Mheshimiwa Spika, niipongeze mamlaka hii, Mkuu wa hiki kitengo alipoteuliwa tu kwa kweli kazi yake ni kubwa sana na ni nzuri. Kuna mapapa hawakuwa wanakamatika lakini sasa wako ndani na kwa kiasi kikubwa sisi kama Wabunge tunashuhudia na wananchi wanashuhudia mitaani wale mateja walikuwa wamezidi kupita kiasi, wamepungua sana. Kwa hiyo,

ninaomba niendelee kuwashawishi Wabunge wenzangu kukubaliana na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hata uanzishaji wa mahabusu kwa kweli ni jambo ambalo tunaliona lina tija kubwa, kule mbele litaisaidia sana Serikali, litaisaidia nchi na wananchi kuondokana na hali ya nguvukazi kupotea kwa kiasi kikubwa kuititia dawa za kulevyta kwa sababu ya watu wachache ambao wanataka kujinufaisha kupata pesa ambazo ni haramu na hatimaye huingiza pesa hizi katika mzunguko kwa njia halali.

Mheshimiwa Spika, wanaingia katika biashara ambazo watu wanafanya na wanafanya biashara kwa ushindani ambao siyo ili yeye mwezetu ana nia ya kutakatisha pesa zile alizopata kwa dawa za kulevyta, sasa mnapofanya biashara unakuta mwenzio anauza rahisi, wewe umenunua ghali, sababu ni hizi.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. Naomba kuwasilisha. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa nami niweze kuchangia kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2022 ambayo inakwenda kufanya marekebisho ya Sheria Nne; Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu Sura ya 432, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Sura ya 95, Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia hasa kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta Sura ya 95. Jambo la kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuipongeza sana hii Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa kazi nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, tatizo la dawa za kulevyta hapa nchini lilikuwa kubwa sana. Kabla hizi hatua madhubuti hazijaanza kuchukuliwa, tatizo hili lilikuwa ni kubwa, vijana wetu walipata matatizo makubwa, uingizaji wa dawa za kulevyta kutoka nje ya nchi ulikuwa mkubwa, usambazaji wa dawa za kulevyta ndani ya nchi ulikuwa mkubwa, matumizi ya dawa za kulevyta ndani ya nchi ulikuwa mkubwa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mamlaka yetu hii imefanya kazi nzuri sana mpaka leo hii tumeingia kwenye rekodi ya dunia kati ya nchi ambazo zinapambana na dawa

za kulevyia kikamilifu. Hii ni hatua kubwa sana katika Taifa. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi, pamoja na marekebisho haya yanayoletwa lakini ukweli ni kwamba tumepiga hatua kubwa na tumedhibiti kwa kiwango kikubwa suala la dawa za kulevyia hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, nikienda ile Ibara ya 13 katika Kifungu Kipywa cha 32(4) na Kifungu Kipywa cha 32(5) ambapo yanawekwa masharti ya kuanzisha mahabusu, mamlaka iwe na mahabusu zake lakini pia iwe na uwezo wa kuweka watuhumiwa kizuizini. Jambo hili ni muhimu sana likafanyika kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, moja, ulazima huu wa mamlaka kuwa na mahabusu zake, mimi sina tatizo na marekebisho mengine, wakamate, wachunguze, wafanye nini, sina tatizo, lakini unapotaka kuanzisha mahabusu zako, kwa ajili ya nini? Yaani ule ulazima wa kuanzisha mahabusu zako ni kwa ajili ya nini? Kwa sababu kama kuna kitu *special* tunakitaka kwenye mahabusu zilizopo sasa hivi ambazo zipo chini ya Polisi, mahabusu ambazo zipo sasa hivi chini ya magereza, tuna uwezo wa kufanya marekebisho *zika-accommodate* yale mahitaji ya mamlaka badala ya kujenga mahabusu nytingine.

Mheshimiwa Spika, suala hili la kutunza mahabusu limekabidhiwa Jeshi la Polisi, wamekabidhiwa Jeshi la Magereza, leo tena tunataka kuwakabidhi na watu wa Mamlaka na wenyewe wawe na jukumu tena la kutunza mahabusu. Na hawa mahabusu na wenyewe wanao utaratibu wake wa namna ya kuwekwa, wa namna ya kutunzwa. Sasa kama kila mtu atakuwa na jukumu la kutunza mahabusu itakuaje?

Mheshimiwa Spika, pia tunaweza kuingia kwenye mkanganyiko mkubwa hata namna ya kushughulika na hizi kesi, kwa maana ya DPP, DCI na Mahakama zenyewe, na maana ya ushahidi huo tunaouzungumza, na hata namna ya upelelezi tunaokwenda kuufanya, kama hawa tunakwenda kuwapa jukumu tena la kukaa na mahabusu badala ya kwenda kupeleka kwenye taasisi ambazo zilishapewa jukumu hilo kulifanya.

Mheshimiwa Spika, pia kuna abuses nydingi msimamizi anapopewa jukumu la kukaa na mtuhumiwa, abuse hiyo inaweza kufanyika kwa sababu *checks and balances* zitakosekana. Wako watu hapa watakwenda kushinikizwa, hata kulazimishwa kukiri, kwa sababu ni huyu msimamizi ndiye anayesimamia na ushahidi huu tunao.

Mheshimiwa Spika, zipo mamlaka ambazo tulizipa jukumu la kutunza tu vielelezo au ushahidi mahakamani, mfano ni TAWA, tuliwapa jukumu hapa la kutunza vielelezo, kutunza ushahidi Mahakamani, wakakaa na mifugo ya

wafugaji, mifugo hao wote walikufa mikononi mwao kwa kutelekezwa bila kupewa dawa au malisho. Tatizo la msimamizi anapopewa atakapofanya abuse nani atamsimamia? Italeta changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 kama sikosei, wakati tunatunga Sheria ya Wanyamapor Na. 5 ya mwaka 2009, kikawekwa Kifungu kile kinachomruhusu Afisa wa Wanyamapor kum-shoot raia yeyote anayepatikana kwenye eneo lililohifadhiwa, akiwa hata anakimbia kukamatwa, wakaruhusiwa kukamata. Ikapita hapa tukaambiwa haitakuwa hivyo, tumekwenda kwenye utekelezaji wananchi wengi wameuawa kwa kupigwa risasi. Tumekwenda kwenye utekelezaji wanyama wengi wameuawa, mifugo wameuawa kwa kupigwa risasi, abuse iliyopitiliza.

Mheshimiwa Spika, leo hili Bunge lako linataka tena kupelekwa kwenye sheria hizi, linataka kupelekwa kwenye sheria za aina hiyo, iende ikafanyike tena abuse hii. Watu wakamatwe unasingiziwa, unatajwa Mpina wewe unahusika na dawa za kulevy, unakwenda kushinikizwa kule unapigwa unalazimishwa usaini mahali. Abuse hiyo nani anakwenda kuisimamia? Na kwa nini kama Taifa tutunge sheria za namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi, tunazo taasisi ngapi zinazohusika na usimamizi. Leo hii TAWA nao watakuja wanashughulika na majangili na majangili na yenyewe ni kesi za kupangwa zinahusisha watu wengi, na wenyewe waanzishe mahabusu zao. PCCB wanakamata watu wengi wa makosa mbalimbali na yenyewe yana mtandao mrefu sana kama rushwa, ufisadi na mambo mengine, na wenyewe waje watuombe hapa wanahitaji wajenge mahabusu.

Mheshimiwa Spika, pia tunao Uhamiaji, wana-deal na biashara mbaya sana ya binadamu, biashara haramu. Hawa nao watuombe tujenge mahabusu itakuaje? Wizara ya Uvuvi wanaohusika na mambo ya uvuvi haramu na wenyewe waje watuombe wakajenge mahabusu ya wavuvi haramu. Nchi hii patajengwa mahabusu kila sehemu. Itakuwa ni nchi gani? (Makof)

Mheshimiwa Spika, kama leo Bunge linaikubalia Mamlaka ya Dawa za Kulevy kujenga mahabusu, mamlaka nyingine zikija kutuomba tutafanya nini? Kwa hiyo nchi hii itajengwa mahabusu kila sehemu, kila mtu atakuwa mtunzaji wa mahabusu, hatuwezi kupiga hatua kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni suala la rasilimali fedha. Mpaka leo hii hatujakamilisha kujenga Magereza kila Wilaya. Kuna baadhi ya Wilaya wanabeba mahabusu kupeleka Wilaya nyingine. Mpaka leo hii kuna Wilaya ambazo mahabusu wanabebwa na kupelekwa Magereza za Wilaya jirani.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunataka kwenda kuli-commit Taifa likajenge mahabusu za Mamlaka za Dawa za Kulevyo ambazo sijui zitajengwa na zenyewe kila Wilaya? ambazo na zenyewe sijui zinakwenda kujengwa kila Mkoa hizo mahabusu? Kama leo hii tumeshindwa kukamilisha ujenzi wa Magereza kila Wilaya, fedha za ujenzi huu wa mahabusu wa Mamlaka ya Dawa za Kulevyo zinatoka wapi? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto kubwa ya kupata fedha za kujenga hizo mahabusu lakini kama fedha hiyo ndogo tunayo, kwa nini tusiende kufanya ukarabati wa zile mahabusu zilizopo Magereza na zile zilizopo Polisi na hata kama tunataka kufanya marekebisho madogo...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):**  
Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):**  
Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia nimpongeze mchangiaji kwa maelezo anayoendelea kuyatoa na mawazo yake hayo. Hata hivyo, nataka nimpe taarifa tu kwamba mahabusu wa madawa ya kulevyo ni tofauti kabisa na mahabusu wengine. Dawa za kulevyo zinasafirishwa kwa njia nydingi sana, binadamu ana maarifa makubwa; lakini iko sayansi ya usafirishaji wa madawa ya kulevyo ambayo unaweza ukute akayameza ndani ya tumbo na yakatakiwa kukaa kwenye tumbo lake mpaka baada ya muda fulani; katika mazingira hayo ndiyo maana chombo hiki kinakuja na mawazo kwamba tupate muda wa kukaa na huyu mtu katika maeneo mahsus, kusubiria endapo kitatokea nini katika kuthibitisha kama anayo kweli tumboni au lah!

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo kuna facility maalum, kuna dawa maalum anazotakiwa kutumia na kuna utaalam maalum. Hayo mambo hayawezi kufanyika kwenye Vituo vyetu vya Polisi. Ndiyo maana Serikali inakuja na mawazo hayo baada ya research na changamoto kubwa. Ninayeongea hapa nilikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, najua yanayotokea. Kwa hiyo, kama tutakaa hapa kama Serikali tunatetea wasafirishaji wa madawa ya kulevyo; nadhani basi hili Taifa linaingia kwenye matatizo. Kwa hiyo nataka kutoa taarifa tu kwamba, hizi ni *special crimes* lazima ziwe tackled kwa *special means*. Ahsante sana. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Mpina unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza hiyo taarifa yake siipokei na yeye kama Waziri alikuwa na nafasi ya kuja kuchangia, angezungumza hayo anayoyasema na Serikali wajipange vizuri kusikiliza Wabunge wanasesma nini.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, unaposema kwamba, Polisi hawawezi ku-handle haya mambo, leo hii tumepambana na madawa ya kulevyta kwa muda gani? Hatua hizi tulizofikia tumezifikiaje leo, kama leo Polisi wanazungumzwa hawawezi ku-handle mtuhumiwa wa dawa za kulevyta; na kama leo mamlaka ya Polisi inaonekana kwamba haina uwezo wa ku-handle watuhumiwa wa madawa ya kulevyta. Kama unataka *special facilities* hizo *special facilities* kwa sababu fedha yote ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hizo *facilities* haziwezi kujengwa polisi? hizo *facilities* haziwezi kujengwa magereza? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri sana kuelewa hata tunachokizungumza na hawa watuhumiwa wa dawa za kulevyta wanakamatwa leo kila sehemu ya nchi. Unakwenda kujenga leo wilaya nzima unakwenda kujenga mahabusu kila wilaya unazo hizo fedha? Kama zipo hizo fedha nimesema mpaka leo hii tunazo wilaya zetu hazina magereza, hizo fedha mbona hazikupatikana leo hii zimepatikana kutoka wapi?

**SPIKA:** Dakika moja malizia Mheshimiwa, kengele imeshagonga, dakika moja malizia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki cha Ibara hii ya 35 hasa kwenye kifungu cha 32(4) na 32(5) kifutwe. Kifungu hiki kifutwe na badala yake uwekwe utaratibu mzuri ambao utawezesha changamoto walizonazo hivi sasa mamlaka...

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina katika hiyo dakika yako moja ya kumalizia naona kuna Mheshimiwa Mbunge amesimama anataka kukupa taarifa.

Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Unajua Mheshimiwa Mpina ni shemeji yangu, sasa naomba nimpe taarifa, bahati mbaya hajashiriki kwenye Kamati yetu ya Katiba na Sheria ambayo yeye ni Mjumbe, tulishafanya mjadala wa kutosha kama Kamati kupitia hicho kifungu ambacho anataka kifutwe. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba angekuwepo kwenye Kamati pengine angeona uzito kwa nini hicho kifungu hatukukifuta. (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina unapokea taarifa hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani na taarifa yake, Bunge ni Bunge, Kamati ni Kamati; na mimi Mjumbe wa Kamati nimeshiriki vikao vyote na haya maelezo yalitolewa mbele yangu na niliyakataa na hapa kwenye Bunge lako nayakataa na naliomba Bunge lako likubaliane hiki kifungu kiondolewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina nilikuwa naangalia makaratasi hapa umeshaleta marekebisho ama hujaleta, umeleta marekebisho ama hujaleta, hii uliyosema kifungu kifutwe umeleta hapa mbele au hapana?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, yapo njiani yanakamilishwa.

**SPIKA:** Umesema?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nawasilisha sasa hivi.

**SPIKA:** Hapana, muda umeshapita.

Nataka Wabunge tuwe tunaelewana, maana mtu atatoka hapa kwamba nimependekeza kifutwe, lakini pendekoz lake halipo Kikanuni kwa sababu kwenye ngazi hii lazima marekebisho yawepo hapa ili Bunge lipate fursa ya kufanya maamuzi juu ya jambo analopendekeza; nadhani nilitoa maelezo kidogo kwa kirefu jana.

Mheshimiwa Hussein Amar atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama tena kwenye Bunge lako Tukufu, lakini pia niwapongeze na kuwashukuru wote ambaa walioniombea dua wakati nikiwa kwenye matibabu nchini India, Wabunge

wote Mwenyezi Mungu awabariki sana. Nimeweza kurejea salama na sasa hivi naendelea vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, niungane na wachangiaji waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kulitumikia Taifa letu. Pia nawe nikupongeze kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kulisimamia Bunge lako, kwa kweli tunakupongeza kazi, inakwenda vizuri sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, nimpongeze Mheshimiwa AG kwa wasilisho lake zuri la Marekebisho Na.2 lakini pia Kifungu 432 kwa ajili ya Marekebisho ya Biashara ya Binadamu, lakini pia Kifungu Na. 95 kwa ajili ya Madawa ya Kulevy.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi sana, kwamba nayaunga mkono marekebisho yote, lakini pia maoni ya Kamati yetu, nayaunga mkono sina pingamizi kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, biashara hii ya madawa ya kulevy au biashara hii ya dawa za kulevy tumeambia tuiseme madawa ya kulevy; dawa za kulevy, tumekuwa tukipambana kuweza kuzuia biashara hii ndani ya nchi yetu pamoja na nje ya nchi kuweza kuyaingiza madawa nchini mwetu. Shughuli hii ya kupambana kuwatafuta mapapa imekuwa haina mafanikio makubwa sana kwa sababu ushirikishwaji wa wananchi umekuwa ni mdogo, mapapa haya wanafahamika, na kazi zao zinafahamika, lakini kwa bahati mbaya taarifa mbalimbali zimekuwa zikitolewa kwa ajili ya hawa mapapa lakini hazifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ushauri wangu mdogo kwa upande wa dawa za kulevy, leo hii mitaa mingi katika nchi yetu kumekuwa na mitaa maarufu kabisa ambayo inahusiana na dawa hizi za kulevy, vijana wetu wameathirika lakini Kitengo hiki cha Kupambana na Kuzuia Madawa ya Kulevy na Jeshi la Polisi limekuwa halifanikiwa kwa sababu; limekuwa halina ushirikishiaji ama ushirikishaji mzuri kuititia wananchi. Nitatoa mfano, naishi Dar es Salaam, kuna mtaa mmoja unaitwa Mtaa wa Pemba, Mtaa ule wa Pemba umekuwa maarufu sana kwa Dawa za Kulevy. Je, Kitengo hiki na Jeshi la Polisi Mtaa huo hawaufahamu?

Mheshimiwa Spika, si huko tu kuna mitaa mbalimbali iliyopo Dar es Salaam na nchi yote kwa ujumla inajulikana kwa shughuli hii ya Madawa ya Kulevy, lakini kumekuwa na usiri mkubwa sana kati ya wauzaji walio wadogo na hao wahusika Jeshi la Polisi na hawa ambao wanazua madawa ya kulevy. Kwa sababu wananchi wamekuwa wakitoa taarifa na wanakamatwa wale watu, baada ya wiki mbili au tatu, unawaona wale waliotolewa taarifa wamerudi

mtaani. Hivyo, wananchi wanakata tamaa kuendelea kutoa ushirikiano, ndiyo maana hali hii inazidi kuwa mbaya. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sasa washirikishwe wananchi kwa kupewa motisha lakini wawe wanapewa taarifa, tulimkamata mtu fulani hatua zimechukuliwa na zimefikia hapa ili kuwatia moyo wananchi. Leo hii kuna ulevi mkubwa umezuka wa dawa za kulevyta, mirungi, mirungi leo hii imekuwa ni kama biashara halali tunataka tujue sasa biashara hii ya mirungi imehalalishwa? Kama haikuhalalishwa kwa nini wananchi hawa ama vijana hawa ambao wamejilingiza kwenye kundi hilo wanakula hadharani na wauzaji wanajulikana na hazichukuliwi hatua. Kwa hiyo, wananchi wamerudi nyuma kutoa ushirikiano kwa ajili ya kupambana na dawa hizi za kulevyta. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwemo pia dawa za kulevyta kama vile bangi, naomba pia njue kwamba dawa ya kulevyta bangi imehalalishwa? Dawa bangi imekuwa sasa hivi vijana wetu wadogo wadogo wamekuwa ni walevi wa hiyo kwa sababu imekuwa kama vile ni halali. Sasa tunataka tujue Serikali, Jeshi la Polisi na Kitengo hiki cha Kuzuia mmehalalisha utumiaji wa dawa hiyo ya bangi? Mtujulishe kama mmeruhusu tuweze kujua ni leseni ngapi zimetolewa kwa wauzaji hawa wa bangi. Kama ni haramu hatua gani ambayo Wizara inaichukua kuweza kuwanusuru vijana wetu, kwa sababu taarifa mbalimbali ambazo zinatolewa za wauzaji bangi na wanafahamika wanaonekana wapo mjini na wanatamba na wanaendelea na biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu naomba itolewe elimu kwa wananchi, lakini pia elimu hii itolewe kwenye shule za msingi, sekondari ili vijana wetu wakue wakijua athari kubwa ya madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba, AG tunamuunga mkono, ushauri wake, mapendekezo yake na ushauri, lakini pia nalishauri Bunge liunge mkono pia mapendekezo ya Kamati ili sasa Jeshi hili ama Kitengo hiki kiongezewe meno ili kuweza kupunguza ama kumaliza tatizo kubwa la madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Zainab Katimba, ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada huu Na.2 wa Mwaka 2022 ambao umeleta mabadiliko ya Sheria tatu; Sheria ya Usafirishaji wa Binadamu, Sheria ya najaribu kutafuta kwa Kiswahili jana umetusisitiza sana, imebidi niandike pembedi.

**MBUNGE FULANI:** Ongea tu lugha ya malkia.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, sawa. Sheria ya Anti-trafficking in Persons Act; Sheria ya Drugs Control and Enforcement; na Sheria ya mwisho ni Sheria ya *The Public Leadership Code of Ethics*. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ya leo imeletwa ya Kiingereza kwa hiyo utaturuhusu tu tusome yaliyoandikwa humu ndani kwa Kiingereza. Nianze na Sheria hii inayohusiana na dawa za kulevyia. Wote tunakubaliana humu ndani kwamba changamoto ya matumizi ya dawa za kulevyia ni kubwa sana na sijamsikia hata mmoja Mbunge mwenzangu aliyekataa kwamba wanaohusika na uuzaji wa dawa za kulevyia ni ma-tycoon, ni watu matajiri; ni watu ambaao wameshikana na mfumo. Tukubaliane tu Waheshimiwa Wabunge, kuna madhara makubwa wamewahi kuyapata baadhi ya Wabunge wenzetu ambaao walikuwa wanapinga au wanajaribu kuwatetea wananchi dhidi ya matumizi ya dawa za kulevyia.

Mheshimiwa Spika, amesema vizuri sana mjomba wangu pale Mheshimiwa Mpina, lakini nafikiri hakusoma vizuri mabadiliko ya sheria; kuhusiana na hizi Selo au Mahabusu; Sheria inasema hivi: Ibara ya 13(3) ya Muswada, inasema: “*The Officer of the Authority shall, in exercising the power under the subsection (1) and (2) and where the circumstance is so required, consult and cooperate with other relevant authority.*”

Mheshimiwa Spika, maana yake nini? Mamlaka wakati wanatekeleza majukumu yao ni lazima washirikiane na mamlaka zingine na naamini mamlaka hizo mojawapo ni Polisi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ikaenda mbele kifungu kidogo cha (4) ikasema: “*For the purpose of exercising the powers referred to under subsection (2), the Authority may establish cells or facilities for keeping a person arrested under the Act.*”

Mheshimiwa Spika, hapo ndiyo pameshikiwa hapo kwamba wataanzisha mahabusu, lakini Kifungu Kidogo cha 5 ndiyo kinafafanua zaidi kinasema: “*The safety of the person detained under subsection (4) and other matters relating to sending such person before the court shall be as provided for under the written laws.*”

Mheshimiwa Spika, tunaongelea watu kukamatwa ambaao mchakato wake umekuwa ni mgumu kweli kweli kuwakamatwa hao wahalifu. Hata hivyo, wakikamatwa wanapelekwa kwenye mahabusu zetu na wengi wanatorokea hapo. Sisi tunafikiria namna bora ya kuzuia wasitoroke kwa maana taarifa

zinavujishwa, vielelezo vinapotea, watu hawa wawekwe kwenye mahabusu maalum. Kama hiyo haitoshi watu wengi wanaokamatwa au wanaosafirisha haya madawa teknolojia sasa hivi inaonesha usafirishaji ni hatarishi zaidi kwa maisha yao kuliko hata dawa zenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo hawa watu ni lazima wawekwe kwenye uangalizi maalum ndiyo maana ya facility; wanawekwa kwenye uangalizi maalum ili kusudi kwanza tumesikia alifariki Msanii Mangwea, yale madawa yalikutwa tumboni na yakatolewa yako tumboni. Sasa imagine kwenye mahabusu za Polisi za kawaida na kama mtu huyo angeweza kupelekwa kwenye eneo maalum, pengine tungeweza kuokoa uhai wake. (Makof) **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane vita ya madawa ya kulevyta ni vita ngumu na mwisho wa siku Polisi ndiyo wanaoongoza kwa kuvujisha taarifa za wauzaji wa madawa ya kulevyta. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku Vituo vyetu vya Polisi havina mazingira mazuri ya kuweza kumsaidia mtu ambaye anasafirisha dawa za kulevyta ambaye wakati mwingine anafanya kwa shinikizo la ujinga, umaskini au la watu wanaomzunguka. Kwenye hilo, naunga mkono kwa asilimia mia moja. (Makof)

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome ngoja twende vizuri, nani amesimama kuhusu taarifa? Subiri kidogo Mheshimiwa Kigwangalla.

Mheshimiwa Salome nilikuwa nasikiliza hapa kwa makini kwanza umemtaja huyu aliyekuwa msanii ambaye ametangulia mbele za haki. Hii taarifa unayoisema mimi binafsi sikuwahi kuona mahali, ni taarifa rasmi, iko mahali kwamba alifariki kwa sababu ya madawa yalikuwa tumboni, ndiyo sababu ya kifo chake, maana sitaki tufike mahali ambapo tutaanza kuulizana haya mambo, maana sheria zetu zinatalinda sisi Wabunge na zinawalinda na watu wengine. Hii ni taarifa mahsus unatoa wewe ama ni taarifa mahsus ambayo Serikali imeitoa kwenye Kamati yenu wakati ikionesha umuhimu wa jambo hili? Nataka tu kujiridhisha na hilo maana sitataka kuletewa kesi hapa kwamba, marehemu amesemwa vibaya. Hizo taarifa mimi sizifahamu ndiyo nazisikia kwako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, marehemu hasemwi vibaya, *it was all over the news*, Vyombo vya Habari viliandika ambapo ni formal na visivyokuwa formal, kwa hiyo...

**SPIKA:** Sasa ngoja ngoja kwa hapa Bungeni ili lisemwe kwa namna hiyo lazima mimi nijue kama hiyo ndiyo sababu ya kifo ambayo imetajwa; maana kila mtu jamani sababu ya kifo si huwa inatajwa. Kama hiyo siyo sababu hayo maelezo kuhusu Mangwea, naomba uyaondoe ili tubaki na hiyo taarifa ambayo ndugu zake watakuwa nayo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Jambo la pili, kabla sijamruhusu yule wa kukupa taarifa ni hii ya polisi, kwamba ndio wanavujisha taarifa za wale wenyewe tuhuma za dawa za kulevyu wanavyokuwa kwenye remand zao. Hilo nalo nataka kujua Waziri wa Nchi uko hapa, ni polisi ndio anavujisha hizo taarifa? Yaani Bunge linataarifiwa kwamba polisi ndio wanaotoa hizo taarifa ama! Nataka tu kujiridhisha ili baadaye chombo chetu cha polisi tusije tukakiweka mazingira kwamba watu wanapelekwa huko halafu chenyewe ndicho kinasababisha utekelezaji wa sheria uwe mgumu.

Mheshimiwa Salome ili tuliweke vizuri ngoja Mheshimiwa Waziri wa Nchi amesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Mheshimiwa Spika, kama nimemuelewa vizuri Mheshimiwa Salome alichokizungumza amezungumzia juu ya complexity ya namna ya upatikanaji wa ushahidi unapotuhumiwa mtu ambaye anasafirisha au anatuhumiwa kwa namna nyingine yoyote au anatuhumiwa kwamba amebeba dawa za kulevyu ndani ya mwili wake; kwamba mazingira yale ni very special. ndicho nilichomuelewa akiwa analizungumzia. Kwamba pengine katika mazingira yale si rahisi kwa mazingira ya vituo vyetu vya polisi kuweza kuwa na mazingira ya namna hiyo. Kwa sababu, hizo special facility zinaweza zikawa hazipo na yule mtu anaweza akawa hajapata fursa nzuri na kwa hivyo tusipate ushahidi unaokusudiwa. Kwamba polisi wanavujisha hili ni jambo lingine sasa ambalo nadhani...

**SPIKA:** Basi Mheshimiwa Waziri utakuwa haukumsikia vizuri maana unayotoa wewe ni yale uliyotoa taarifa kuhusu Mheshimiwa Mpina. Yeye Mheshimiwa Salome anaunga mkono kabisa kutengenezwa hayo mazingira mahususi kwa ajili ya hawa ambao ni watuhumiwa wa dawa za kulevyu, anaunga mkono hoja hiyo. Hoja yangu mimi ni pale ambapo kwenye lugha ya mazungumzo anasema; kwa kuwa hawa watuhumiwa wanapelekwa polisi kwenye remand zile za kawaida, polisi ni sehemu ya watu ambao wanatuhumiwa kuvujisha taarifa zinazowahusu wale watuhumiwa. Kwa hiyo,

tusikilize vizuri ili Bunge letu lisije likakaa na taarifa ambazo kidogo zitatufunga sisi wenyewe hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo kuna watumishi ambao si waadilifu, baadhi, kwa sababu haiwezi ikawa wote mwisho wa siku kuna wengine wanafanya vizuri wengine wanafanya vibaya. Lakini kwenye mazingira yanayohusiana na dawa za kulevyta wapo askari polisi ambao wanahusika moja kwa moja kwa ajili ya kuvujisha taarifa, ili kuweza kumlinda aidha yule anayesafirisha madawa ya kulevyta au yule aliyemtumia nafasi yake kuuza madawa ya kulevyta **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ngoja kwanza, Makamu Mwenyekiti nimekuona malizia.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Yaani sio malizia mchango malizia ufanuzi wako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sio wote lakini wapo ambao wanahusika kufanya hivyo wanaweza wakawa sio wote. (Makofii)

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya unajua haya mambo yamejadiliwa huko kwenye Kamati. Mheshimiwa Kigwangala nilikuona, lakini nimpe kwanza Mwenyekiti wa Kamati kwa sababu nataka kujiridhisha haya mambo ya polisi kuvujisha ni mambo yanayosikika au ndio uhaliisa? Si kwamba polisi nzima yaani wapo polisi wanaovujisha taarifa? Hiyo ndio hoja. Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti.

## **TAARIFA**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Salome. Kilichozungumzwa ni kwamba, si kutokuliamini Jeshi la Polisi. Hayo anayosema yeye ni hayo lakini kilichozungumzwa na kujadiliwa ni

kwamba wale wanaoingia kwenye mahabusu za polisi ambao ni watuhumiwa ndio wanaovujisha hizo habari na kukosa kupatikana ushahidi wa sehemu nyingine ambayo inatakiwa zikakamatwe hizo dawa. Hivyo ndivyo tulivyokubaliana.

**SPIKA:** Haya, alikuwa amesimama Mheshimiwa mwingine, Mheshimiwa Kigwangalla.

### TAARIFA

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilipenda kumpa taarifa Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, kwamba hata kama zitakuwepo mahabusu maalum ambazo zitakuwa zinasimamiwa na hii Mamlaka ya Kudbiti Dawa za Kulevy, huo wasiwasi alionao, kwamba kuna polisi ambao wana changamoto ya kuvujisha taarifa za watu wanaofanya biashara ya dawa za kulevy; kwa kuwa hata huku kwenye chombo hiki cha mamlaka wanaofanya kazi ni binadamu ni Watanzania wenzetu na hawako perfect vile vile yanaweza yakajitokeza na huku pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kuzingatia muktadha kwamba wanaofanya kazi kwenye hivi vyombo ni binadamu, ni Watanzania wenzetu asitumie lugha ya kujenga hoja ambayo inalituhumu moja kwa moja Jeshi la Polisi na Askari wetu, chombo ambacho tunakiamini na tunakitegemea katika kusimamia usalama wa raia kujenga hoja ya uhalali wa kwamba basi tuwe na chombo hiki pengine hiki kitakuwa waterproof. Kwamba kitakuwa kina watu ambao ni wazuri zaidi kuliko wale polisi kwa sababu wote ni binadamu. (Makofii)

**SPIKA:** Sawa; sasa Mheshimiwa Salome kabla sijakupa fursa ya kuipokea ama kuikataa taarifa hiyo kwanza, nimeendelea kutoa maelezo pamoa na wewe kutoa ufanuzi wa kusema si wote ni baadhi. Ukipokea baadhi kwa sababu tunazungumzia chombo ambacho kinasimamia usalama wa raia, hata hao baadhi tutataka kujua kama ushahidi upo ama haupo. Kama ushahidi haupo hili la baadhi liondoe wewe endelea kujenga hoja yako. Kwamba, kwa nini kuna umuhimu wa kuwa na hizi mahabusu maalum kwa ajili ya watu hawa ndio hoja yako ya msingi. Hawa wanaovujisha sijui akina nani, baadhi; kama hatuna ushahidi hasa wa kwamba kuna polisi ambao wamewahi na wenywewe sasa baada ya kuvujisha wakutuhumiwa, hilo tuliondoe kwenye taarifa zetu rasmi halafu wewe jenga hoja yako ambayo ulikuwa umeanza nayo tangu mwanzo. (Makofii)

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniongoza, na nimuombe Mheshimiwa Kigwangalla asinilishe maneno mdomoni. Kama alikuwa anataka kuchangia achangie ya kwake lakini asinilishe mimi maneno

ya mambo ya uadilifu na kutegemea Jeshi la Polisi. Kwa sababu, hata mimi najua umuhimu wake na siwezi kusema hivyo ulivyosema wewe kwa hiyo sikubali mchango wako. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nimalizane na hoja ya dawa za kulevyta hakuna kipyta ambacho tunakifanya.

**SPIKA:** Ngoja ngoja umefanya vyema taarifa yake umeikataa sasa rekebisha yale maneno yako yafute yale kama ulivyofuta ya Mangwea halafu muda wako mimi naulinda usiwe na wasiwasi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nimeyafuta naomba niendelee samahani sana.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hakuna jambo jipya ambalo tunalifanya kuhusiana na kuanzisha cell/remand au special facility kwa watu ambao wanaathirika na madawa ya kulevyta. Katika East Africa Rwanda na Kenya wanafanya. Duniani Italy, Marekani, India na Brazil; na nchi kibao wanafanya. Kwa nini wanafanya hivyo, ni kwa sababu ya unyeti wa jambo hili na wahusika wanaohusika na mambo hayo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo niende kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Binadamu. Nimeona tunajaribu kuongeza kiwango cha adhabu kwa maana ya kifungo na faini kwa watu wanaohusika na usafirishaji wa binadamu. Mimi sijui ni kwa nini Serikali hawajalionta hili kwa uzito kama walivyoliona la dawa za kulevyta, sijui ni kwa nini. Biashara ya usafirishaji wa binadamu ilishapigwa marufuku miaka mingi iliyopita, hatuna sababu yoyote ya kuendelea kubembeleza watu wanaosafirisha binadamu. Kusafirisha binadamu ni unyama.

Mheshimiwa Spika, juzi nimeona kwenye taarifa ya habari, kuna mtu amesafiri sijui kutoka Mbeya kakaa kwenye lile buti la basi. Hivi fikiria wewe ukae kwenye buti la basi kuanzia asubuhi mpaka jioni eti unasafirishwa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako mimi nafikiri hivi viwango vya *fine vilivyowekwa*; kwanza hakuna sababu ya kutoza eti faini ya Shilingi milioni 50. kwa sababu kama mimi nataka kusafirisha binadamu nawapeleka nje kwenda kufanya kazi ambayo mtu mmoja analipwa kuanzia dollar 5,000 mpaka dollar 15,000 hivi kweli faini ya Shilingi milioni 50 ni kitu gani? Faida wanayoipata hawa watu wanaofanya *human trafficking* ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku ninachoshauri, ningependekeza kuwe kuna kifungo cha maisha kwa watu watakaokutwa wanafanya shughuli ya kusafirisha binadamu. Na ukiacha hivyo, kusiwe na faini, kwa sababu faini tunatengeneza majadiliano. kusiwe na faini yoyote kuhusiana na kosa hilo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Sheria ya mwisho ya Maadili ya Utumishi wa Umma. Sheria hii ya Kanuni ya Maadili kwanza, sijui labda inawezekana wamepitija; wanarekebisha kifungu ambacho hakipo. Wanasema sehemu ya nne ya Muswada sheria inarekebisha kifungu cha 9 (1)(c) kwenye sheria inayorekebisha hicho kifungu hakipo nataka kuamini kwamba walipitiwa kwa sababu kuna (a) na (b). Sasa, hicho kifungu cha (c) ambacho kinabadilishwa wanaongeza kwa kusema eti mtu anapoacha kazi anatakiwa kujaza ile fomu ya maadili angalau miezi mitatu kabla hajaacha kazi. Sasa kipindi cha mwendazake tulikuwa tunaona mtu ukienda kwenye mkutano wa hadhara unatumbuliwa sasa hiyo miezi mitatu nyuma utaipata wapi ya kujaza fomu? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tunaona kuna watu wanaachishwa sijui watumishi hewa angepata wapi muda wa kujaza fomu nadhani hapo mmesahau kidogo, hiyo sifa ya kwamba ujaze miezi mitatu kabla ama iondolewe au iboreshwe kwa mazingira kama hayo ya mtu ambaye hatopata hiyo nafasi ya kupata miezi mitatu kabla ya kujaza fomu ya maadili.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Sehemu ya nne, Ibara ya 20 ya Muswada inarekebisha kifungu cha 11(2) ambayo inaongeza wigo wa mali zinazotakiwa kuorodheshwa na mtu ambaye anatakiwa kujaza fomu ya maadili. Wote tunajua huwa tunajaza mashamba gari nini, sasa zamu hii kwa kweli Mheshimiwa Attorney General umeleta kichekesho. Umeleta kichekesho kwa sababu meongeza katika mali zinazotakiwa kuongezwa eti tuzijaze ni hizi zinaitwa *household goods*. Sasa nimeenda kwenye tafsiri ya sheria kuangalia maana ya...

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Najma Giga.

## **TAARIFA**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Salome, inawezekana hajaisikiliza vizuri taarifa yetu ya Kamati. Ni

kwamba Serikali wameshakubali na wamekiondoa hicho kifungu kwa hiyo wameona hakina maana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Najma taarifa yako naipokea lakini kwa manufaa ya wengi ambao hatukuwepo kwenye Kamati walikuwa wameweka kitu kinaitwa *household goods*. *Household goods* zinahusisha nilienda kwenye google tuliambiwa tu-google inahusisha wanyama wale nyau, mbwa wa pale nyumbani kwako, mabakuli, vitanda. Sasa tuna kitu kinaitwa *admin means rule...* (Makofi/Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa hiki kifungu kimefutwa nafikiri Mheshimiwa Salome anajaribu kuweka msisitizo ili kisije kikarejea tena humu Bungeni. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (Makofi/Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, lengo langu ni kulinda hadhi ya mwenendo wa majadiliano ya Bunge kitu kikishaondolewa hakipaswi kuingia kwenye kumbukumbu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Attorney General mimi nakumbusha tu ili tuongeze umakini kwa kweli taaluma ya sheria, tunatumia muda mwangi sana kusoma na kwa kweli sikutegemea kama tutakutana na mambo kama ya nyau. Kwa hiyo, niombe tu tuongeze umakini kwenye eneo hilo kwa sababu nakuamini sina wasiwasi na wewe na ndiyo maana ulikubali *that is household goods* haiwezekani. Mimi nakubaliana na mabadiliko ya sheria lakini nakushukuru sana. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na Muswada huu wa Sheria kwa marekebisho haya kwenye eneo la usafirishaji wa binadamu lakini pia dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, jopo letu la wanasheria katika Kamati ya Katiba na Sheria tumekaa tukajadiliana kwa makini sana; na kimsingi tumekubaliana na mapendekezo ya Serikali juu ya suala linalohusiana na marekebisho ya sheria hii, Ibara ya 9(13) na Sheria ya Dawa za Kulevyta, kwamba yanafanana kabisa na Sheria ya Usafirishaji wa Binadamu. Haya yanaitwa ni makosa ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ambao wanahusika moja kwa moja kwenye suala la usafirishaji wa binadamu na dawa za kulevyta ni matajiri wakubwa sana ambao kimsingi wao wanapata fedha lakini athari kubwa sana inakuja katika jamii ambao ni masikini. Watu wa mwisho ndio ambao wanakuja kupata athari kubwa sana, ikiwepo makundi ya vijana, wanawake pamoja na watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuhusiana na suala la usafirishaji wa binadamu Kamati imekaa na imekubaliana na kifungo hicho. Na mimi nasema, ni vizuri basi sheria hii ikitiliwa mkazo ili wasafirishaji hawa wanaofanya biashara hii ya usafirishaji wa binadamu waweze kupata kifungo cha Maisha. Sambamba na kifungo cha maisha mahakama ipate nafasi ya kuongeza kifungu cha kutoa faini, ambayo ni Shilingi milioni 100 au Shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nilikuwa nataka tu nitoe ufanuzi ili kutoa uelewa kwa nini tunazungumzia suala la usafirishaji wa binadamu. Ni kwamba, suala hili halifai na tunalipiga vita sana, na ndiyo maana imeletwa sheria hapa ili kuweza kurekebisha katika vifungu hivyo na kutia mkazo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi binadamu anaposafirishwa kwenda kwenye maeneo mbalimbali maana yake wanakwenda kutumika visivyo wakati mwingi tumeona kwamba kuna malori yanapita ndani ya nchi yetu yakisafirishwa kwenda kwenye maeneo mengine tunakuta kuna binadamu pengine zaidi hata ya 200 wamepoteza maisha, wamefia humo kwenye malori.

Mheshimiwa Spika, pia wapo wafanyabiashara wa usafirishaji wa binadamu ambao kimsingi wanachukua binadamu wanawadanganya kwamba labda pengine wanakwenda kupata ajira sehemu, hususani mabinti na wanawake. Wanawaambia kwamba tunakwenda kuwapeleka huko na mtapata kazi nzuri mtapata ujira mkubwa. Mwisho wa siku wanakwenda kuwatumia kwa masuala mbalimbali ikiwepo masuala ya madanguro; wanatumika vibaya huko, lakini pia wamekuwa wakipoteza maisha. Hii pia inaambatana na biashara ya viungo vya binadamu. Kwa hiyo kumekuwa na athari kubwa sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napendekeza pia kwamba sheria kali hii itiwe mkazo kuitia Bunge lako Tukufu ili suala hili liweze kukomeshwa mara moja. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na dawa za kulevyta; kifungu Na. 32(5) kimeletwa katika Bunge hili kupitia Kamati ya Bunge, lakini pia Serikali ili kiweze kufanyiwa marekebisho. Sisi kama Kamati tumeshauri kwamba ijengwe mahabusu maalum kabisa ambayo itashughulikia suala la hawa mahabusu wanaohusiana na dawa za kulevyta. Nimeona hapa kuna hoja mbalimbali, taarifa na nini, lakini kimsingi niseme tu kwamba, mahabusu hii incnjengwa kwa makusudi kabisa ili iweze kutoa wigo mpana wa taasisi maalum kushughulikia suala hili kwa ukaribu na kwa ukamilifu zaidi bila kuathiri tendo lenyewe la kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, hawa wenzetu ambao wanashughulika na dawa za kulevyta wamekuwa wakihitaji zaidi kupanua masoko yao. Endapo wanakutana na makundi ya watu wawili watatu basi ni fursa kwao kwa ajili ya kutoa elimu dhidi ya dawa za kulevyta na kuhamasisha suala hili liweze kuendelea na kukua zaidi. Kwa misingi hiyo, endapo muuzaji wa dawa za kulevyta anakamatwa anahusishwa kwenye mahabusu ya raia wengine wakiwepo pale polisi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mahabusu haichagui, maana yake mwizi wa kuku atakuwa humo, mwengine amebishana tu jirani yake atakuwa humo, wengine wana makosa madogo ya udokozi watakuwemo humo. Sasa anapoingia gwiji huyu wa dawa za kulevyta kwenye mahabusu hiyo ya polisi ni wazi kwamba atatoka mle ameshafanya kazi yake ya kuwaelimisha na kuwashamasisha waliomo mle waondokane na wizi wa kuku, udokozi na uvutaji wa bangi na mambo mengine. Badala yake sasa waingie kwenye biashara ya dawa za kulevyta kwa kuwashamasisha kwamba biashara hii inalipa na kwamba wanaweza Kwenda kuwasaidia kupata uwezeshaji ili nao waweze kusafirisha madawa hayo ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, na mtu akishawishiwa kwenye maeneo hayo anakubali, anaona kwamba kama mnaiba kuku na nimefikia hapa je, nikisafirisha dawa za kulevyta maana yake atapata pesa nyngi. Kwa hiyo kuwakutanisha na wale watu wa aina hiyo kunatoa fursa kwa wauzaji wa dawa za kulevyta kushawishi jamii nyngine ambayo sasa hatimaye inaingia kwenye janga hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nizungumzie pia dawa ya kulevyta aina ya bangi. Pamoja na kukaa na jopo la wanasheria wenzangu ndani ya Kamati lakini mimi nimetoka pale nikiwa niko tofauti kabisa na wanasheria wenzangu. Mimi nitazungumzia bangi kivingine kabisa leo tofauti na ambavyo tumezungumza kwenye kamati.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunaweza tukahangaika na cocaine tukahangaika na heroine ambayo kimsingi hatuizalishi katika nchi yetu hapa, inakuja kutoka katika nchi nyingine. Tumekuwa tukihangaika kuziba mipaka na kununua vifaa vingi vikubwa vya gharama kubwa kwa ajili ya ku-sense hayo madawa ili hatimaye tuweze kubainisha madawa hayo na kuhakikisha kwamba tunayatokomeza. Lakini bado tatizo lipo na ndugu zetu, wananchi wenzetu wanaendelea kuteseka na hizi dawa na athari kubwa imeendelea kusambaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiacha cocaine, heroin na dawa nyingine zinazofanana na hizo, suala la bangi mimi naona ndilo tatizo kubwa sana, kwa sababu bangi inalimwa hata kwenye upenuni mwa nyumba, hata bafuni mtu anaweza akaiveka bangi hiyo na ikalimwa hapo na kwamba mtu atai'bembeleza mwisho wa siku anavuta kimya kimya. Hatuna vifaa ambavyo vita-sense kwamba nyumba hii kuna bangi, shamba hili lina bangi.

Mheshimiwa Spika, sasa basi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Maoni yangu; kwa nini suala hili la bangi tusilichukue tukakaa upya tukajadiliana ili ikiwezekana bangi hii tui-process na tuweze kujenga viwanda ambavyo vitapunguza makali ya ile bangi ili bangi hii iweze kutumika kwenye maeneo mbalimbali? Kwa sababu wako watu wakitumia hivyo wanaweza kulima zaidi anaweza kufanya hii na mwingine anavuta tu kama sigara. Pia nitoe mfano kuna nchi ya Zimbabwe wanalima bangi na tayari wameshaipitisha na ni biashara inaingiza Pato la Taifa. Jamaica, Marekani, Korea Kaskazini kwa nini sisitusi-process tukapunguza makali na hatimaye watu wakaitumia kadiri mtu anavyoona. Sawasawa na sigara wanasema tumia lakini ni hatari kwa binadamu wameweka caution pale, kwa hiyo mtu ana hiari kuitumia au kuiacha, kuliko kuacha Pato hili la Taifa linaendelea kutokomea wakati watu kila nyumba na katika maeneo mbalimbali wanaendelea kuitumia hii bangi na hatuna vifaa vya ku-sense hiyo bangi kuibaini.

Mheshimiwa Spika, asante sana naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, atafatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili mimi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Pia niipongeze Serikali kwa kuleta muswada huu wa marekebisho ya sheria. Kama ilivyosomwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali marekebisho ya sheria yatagusia sheria tatu. Sasa kuna sheria ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu na kwenye marekebisho yamegusa kifungu cha 4, 5, 6, 7 na 8(a) katika Sheria hii ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyoletwa na Serikali ni kwamba, mnataka makosa haya ya usafirishaji haramu wa binadamu yaongezewe adhabu; na ndicho kilichofanyika. Katika marekebisho katika hivi vifungu tunaona kwamba hapo awali kulikuwa kuna nafasi ya mahakama kuchagua adhabu kati ya kutoa faini au kifungo. Lakini kwa marekebisho haya tunaona sasa kifungo ni adhabu ya msingi kwa makosa yote yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, halafu kunakuwa pia kuna adhabu ya ziada ambayo ni ya kutoa faini.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye marekebisho haya haikutosha kuishia hapo kuna marekebisho ya Kifungu cha 13 ambacho chenyewe kinaenda kuongeza adhabu, yaani kuweka severe penalty. Kwa maana ya kwamba wale watuhumiwa ambao wanakuwa wamerudia makosa haya ya usafirishaji haramu wa binadamu basi faini yao inakuwa ni ya juu zaidi, kwa maana isiyopungua milioni 100 lakini isiozidi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naunga mkono marekebisho haya na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wengine waunge mkono marekebisho haya kwa sababu yana tija. Kwa sababu ukitizama athari kubwa ya makosa haya ya usafirishaji haramu wa binadamu katika jamii basi kunakuwa kuna umuhimu wa kuweka adhabu kali zaidi ili kuweza kuzuia watu kujihusisha katika tabia hizi za usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, muswada huu umeenda pia kufanya marekebisho katika sheria na kanuni ya maadili ya viongozi wa umma. Na yamezungmzwu hapo awali lakini kwa msisitizo tu, kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati na tulizungumza na Serikali, na wameridhia tunaona wameleta jedwali la marekebisho, na tumeona kwamba wameondoa yale marekebisho waliyokuwa wamependekeza katika kifungu cha 11(2) ambacho kilikuwa kinataka kutamkwa kwa baadhi ya mali kwenye tamko la kiongozi wa umma. Yaani waliweka kuna baadhi ya vitu ambavyo sisi kama kwenye Kamati tumeona ni vigumu sana utekelezaji wake. Yaani unavyomwambia kiongozi wa

umma atamke mali binafsi au vyombo vya nyumbani, samani, furniture vitu kama hivyo; tumeona inakuwa ni ugumu katika utekelezaji. Uzuri Serikali ni Sikivu, kwa hiyo imeleta kwenye jedwali la marekebisho na kifungu hicho naona kimefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Muswada huu pia imeenda kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyo Sura ya 95. Msingi hasa wa marekebisho hayo pia ni kuwaongeza mamlaka kwa maafisa, ambapo maafisa sasa wa chombo hicho, wa mamlaka hii ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyo waweze kuwa na madaraka ya kukamata, kupekua na kuchunguza makosa ya dawa za kulevyo. Kama vile tunavyoona kwenye *Criminal Procedure Act* polisi wamepewa mamlaka hiyo basi na maafisa hawa wa mamlaka hiyo wapewe sasa mamlaka kubwa zaidi kutokana na aina ya makosa haya ya dawa za kulevyo.

Mheshimiwa Spika, muswada pia umingiza vifungu vipyta, kifungu kipyta cha 32(4), kifungu kipyta cha 32(5) ambacho kinaanzisha au kimetoa mamlaka ya kuanzishwa kwa mahabusu. Na kifungu hiki hakijatamka kwamba mahabusu hizi zitaanzishwa katika kila wilaya, hapana. Kifungu hiki jinsi kilivyoandikwa na tafsiri yake kwa upana ni kwamba mamlaka imetolewa ya kuanzisha mahabusu lakini haimaanishi zote zitaanzishwa kwa wakati mmoja lakini zitaanzishwa pale zinapohitajika.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge niwaambie tu, mazingira ya kesi za dawa za kulevyo, sisi tunaishi kwenye jamii, tunafahamu, mazingira yake ni tofauti na kesi nyingine mbalimbali. Kesi za dawa za kulevyo zinahusisha fedha nyingi, zinahusisha watu wenyewe uwezo mkubwa wa kifedha na sisi tunajua fedha inaleta ushawishi. Kwa hiyo mimi naomba tuiamini Serikali na tuwezeshe; kwa sababu marekebisho ya sheria pia yanatokana na changamoto za utekelezaji. Lakini pia marekebisho ya sheria yanakuja kuboresha zaidi yale ambayo tayari yanafanyika. Kwa hiyo katika kuboresha mimi ninaamini kwamba kuanzishwa kwa hizi mahabusu kutaweza kuipa mamlaka hii ya kudhibiti dawa za kulevyo nguvu zaidi ya kufanya kazi yake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, na kwenye sheria kuna *doctrine* moja ambayo inaitwa *The Doctrine of Chain of Custody*. Yaani unapokuwa kuna ushahidi ambaao unahitaji uchukuliwe na na hatimaye ndio ambaao utakuja kutumika katika kesi. Kuna haja kubwa sana ya ule mlolongo mzima wa kuchukua, kuhufadhi, kurekodi kumbukumbu za ushahidi kuna umuhimu sana uende vizuri, uende bila kuwa na mianya yoyote ya upotevu, uende yaani kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira ya kesi za dawa za kulevyta kama walivyozungumza wengine wamesema unakuta kuna wakati mtuhumiwa amemeza dawa za kulevyta na atahitaji muda fulani ambapo atapewa dawa za aina fulani ambazo zitawezesha kutoa zile dawa za kulevyta ambazo hatimaye ndivyo vinakuwa vidhibiti katika hizi kesi za dawa za kulevyta. Kwa hiyo hizo taratibu zote mimi nadhani kwa utaratibu wa kuwatenga watuhumiwa na taratibu zote hizi zikafatwa kwa ufasaha wakiwa wamewekewa na vifaa mahsus katika hizo mahabusu; mimi ninaamini itasaidia sana kesi za dawa za kulevyta ziweze kufanikiwa vizuri na kwa kasi zaidi kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba tutoe imani kubwa sana kwa Serikali. Tayari tunaona mamlaka inafanya kazi kubwa sana, basi tuiongezee nguvu iweze kufanya kazi hii kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini, jambo la msingi ambalo tunalisisitiza ni kwamba, katika kuruhusu kifungu hichi tunaomba sana masuala ya msingi ya kisheria yazingatiwe hasa kwa wale watuhumiwa. Tunataka tuone adherence of human rights; yaani kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinazingatiwa. Pia tunataka tuone ile doctrine ya presumption of innocence; yaani kwamba mtuhumiwa hajahukumiwa kwa hiyo taratibu zote zile za mtuhumiwa ziweze kufuatwa bila kumchukulia mtuhumiwa kama tayari ni mkosaji halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya michango hii naomba sana Waheshimiwa Wabunge waunge mkono Muswada huu ili uweze kupita sheria hizi ziwe zina mabadiliko waweze kwenda kufanya kazi. Ninaomba sana Serikali iangalie utaratibu mzuri sana wa mamlaka hizi za kudhibiti dawa za kulevyta, hii ya Tanzania Bara na ile ya Zanzibar ziweze kufanya kazi kwa ushirikiano zaidi. Kwa sababu tunafahamu changamoto za dawa za kulevyta zipo katika pande zote za Muungano, kwa hiyo washirikiane.

Mheshimiwa Spika, cha mwisho kabisa, ninaomba Serikali; dawa za kulevyta zipo kwa aina tofauti tofauti. Lakini kuna dawa za binadamu ambazo zinaweza kutumiwa na wale wenye addiction ya dawa za kulevyta wakazitumia sasa kama dawa za kulevyta. Kwa hiyo naiomba Serikali itengeneze utaratibu mzuri wa kuweza kusimamia ununuzi wa dawa. Kwa sababu kuna dawa za aina mbili; kuna dawa ambayo wanaita over the counter, kwamba unaweza ukaingia kwenye duka la dawa ukaweza kununua bila kuwa umeandikiwa cheti na daktari. Halafu kuna zile prescription medication ambazo mara nyingi hizo ndiko kuna baadhi ya dawa ambazo watu wenye uraibu wa matumizi ya dawa za kulevyta wanaweza kutumia. Kwa hiyo Serikali iangalie usimamizi, zile dawa ambazo ni prescription medication lazima mtu aende na cheti kwenye duka la dawa ili aweze kuzinunua. Serikali isimamie ili wananchi wetu waweze kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofisi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atafatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Abdallah Ali Mwinyi ajandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Nami nimepata heshima ya kuweza kuwa mwanakamati na kushiriki katika kuchambua muswada huu ambao uliletwa na Serikali, na tukachambua kwa kina na tukafikia maamuzi ya pamoja na tunashukuru Serikali kwa kukubaliana na michango yetu Wanakamati.

Mheshimiwa Spika, fursa niliyo nayo leo nataka kugusia sheria zilizoletwa. Katika Muswada huu wa kubadilisha sheria mbalimbali una marekebisho udhiti na kupambana na madawa za kulevyia Sura Namba 95, pia usafirishaji haramu wa binadamu Sura 432 Ibara ya 3 hadi 9, vilevile Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama tunavyojua, hii biashara haramu ya watu inaleta matatizo makubwa nchini kwetu. Kwa hivyo tuliona kwamba zile adhabu zilizopangwa ziliikuwa hazitoshi. Tukapendekeza kwamba adhabu ile ya kulipa milioni 100 hadi 200, na kama mtu itatokea kurudia tena kosa lilelile basi apate kifungo cha maisha. Kwa sababu shughuli nyingi zinaharabika, kuwarundika watu kama wanyama kwenye magari kuwasafirisha kuwapeleka sehemu mbalimbali wakatumika kinyume na matakwa yao hapo tunaona haki za binadamu zinakiukwa. Kwa hivyo kwa Serikali kuleta jambo hili pengine litasaidia kwa kiasi kikubwa kuwavunja kasi wale ambao wanashughulika na biashara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 13 tulipendekeza kufuta kifungu cha 32 na kuandika upya, kuchunguza makosa chini ya sheria hii. Binafsi katika sehemu hii tuliona kwamba hii mamlaka ya kudhibiti na kuzuia dawa za kulevyia ipewe meno ya ziada. Na kwa hivyo ikapendekezwa kwamba, wawe na fursa ya kuwa na mahabusu ambazo watazisimamia wao wenye ili kuweza kuzuia kutovuja katika mtiririko wao wa kufanya uchunguzi. Kwa sababu kwenye mahabusu hizi za kawaida unachanganya watu wenye kesi za dawa za kulevyia, walioiba kuku, walioiba mbuzi, waliotuhumiwa tu; ambapo taarifa pale zinaweza zikachanganywachanganywa mtu akamwambia hebu nipelekee taarifa yangu hii ili hata mzigo kama umefichwa mahala ukaondoka.

Mheshimiwa Spika, lakini hao watu wakipewa mamlaka hii ya kuwa na uwezo wa kumudu masuala yao wenyewe itatusaidia sana. Kwa sababu tunajua hasara ya dawa za kulevyta taifa linaangamia na wachache wanatajirika kutokana na biashara hii, lakini sehemu kubwa ya wananchi watoto wetu wanaharibika, hali si nzuri na udhibiti unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, na hata ukiangalia unakuta kwamba jinsi ya kuweza kuwapata wale wenyewe, mapapa wakubwa inakuwa vigumu lakini wakipewa maeneo ya ziada hawa mamlaka na kwa walivyo hao wenyewe, na kamanda wao, kama mlivyomwona pale alivyosimama kupokea *tension* yake mambo yanaweza yakabadilika sana na hawa wahalifu wa mambo haya tunaweza tukawakamata kwa kirahisi sana.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine tuliyoweza kuyazungumzia na tukayakubali ni juu ya mamlaka haya ya Sheria ya Maadili. Kwenye sheria hii tuliona mambo mengine ambayo tulishauriana tukakubaliana nayo lakini yale ambayo tumeshauri kama kutoa ripoti baada ya miezi mitatu tumeona kwamba ni jambo la kufaa, kwa sababu watu tuweze kuadhibiti, tuweze kujua mali umepata kwa namna gani, ili utaratibu uliokuwepo uweze kufahamika nafikiri tutakapoweza kuweka vizuri mambo haya, hamna shaka mambo yetu yatakuwa vizuri, kwa sababu lazima tukishakuwa kwenye Sheria kwamba tunadeclare mali zetu, kwa hivyo ukiwa unafahamu mapema itakuwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia haya mamlaka kuweza kuupa nguvu zaidi ili waweze kuchunguza wenyewe mambo yao na kuendesha kesi wenyewe na haina maana kwamba hatutambui kazi nzuri inayofanywa na Polisi ila tutataka ushirikiano zaidi na Polisi. Tunatambua sana kama Polisi wanafanyakazi nzuri, kwa hivyo vyombo hivi viwili vifanye Pamoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukaona pia kwa sababu madawa ya kulevyta yanatembea sehemu nyingi, ukanda wa pwani na nini, tukaomba pia kuwe na ushirikiano zaidi baina ya Zanzibar na Bara ili kuweza kudhibiti, kwa sababu hili shauri la dawa ya kulevyta haliwezi kuwa udhibiti wake hauwezi kuwa wa upande wa mtu mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya kuimarisha mamlaka hii siyo kama tunapora mamlaka ya Polisi na kazi zake lakini tumeona iko haja ya kufanya hivyo. Madawa ya kulevyta kama tunavyoona ni tatizo kubwa kwa hivyo tushirkiane na maelekezo ya Serikali na tuupitishe Muswada huu ili tuweze kupunguza kadhia hii. Ahsante sana.(Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kama walivyotangulia kusema Wabunge wenzangu Muswada huu umekuja na marekebisho ya Sheria Tatu, nikianza na Sheria yetu ya kwanza ambayo inahusiana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu naungana moja kwa moja na Wabunge wenzangu waliotangulia kusema kwamba tunashukuru sana kwa sababu Serikali imeona unyeti wa jambo hili na nachelea kusema kwamba mambo haya usafirishaji haramu wa binadamu na biashara ya madawa ya kulevyaa waathirika wakubwa zaidi ni vijana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali imeona haja ya kuongeza adhabu kwenye mambo haya hasa hasa haya ya usafirishaji haramu wa binadamu. Nami kwa kutoa tu mawazo yangu kwa sababu kuna mazingira ambayo Serikali imekwishaona ya kujirudia kwa makosa haya, kwamba mtu anahukumiwa mara ya kwanza anapewa adhabu, mara ya pili anarudia tena ya tatu na Zaidi, ninaomba tuone namna ya kuweka adhabu ya kifungo cha maisha bila mbadala wa faini ili tuweze kudhibiti watu hawa, kwa sababu biashara hii inakwenda ku-determine moja kwa moja haki za binadamu za watu wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la mabadiliko ya Sheria hii inayohusiana na Udhibiti wa Madawa ya Kulevyaa nami niungane na Wabunge waliotangulia kipongeza Serikali kwamba, bado inaendelea kuangalia namna mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunadhibiti biashara hii. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nkinukuu takwimu zilizotolewa kwenye taarifa ya hali ya dawa za kulevyaa ya mwaka 2021 ya nchi yetu iliyotolewa na Tume yetu ambayo inatoa taarifa kuanzia mwaka 2021 mpaka Juni 2022, taarifa hii inaonesha kwamba kwa miaka karibu Tisa tangu mwaka 2012 mpaka 2021 kumekuwa na uongezeko mkubwa sana wa kilo za madawa ya kulevyaa hasa heroin yanayokamatwa kwenye nchi yetu. Kuongezeka huku cha kushangaza hakuendi sambamba na kuongezeka kwa watuhumiwa wanaokamatwa. Maana yake ni nini, watuhumiwa wale wale wanaokamatwa idadi ile ile ongezeko dogo sana au pungufu dogo lakini kiwango cha dawa zinazokamatwa kinaongezeka. Nitoe mfano takwimu za mwaka 2021 zinaonesha kwamba watu 588 wamekamatwa wakiwa *in possession* ya heroin, madawa ya kuleya aina ya heroin na takwimu hizi zinaenda sambamba na zile takwimu za mwaka 2014 ambapo watu 584 walikamatwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 watu hawa 584 walikuwa na kilo 400 za heroin wakati mwaka 2021 watu hawa hawa 588 walikuwa na kilo zaidi ya 1,500

ya heroin. Mimi naomba kui-challenge Serikali wao wametoa sababu kwenye taarifa yao kwamba hii inasababishwa na kuongezeka kwa ushirikiano kati ya wananchi na Tume yetu na vyombo vyetu ambayo imesaidia kupatikana taarifa kwa wepesi zaidi na hivyo wamekamata kiwango kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, hii ingekuwa ni sababu pekee nadhani tungakuwa tumeona ongezeko la watu sambamba na ongezeko la kilo, sasa hii mimi nachelea kusema inatuonesha kwamba kunaweza kuwa na watu wale wale ambao adhabu zetu zinawapa nguvu ya kurudi kwenye jamii na kwa vile *tumesha-establish* na Wabunge wenzangu wamesema kwamba hii ni biashara ambayo ni organized imepangwa vizuri kimkakati na inafanyika kwa watu wenyewe uwezo mkubwa wa kifedha, maana yake wanapata nguvu ya kufanya zaidi wanapata uwezo mkubwa zaidi wa kifedha na hata udhibiti wao nadhani unakwenda kuwa mgumu zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili la kilo nyngi zaidi za dawa za kulevyia zinaashiria ongezeko la idadi ya watu ambao wanaathiriwa na dawa hizi za kulevyia. Kama Serikali inaamini kwamba kuanzisha mahabusu private kwa Tume hii ya kuwa ina-handle watu hawa inakwenda kupunguza idadi ya kilo hizi na hivyo kupunguza idadi ya waathirika, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Lakini tu nitoe pendekezo langu na ushauri wangu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba naunga mkono hatuwezi tuka-ignore ukweli kwamba bado rasilimali fedha ni tatizo. Bado ni kweli kwamba kuna mahabusu ambazo bado tunahitaji ziwepo lakini hazipo kwa sababu za kibajeti, bado tunahitaji vituo vingi zaidi vya Polisi lakini havipo kwa sababu ya changamoto za kibajeti, hivyo kama tumeamua kwenda kuanzisha mahabusu hizi ninaishauri Serikali iangalie kwanza na kutoa kipaumbele kwa Mikoa mikubwa ya kimkakati ambayo takwimu zinaonesha kwamba ina mzunguko mkubwa wa biashara hizi ili sasa tuanze kudhibiti kule na kadri rasilimali fedha zinavyozidi kupatikana basi tuende na sehemu zingine. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba pia wakati tunaanzisha mahabusu hizi tuisahau suala zima la haki za binadamu ili mwisho wa siku tusije tukazitumia hizi sasa kama kichaka, watu wakiingia kule akija kutoka tumemsahau. Tumeona kwamba hata kuna kipindi Mheshimiwa Rais alipiga kelele kwamba Majeshi yetu ya Polisi kuna namna yanatumika kuvunja haki za binadamu, basi hebu tuendelee kuhakikisha kwamba tuna-withhold haki za binadamu ili hizi mahabusu zetu ziendelee kuwa zinaangalia haki hizi.

Mheshimiwa Spika, pia tuendelee kutoa mafunzo kwa watumishi wetu wanaohusika kwenye suala zima la *ku-handle* haya madawa ya kulevyia ili waendelee kuwa na uadilivu, waendelee kuendana na kasi ambayo Serikali

yetu inaona kwamba ni muhimu tuende nayo ili tupunguze changamoto hizi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nami kwa hoja hizi naomba kuliomba Bunge lako Tukufu kupidisha mabadiliko haya kwa sababu ya tija kubwa inayokwenda kuwa nayo kwenye jamii. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Ali Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, mto aho hoja ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa wasaa huu wa kuchangia huu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022 ambaa umelenga kurekebisha Sheria Tatu. Sheria ya kwanza ni Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyaa Sheria ya Kanuni ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, hakika wenzangu wengi wameyazungumza na kwa kiasi kikubwa wamenifilisi yale ambayo ningependa kuyachangia lakini ningependa tu kusitiza na kuwekea mkazo maeneo machache ili kuongeza uelewa na kwa nini Bunge hili Tukufu liunge mkono sheria hizi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, katika Kamati sheria yoyote ambayo inayoletwa lazima iwe na sababu ya kwenda kurekebishwa. Sheria ni kitu hai kama binadamu kama vitu hai vingine vyovyo ambayo vikiendelea katika mchakato wa utekelezaji wake mapungufu yanaonekana na watu wanakaa wanaamini wapi tuende kurekebisha ili azma yetu ile ambayo tumeipanga iweze kutekelezeka vizuri. Katika haya yamekuwa vilevile.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia zaidi hii Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa za Kulevyaa. Ndani ya Kamati baada ya kupokea maeleo mazuri ya awali ya Serikali, Wajumbe wengi walikuwa wanafikiria mambo makuu matatu katika mabadiliko ya aina yoyote. Kwanza ni haki za binadamu, pili ni rasilimali watu na rasilimali fedha ambazo zitatumika kisawia na la tatu, utekelezaji wake utaleta ufanisi au la. Kwa vigezo vyote hivyo vitatu tumeona bayana kabisa kwamba taasisi hii imeletwa kwa sababu za msingi kabisa.

Mheshimiwa Spika, huko tulikotoka kesi zinazohusiana na masuala ya madawa ya kulevyaa nyingi sana zinashindwa Mahakamani kwa sababu kama Mheshimiwa Zainab Katimba alivyosema *doctrine of chain of custody*, ili uweze kushinda kukusanya ushahidi kwa ufanisi mkubwa lazima taasisi moja toka mwanzo mpaka unavyofikisha kesi Mahakamani iwe *in control*, iwe imedhibiti

maeneo yote. Hiyo ndiyo sababu kubwa kabisa ya kuingiza na kuipa mamlaka hii taasisi ya kuwa na mahabusu, hawakuamua tu kuwa na mahabusu bila ya sababu, sababu hii ni ya msingi kabisa ambayo itawezesha Serikali kushinda hizi kesi. Hawa watu wa madawa ya kulevyta ni watu wenye rasilimali fedha kubwa sana ambao wanaweza kuleta ushawishi na kuwarubuni watu wengi katika taasisi mbalimbali, lakini mkiwa na mlolongo mmoja kutoka mwanzo mpaka mwisho inasaidia hizi kesi kuzishinda Mahakamani, hilo ndiyo jambo la msingi na kubwa pamoja na mengine yote ambayo wenzangu wameyachangia. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ningependa kuzungumza la ujumla hapa sheria hizi mbili ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa na Kulevyta zote zinagusia eneo moja la masuala ya ulinzi na usalama. Haya yote ni masuala ya jinai, haya yote ni masuala ya ulinzi na usalama wa Taifa na yanapaswa yaguswe pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Sheria moja hii ya Kudhibiti Madawa ya Kulevyta ni Sheria ya Tanzania Bara tu, wakati Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ni Sheria ya Muungano. Hapa kuna jambo ambalo tungependa tulitazame kwa ujumla wake. Masuala ya madawa ya kulevyta ukiyazungumza na ukiyajadili na wataalam wanavyotuambia ni kwamba yanapita sehemu zote. Sehemu ya Zanzibar yanapita, sehemu ya Bara yanapita na kuwa kuna taasisi mbili ambazo haziingiliani, ufanisi wake wa utekelezaji wa kazi inabidi taasisi zote mbili zizungumze badala ya kuwa na taasisi moja. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ningependa tuone kama kuna uwezekano ama Kamati zetu za Katiba na Sheria au Bunge au uongozi wa juu pande mbili zote za Muungano zikae ziyajadili haya mambo tujue jinsi gani ya kuleta sheria ambazo kimsingi zinatakiwa ziwe za Muungano na zile ambazo kila mtu anaweza akazileta kwa upande wake kwa mujibu wa mfumo mzima wa Katiba yetu na Sheria za Muungano na ambazo siyo za Muungano. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninapenda kuwasihhi wenzangu tuunge mkono marekebisho haya ya sheria na nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete leo akisaidiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali karibu kwa mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kuunga mkono hoja. Kipekee kabisa niipongeze sana Kamati ya Bunge ya Sheria kwa mchango wake mzuri waliota lakini pia michango iliyotolewa na Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja hii iliyowekwa mbele yetu ya marekebisho ya Sheria ya *Miscellaneous Amendment No. 2* ya Mwaka 2022, ambayo ndani yake inabadilisha au inafanya marekebisho katika sheria zetu tatu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, binafsi niwapongeze sana Wajumbe lakini kwa kipekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Attorney General kwa yeye mwenyewe kuona kwamba kuna umuhimu wa kuleta sheria hii sasa hivi lakini kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa sababu sheria hizi zinaenda kuipa sura nzuri nchi yetu katika uwanda wa mahusiano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Zuio la Usafirishaji wa Binadamu inatupa heshima kubwa sana nchi yetu kwa sababu, dunia imekumbwa na tatizo kubwa sana la biashara isiyokatika ya kuza watu nje lakini katika vigezo mbalimbali. Sheria hii inafanya marekebisho katika kipengele cha Nne, kipengele cha tano, kipengele cha Sita, kipengele cha Saba na kipengele cha Nane. Pia kipengele Namba 13 na kuongeza sasa badala ya faini na kuiachia Mahakama kuamua vipengele vya vifungo ikiwa ni sehemu kwa lugha ya kisheria au kwa lugha ya Kiingereza wanasema ni *mandatory sections*. (Makof)

Mheshimiwa Spika, vipengele hivi kwa kweli vilikuwa vinaleta ukakasi mkubwa sana kwa sababu, wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa wanafanya biashara hii mpaka inaonekana kwamba ni biashara sahihi kufanyika, lakini kwa kuleta vipengele hivi Bunge lako nataka niwashawishi Wabunge wenzangu kwamba tupitishe sheria hii kwa sababu sasa inaenda kutoa mwarobaini wa wale ambao walikuwa wanafanya biashara hii wakiamini kabisa kwamba wao ni watu wenye haki ya kuuza watu wengine duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa ninaipongeza Serikali na mimi ninaunga mkono sana hoja hii ya kubadilisha au kuongeza baadhi ya vipengele katika Sheria yetu hii ya Madawa ya Kulevyo.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kulevyo yameumiza vijana wengi sana yameharibu rasilimali ya nchi lakini pia yamepoteza nguvu kazi kubwa ya Taifa letu. Kwa kuongeza vipengele hivi ambavyo vimeletwa sasa ambavyo vinatoa ushahidi wa dhati juu ya nia ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya kupambana na kuhakikisha kwamba nguvu kazi ya Taifa hili inaendelea kuhifadhiwa ni jambo kubwa la msingi ambalo linapaswa kuongelewa kwa lugha kubwa lakini kupazwa sauti ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka niwatoe wasiwasi baadhi ya wazungumzaji ambao walichangia katika hoja hii, ambao walionesha kwamba wanao wasiwasi kwamba viko baadhi ya vipengele vya kisheria ambavyo vinakwenda kuondoa mamlaka katika baadhi ya mamlaka zao. Kwa mfano, ndugu yangu Mheshimiwa Mpina amezungumza juu ya kwamba uundwaji wa sheria hii au marekebisho ya sheria hii yanakwenda kuinyima haki Jeshi la Polisi katika nguvu yake ya kuendelea kushikilia wafungwa au wale watu wanaoshutumiwa kutenda baadhi ya makosa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Mpina kwamba sheria hii inayowekwa inakwenda kuipa Mamlaka ya Madawa ya Kulevy siyo kwamba sheria hii inainyima Jeshi letu la Polisi hapana, Jeshi la Polisi inayo mamlaka yake na kitengo cha madawa ya kulevy nayo pia kina mamlaka yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu jinsi gani wale watuhumiwa wanaenda kukaa nataka nimrudishe katika Sheria ya National Prosecution Act ambayo inatoa mamlaka kwa DPP ya kuangalia juu ya uendeshaji wa jela zote au cell zote na jinsi gani wale wafungwa wanaopelekwa katika maeneo hayo wanaangaliwa katika utaratibu ambao unasomwa pamoja na sheria nyngine zikiwemo zile zinazozingatia haki za binaadamu. Kwa hiyo, nataka nilihakikishie Bunge lako lakini pia kuwashakikishia Umma kwamba sheria hii si kwamba inawanyima Polisi mamlaka yao lakini inakwenda kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na hivyo wawe na hakika kabisa kwamba taratibu na sheria zitasimamiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia, sheria hii inakwenda kuweka utaratibu wa jinsi gani Jeshi letu hili au kitengo hiki cha madawa ya kulevy kinakwenda kusimamia utaratibu kuanzia kwenye *investigation*, kukamata mpaka kupeleka watu katika maeneo husika. Kwa hiyo, nilitaka nizungumze hili pamoja na kuunga mkono mchango mzuri uliotolewa na Waziri wetu wa nchi juu ya kwamba sheria hii inakwenda kuweka taratibu nzuri ambazo zinakwenda kuhakikisha kwamba ulinzi wa ushahidi nao pia unaangaliwa, hivyo wasiwe na wasiwasi Watunga Sheria kwamba kuna tatizo litaenda kujitokeza katika hilo.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa mchango wanguhuo mfupi, naunga mkono hoja na nnawaomba Wabunge wenzangu tupitishe sheria hizi kwa nguvu moja.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, uje uhitimishe hoja yako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kushukuru tena kwa kunipatia fursa hii kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, tumepata jumla wa Waheshimiwa Wabunge 11 ambao wamechangia Muswada hapa na Waheshimiwa hawa ni pamoja na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Yahaya Massare, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, Mheshimiwa Zainabu Katimba, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Ng'wasi Kaman, Mheshimiwa Abdallah Ally Mwinyi na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa sababu mimi ni Wakili namba moja sasa kwa seniority ya Wanasheria katika kazi zetu mara nyingi Senior Counsel anakuwa na mwininge ambaye anakuwa pembeni kwake. Nikutoe wasiwasi Ridhiwani Kikwete pamoja na nyadhifa nyingine yeye ni wakili ambaye amesajiliwa kwa namba 1582. Nilisema vile vile chochote tunachofanya hapa kama Serikali tunafanya vilevile succession plan kuhakikisha tunawajengea uwezo wote ambao wanafanya kazi kwa niaba ya Serikali kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri, tumepokea maoni mazuri sana ambayo yamelenga kuboresha sio Muswada tu bali ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi tosha kabisa kwamba suala ambalo limekuwa mbele yetu ni suala ambalo lilihitaji sisi kama Serikali kuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, nafikiri kwa jinsi ambavyo wewe mwenyewe umeshuhudia michango yao bora lakini vile vile na ufanuzi waliooutoa kulinda *integrity* ya Kamati yao imeonesha jinsi ambavyo Serikali na wao tulipata muda wa kutosha kujadili Muswada huo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yapo mambo kadha wa kadha ambayo yametolewa yale ya ushauri, kwa ufupi tu niseme kwamba, yote kama Serikali tumeyapokea kwa sababu lengo la Serikali siku zote ni kuhakikisha kwamba tuna mifumo mizuri zaidi ya sheria na tuna sheria ambazo ni bora kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanalindwa na sheria, lakini vile vile wanakuwa na fursa nzuri ya kushiriki katika shughuli zao za kimaisha na kiuchumi. Nchi yetu inafuata vile vile utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nigosie baadhi ya mambo kadhaa lakini nikishukuru sana maelezo ya utangulizi ambayo Mheshimiwa Kikwete ameyatoa.

Nitapenda nieleze kwa dhana za kisheria na mustakabali wa nchi yetu hasa kuhusu vyombo vinavyosimamia sheria. Kuja na Muswada huu hakukuwa na maana ya kuonesha kwamba vyombo vingine vya kisheria havitekeleza majukumu yake vizuri, kama kuna dosari zinapimwa kuligana na utekelezaji ndani ya sheria zinazowahusu. Kwa hiyo tumekuja na Miswada hii, kwa mfano, Muswada ambao unahu su udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Dawa za Kulevya ni Mamlaka ilioanzishwa na Serikali, ilioanzishwa na sheria na inatekeleza majukumu yake kwa kujitegemea. Kwa hiyo, kwa nini kuna dhana ya wao kuwa na mahabusu, sheria imetumia neno *may* lakini sheria hii hii imetumia maneno kwa kushirikiana na vyombo vingine. Vile vile mahabusu hizi zikianzishwa Waziri mwenye dhamana lazima atahakikisha viwango vyake. Mheshimiwa Simbachawene alieleza kwa undani kueleza mazingira ya kipekee ambayo yanahitajika, ambayo mazingira hayo hayapatikani kwenye Vituo vyetu vya Polisi vya kawaida. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kwa minajili hii basi, ielevweke kwamba mahabusu zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Sheria lazima zianzishwe kwa kuzingatia vile vigezo vyote. Vigezo vya mahabusu zetu ziwe za Polisi, viwe vilivyopo kwenye Magereza yetu maana yake zinajengwa kwa kuhakikisha zimezingatia yale mahitaji ya ujazo, ile nafasi kwa watu wangapi na yale mahitaji ya msingi kwa binadamu ambayo lazima yawepo. Sasa ni kwa msingi kama huu ilielezwa vizuri shida inayokuwepo kwa hawa ndugu zetu wanaoangukia kwenye biashara hii ya usafirishaji wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, anapofanyiwa vile vipimo akapimwa na akajulikana kwa mfano ndani ya tumbo lake amebeba dawa za kulevya labda kete kadhaa utaratibu wa kuzitotoa unaendana na ujazaji wa fomu na hazitotolewi kwa wakati mmoja. Kwa hiyo mkiangalia zile sheria ndio maana kuna zile *observation* fomu na kuna mashahidi na kadhalika. Mahitaji ambayo ni vigumu sana kama tunafuata ile misingi ya haki za binadamu na faragha za binadamu, kuipata kwenye *lockup* zetu za kawaida. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuelewe kwamba kutokuwepo kwa *lockup* za Polisi mahala fulani kusizue mamlaka kufanya kazi zake. Kwa hiyo ndio maana ya kusema kwamba pale mahitaji yanapohitajika *lockup* hizo zitaanzishwa na neno lililotumika ni *may*. Kingine ambacho ningependa vile vile kwa mashirikiano yaliyopo kisheria *lockup* zile kama hazina mahabusu wa dawa za kulevya haitakuwa kizuizi kwa taratibu za vyombo vyetu kutumika vilevile kwa wahalifu wengine waliokamatwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mpina nikutoe wasiwasi kwa sababu hatua ya mtu kuingia mahabusu sio kitendo cha kukurupuka, lazima afike kitu kinachohusika kwa maana ya mamlaka, Mamlaka imkamate mtu, baadaye kuna *lockup register* ambayo mtu atasajiliwa, baadaye kama alivyosema Mheshimiwa Kikwete, Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka yalipoongezwa mwaka 2008 ya kukagua mahali popote wanapozuiliwa wahalifu maana yake ni kwamba kuhakikisha kwamba nchi yetu inazingatia haki za binadamu kwa mtu ambaye hajatiwa hatiani kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo hili ningependa wote ambaao walikuwa na mashaka hii, basi wajue kwamba zikitumika vinginevyo kutakuwa na changamoto nyingine.

Mheshimiwa Spika, kingine ni ile dhana kufikishwa mahakamani kwa hawa watu kutafuta sheria zetu na sheria hii imetambua hilo, ndio maana kifungu cha 32 cha Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ambacho kimetambuliwa kisheria kwenye hii sheria Sura 95 kinasema mtu aliyekamatwa atafikishwa mahakamani as soon as is practicable, maana yake mapema kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Makamba ameeleza mfano wa nchi kadhaa ambazo zina utaratibu huu. Kwa hiyo jambo hili niliona niwatoe wasiwasi wote ambaao huenda walikuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwa ujumla Sheria ile ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, mwanzoni kufungwa haikuwa sharti la lazima, kwa hiyo tulichokifanya Serikali imeona baada ya tafiti na baada ya kuangalia mikataba ambayo Serikali imeridhia, sasa ni kuona kwamba angalau kuwe na kifungo kama adhabu ya lazima na zaidi yake sasa pale ambapo kuna sababu za nyongeza, basi kunakuwa na faini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama tumefuatilia Muswada na Jedwali letu mtaona kwa mfano chini ya kifungu cha nne kifungu ambacho zamani kilikuwa cha hiyari ilikuwa option miaka miwili hadi kumi sasa ni lazima, miaka 20 hadi 30, kwa maneno mengine isiyopungua 20 na isiyozidi 30. Kifungu kidogo cha 5(3) zamani ilikuwa mwaka mmoja hadi miaka saba lakini ilikuwa ni option kwa sasa ni mandatory, si chini ya miaka mitano na isizidi miaka 10. Kwa wale waliokuwa wanasema adhabu ya maisha kifungu cha 5(4) zamani ilikuwa miaka isiyopungua 10 hadi 20 kwa hiyari, lakini sasa ni lazima, miaka isiyopungua 30. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sheria inaposema isiyopungua 30 maana yake Mahakama kwa kuzingatia mazingira ya shauri husika inaweza ikapandisha kutoka 30 na kwenda juu *ime-set minimum*. Kwa hiyo hili nafikiri ni jambo ambalo ningesema kwamba kwa sasa ambacho kitafuatia ni kuona jinsi ambavyo tunasimamia sheria hii ili kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuona tunafanya nini sisi kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sheria yetu hii na mamlaka yetu hii na Mamlaka ya Zanzibar tumepokea ushauri na nafikiri ni jambo ambalo litaendelea kufanyiwa kazi. Hata kwenye Kamati tuliwaahidi kwamba, jambo hili tutaendea kulitolea taarifa.

Mheshimiwa Spika, suala la hoja ya bangi, mirungi kama sheria haiharamishi sheria zetu zinaharamisha vifungu kuanzia cha 12-15 cha sheria mama tunayojadili imeongelea jinsi inavyoharamisha makosa haya. Kwa hiyo mjadala unaoendelea sasa hivi na sio Tanzania tu ni je, twende zaidi ya kifungu chetu cha 13. Kifungu cha 13 hata sasa kwa matumizi mahsusimtu anaweza akaomba kibali kwa *Commissioner General* na akaruhusiwa kuwa na kiasi cha dawa hizi kwa matumizi ambayo maana yake yamerasimishwa na sheria, lakini kuingia kwenye *commercial* au *demand* kubwa na kadhalika hapana, haya yameharamishwa na sheria hii na mengineyo yatakayofuata.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri kuanzia wa Kamati na wa Bunge hili la kufanya utafiti mkubwa ili tuone jinsi ambavyo nafikiri baadaye nchi yetu itafanya maamuzi kwanza kuhusiana na mikataba ya Kimataifa ambayo sisi tumejifunga nayo, lakini baadaye kuja kuona tunafanya nini na sheria zetu. Kwa hiyo hili nalo ningependa Waheshimiwa Wabunge wasione kwamba ni jambo ambalo halitafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nishukuru sana na nizidi kuomba tu kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyo ada kazi yetu mojawapo kati ya kazi nyingine ni kuhakikisha tuna sheria zenye tija na tutaomba sana tuendelee kupokea maoni hata baada ya hapa kwa sababu ndio kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika Muswada huu na kushiriki na wale wengine ambao kwa njia moja au nyingine wameufuutilia, sasa naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Kwa mujibu wa kanuni ya 34 tutaendelea.

Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**SPIKA:** Kamati ya Bunge zima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2022**

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 4

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu cha 4 kina Marekebisho ya Serikali, lakini nilikuwa nayapitia hapo juu Mwanasheria Mkuu wa Serikali hebu tusaidie, haya marekebisho yanasema tuongeze maneno or to both baada ya maneno *ten years* yanayotokea kati ya *ten years and substituting*. Sasa nikisoma hapa naona marekebisho ya humu kwenye ule, naona kama sheria yetu sijui itakuwa inasomeka namna gani hebu tusaidie.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, tulileta mapendekezo ya kuongeza maneno or to both kwenye kifungu mama kabla ya marekebisho ili kiondolewe nacho. Pale ilipokuwa inaishia ile phrase *years* kwenye kifungu mama kwa mfano kifungu cha nne kwa hiyo kabla ya kufanya *substituting* maneno or to both yanaondolewa, kwa sababu yalikuwepo ili sasa, lengo lilikuwa ni lile lile habari ya kuja kuhakikisha kwamba angalau sheria inaanza na kutoa ile adhabu, *custody halafu* ile *addition* ndio. Bila kuyaondoa haya kwa maneno mengine, tungetoka hapa na kukiandika upya kile kifungu, maneno yale yangefanya kifungu kizima kisiwe na maana.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa ajili ya uelewa ili nijue tunachopitisha hapa, kifungu chetu kwa sasa kitasomeka vipi Bunge likishahojiwa hapa? Nisaidie hivyo ili niwe na fuatilia hapa mbele. Tumia tu muda wako, tafuta hicho kifungu mama, kwa sababu mimi niliyonayo hapa ina maneno yanayoashiria yanatoka kwenye kifungu mama halafu na haya ambayo yanarekebishwa. Kwa hiyo

marekebisho haya yaliyoletwa na jedwali lako maana yake yamekuja kurekebisha siyo kifungu mama, yanakuja kurekebisha yale ambayo ulikuwa umeleta kama marekebisho hapa Bungeni. Kwa hiyo, nisomee namna kitakavyosomeka sasa hiki kifungu na kwa usahihi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa kitasomeka: “A person who commits any of the offences or acts specified under this section shall on conviction reliable to imprisonment for a term of not less than twenty years but not exceeding thirty years, provided that, the court may, in addition to imprisonment, order the convicted person to pay a fine of not less than fifty million shillings but not more than one hundred million shillings.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Attorney General ukitusomea hivyo kinasomeka vizuri kabisa, lakini hili jedwali lako sasa la marekebisho ambalo linasema *in clause four by inserting the words or to both immediately after, unaongeza wapi*, kwa sababu haya ya ten years yanatokea kwenye kile kilichopita, yaani hivi ulivyosoma ndivyo kinavyosomeka hata bila hili jedwali, ila marekebisho yale ambayo umeshajadiliana na Kamati ukikisoma sasa hicho kilichopo cha zamani na haya marekebisho ndio kinakwenda vizuri, haya maneno or both hujayasoma hata wewe, sasa hivi nilivyosema kinasomekaje, hujayasoma hata wewe. Kwa hivyo, uko sahihi kwamba haya marekebisho ambayo unayasema *by inserting the words hakuna ku-insert chochote hapa kwenye hiki kifungu*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Tungeweza *tusi-insert pale* lakini tungekuja tena huku mwisho baada ya marekebisho *ku-delete* kwa sababu mwisho wa subsection five unayaona yanasomeka or to both.

**MWENYEKITI:** Labda niseme hivi kwa ujumla na Mheshimiwa Ridhiwani upo hapo muwe mnatazama wote, vifungu hivi vilivyorekebishiwa na haya maneno sijui *substituting* yameingia hapa yameingia hapa. Ukiyaingiza haya maneno kwenye haya marekebisho uliyokuwa umeliletea Bunge kabla yaani sheria inakuwa haisomeki kwa ule mtiririko.

Kwa mfano, hii Na. 4 niliposema tusomee, itasomeka vipi sasa? Inasomeka vizuri zaidi, ama inasomeka kwa kuelewaka, na ndivyo inavyotakiwa, ukisoma ile ya mwanzo na yale marekebisho uliyokuwa umeyaleta kwenye Muswada bila haya marekebisho ya ule Muswada. Sijui kama naelewaka! Haya, kama umenielewa na kama ndivyo, haya marekebisho yako sasa, hapa kwa sababu muda uliofika ni wa kulihoji Bunge, na kile ulichokisoma hakina haya maneno; haya mabadiliko yako, kama nimeelewa sawa sawa na sheria inasomeka vizuri, sisi Bunge tutayakataa, tutayakubali yale ambayo uliyaleta mwanzo.

Haya hebu toa hayo maelezo halafu ndiyo tujue tumeenda sawa sawa na sheria yetu tumeiandika vizuri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu kidogo cha (5)...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza tuko kwenye clause four.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yes.

**MWENYEKITI:** ...ambayo clause 4 inasomeka clause kwa sababu inabadilisha yale ya kule kwingine. Sasa hii clause 4 ndiyo tunaisoma na hapa haina hicho kifungu unachosema kidogo cha (5) sijui kinakuja wapi? Mimi sina hapa mbele. Hebu nisaidie.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, clause 4 itakuwa: "The Principal Act as amended in section 5(4) it is the words..."

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja. Rudia kidogo hapo twende sawa sawa, yaani anza upya kusoma. Ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *The Principal Act as amended in clause 4(5) by deleting the words "five million shillings but not more than one hundred million shillings or to imprisonment for the term of not less than two years and not more than ten years" and the words to both took them, substitute the words to imprisonment for the term of not less than 20 years but not exceed 30 years provided the court may in addition to imprisonment or the convicted person to pay a fine of not less than 50 million shillings but not more than one hundred million shillings.*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa baada ya hayo maelezo, Mheshimiwa AG tusomee namna kitakavyosomeka ili nilihoji Bunge.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 (5) sasa kitasomeka: "A person who commits any of the offences or Acts specified under this section shall on conviction be liable to imprisonment for a term of not less than 20 years but not exceeding 30 years provided that the court may in addition to imprisonment order the convicted person to pay a fine of not less than 50 million shillings but not more than 100 million shillings.

**MWENYEKITI:** Sawa. Ahsante Mheshimiwa AG unaweza kukaa. Nimeshaletewa ile sheria mama yenyewe, haya maneno "or both", ni kwamba yalisahaulika kwenye kusoma kile cha mwanzo, lakini ambacho Bunge

linarekebisha ni hiki cha pili ambacho kikienda kusomwa kule, maneno “or both” hata hayana maana yoyote, kwa sababu tunaenda ku-substitute.

Sasa tukiyakubali haya ni kama vile, yaani kile kifungu kitaendelea kuwepo fulani hivi. Kwa hiyo, kwa sababu haya maneno yako kwenye original, hayana sababu ya kuja kurekebishwa hapa. Sijui kama naeleweka. Hiki kifungu ambacho Bunge linapitisha, ni kwamba yale maneno ambayo tunataka Bunge liyaweke, ndiyo ambayo hasa tunataka kuhoji. Yale ambayo yanaondolewa, tusililetii Bunge sasa hivi, kwa sababu namna hiki kifungu kilivyo, yaani tukikipitisha na marekebisho ya Serikali, maana yake ni kwamba tumekubali maneno “or both” yaingie hapo unaposema. Sasa hayana maana yoyote kwa ngazi hii ya utungaji sheria. Kwa ngazi hii haina, kwa sababu siyo marekebisho ambayo tunataka sheria isomeke vizuri. Kwa hiyo, hicho kifungu namna ulivytosomea, kinaendana na yale marekebisho uliyokuwa umeyaleta kwetu na Kamati imeshayapitia.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmelewa, nitakachokuwa nawahoji ni kifungu alichokisoma Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambacho kinaendana na Marekebisho ya mwanzo yaliyoletwa bila haya marekebisho ya pili. Nadhani tumelewana vizuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 5

**MWENYEKITI:** Kifungu cha (5) pia kina maneno kama hayo hayo, kwa hiyo tutarudi kwenye ule ule mjadala. Haya maneno yaliowekwa sijui “or both”, halafu tena substituting na yenyewe yanakuja kukichanganya hiki kifungu. Si ndiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

Waheshimiwa Wabunge, mmelewa ninachojaribu kukisema? Kuna maneno tukyaongeza, tunakuwa tunaongeza kwenye ile sheria mama na siyo kwenye marekebisho ambayo hasa ndiyo tumeletewa kwa ajili ya kubadilisha.

Waheshimiwa Wabunge, nawahoji sasa. Kwa hiyo, mabadiliko ninayokuwa nayasema ni yale yaliyomo humu kwenye Muswada.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6

Kifungu cha 7

**14 SEPTEMBER, 2022**

Kifungu cha 8

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 9

**MWENYEKITI:** Hiki kifungu cha 9 nimeletewa ujumbe hapa kwamba 9 1(c), hakuna. Hebu tazama vizuri. Ni namba ngapi Mheshimiwa Salome Makamba?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 wameandika kwamba kifungu kinachorekebishiwa ni 9(1)(c), lakini kwenye sheria mama hicho kifungu hakipo. Kwa hiyo, ni Ibara ya 18, siyo ya 9.

**MWENYEKITI:** Aah, okay sawa. Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 10

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa kabla hatujahamia kwenye kifungu cha 10 kwa sababu kinaingia kwenye sheria nyingine, yale maelezo niliyokuwa nimeyatoa hapo mwanzo tulipoanza na marekebisho aliyoyaleta Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya (a), (b), (c), (d) na (e) yote yanaingia kwenye mtindo huo huo kwamba Bunge halirekebishi sheria yake ile nyingine, ila inarekebisha ile sheria yake nyingine kwa Muswada ule ulioletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Yale maneno ambayo yapo kwenye ile sheria iliyopita, sicho tunachorekebisha. Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza akayaweka namna ambavyo sheria itasomeka vizuri ile ambayo tunaipitisha leo na Bunge.

Sasa tunaingia kwenye sheria nyingine ya Drug Control and Enforcement Act.

Kifungu cha 10

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 11

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 12

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 13

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 14

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja, najaribu kutazama hapa. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuna neno “police” sijui linafutwa sehemu gani kwenye jedwali? Mnisubiri kidogo Waheshimiwa Wabunge.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali nisaidie hiki kifungu Namba 14 neno “police” linafutwa hapo. Clause 14, by delete (a) deleting the words “police” appearing in the opening phrase of the proposed section 32 A (1). Umeshapapata hapo! Clause 14. Ile tumetoka 13 tumepitisha, sasa ni clause 14. Hiyo 14 marekebisho uliyoyaleta yanaashiria tufute neno “police” hapa kwenye opening statement. Sawa, hebu tusomee, kitasomekaje tukifuta.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitasomeka: “the Commissioner General or officer in charge of the police station may by writing authorize any officer to.”

**MWENYEKITI:** Tukifuta “police” hapo, halafu tukaacha maneno “a police station.”

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yah, ni sawa.

**MWENYEKITI:** Somebody else will be in charge of that police station who is not police.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yah!

**MWENYEKITI:** Okay. Aah, somebody else who is not a police officer.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, logic yake hapa ni yeye sasa yale mamlaka ambayo tumesema, kwa sababu ndiyo law enforcer katika sheria hii, anaweza akawatumia vyombo vingine kutekeleza yale ambayo ana-initiate. Ndiyo maana kule nyuma kulikuwa na kile kifungu kile cha yeye kufanya *re-consultation* na *re-collaboration* na vyombo vingine na kwa mujibu wa sheria nyingine zilizopo. Yaani ni sawa na atakavyoendelea kutumia *lockup* nyingine za Polisi. Maana yake kilichokuja, kwa mfano, tukiangalia marekebisho ya mamlaka *may establish cell* zake, lakini haitazuia kwa sasa kutumia zile cell za vyombo vingine ambazo viko established.

**MWENYEKITI:** Jambo ninalotaka kulielewa, Commissioner General anayeongelewa hapa ni Commissioner General wa Madawa ya Kulevy. Halafu huyu Commissioner wa Madawa ya Kulevy or any officer in charge of a Police Station. Ukitisema any officer in charge of a Police Station, unataka huyu Commissioner General awe na powers kwenye Police Stations, yaani watu wake wawe wanapitiliza tu kule. Maana kwenye *cells* ambazo ni zake *that is something else*, lakini kwenye *cells* ambazo ni za police, yaani any officer in charge, yeye ataweka watu wake kwenye *hizo* police au atakuwa anawatuma? Maana unasema “*in charge of a particular police station.*”

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongee sasa practically.

**MWENYEKITI:** Okay, sawa, utanisaidia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia leo hana *lawfull establish lockups*, lakini anatumia zile zilizopo za Polisi. Sasa kunatakiwa ziwepo *lockup* ambazo yeye anazianzisha na yale mahitaji ziwe specified kwa vigezo ambavyo Waziri mwenye dhamana atakuwa ame-approve.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapofika Kituo cha Polisi chochote, kuna *lockup register*. Kwa hiyo, wale watu ambao kwa mfano, si ana mamlaka sasa ya ku-arrest na ku-search, amewapata tuchukulie kesho; mahali pekee atakapohitaji kuwapeleka ni palipo na *law of established custody*; na huku tujue kwamba sheria inamtaka atumie sheria nyingine zilizopo, afanye kazi na vyombo vingine, nao kupitia kwenye Criminal Justice Forum, kwa mfano, ambayo imeanzhishwa na kifungu cha 27 cha National Prosecution Service Act. Maana yake kule kuna yale matakwa ya wao kufanya kazi pamoja.

**MWENYEKITI:** Mimi swali langu ni moja tu, yaani unisaidie hapo uelewa. Huyo ambaye ni officer wa Madawa ya Kulevy anakuwaje *in charge of a Police Station?* That is my question. (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa itoshe hata kama huyu Commissioner General hajapeleka afisa wake pale, hao other law enforcers wa-enforce matokeo ya kazi ambayo wame-initiate kwa taratibu ya sheria nyingine zilizopo.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa mimi ninayoona italeta mgongano, kwa sababu sasa hivi hizo cells hazipo, zilizopo ni za Polisi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yes.

**MWENYEKITI:** Hapa inayozungumzwa, maadam maneno “Police Station” yanaendelea, maana yake siyo lockup zile za kwake, ni zile za Police. Ni mazingira gani tutampata officer ambaye ni wa Madawa ya Kulevyia awe in charge of a Police Station? That is my question. Yaani ukiondoa hapa neno “police”, maana yake kuna Afisa wa Commissioner General atakuwa in charge of a particular Police Station ili aweze kufanya hizi functions. How?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwenye maandalizi yao kwa sasa, na kwa majukwaa yao, upo uwezekano wa wao ku-place watu pale, wa kwao, kwa makubaliano yao, kama ambavyo leo kuna maafisa kadhaa wa Polisi na vyombo vingine, law actors wamekuwa seconded kwenye hii mamlaka. Kwa hiyo, mengine yatafuata; regulations na miongozo ya vyombo. Pia naeleta shida unayoipata...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo itanipa wakati mgumu kweli kukipitisha hiki kifungu kwa sababu sielewi ni mazingira gani afisa huyu anayetoka nje ya Polisi atakuwa in charge wa Police Station, hata kama anaye mtu mmoja, wawili, watatu au kumi kwenye a certain cell ya Police Station, yeye kweli atakuwaje in charge of a Police Station? That is my issue. Anaweza kuwa in charge wa wale watu wake wanaomhusu, wengine wote hawamhusu, atakuwaje in charge of the Police Station. (Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shida kukiondoa.

**MWENYEKITI:** Aah, shukrani, lakini naamini umenielewa hoja. Kwa sababu Afisa wa Madawa ya Kulevyia hawezi kuwa in charge of a Police Station. Police Station atakuwa Polisi ndiyo yupo in charge, huyu mwengine yupo in charge na watu wake. Kwa hiyo, ule utaratibu unaoendelea, uendelee tu; na kama atakapotengeneza hizo cells zake, ambapo hatahitaji Police Station, yeye ataendelea, si tumeshamruhusu. Naamini Wabunge tutakavyofika hicho kifungu tutakuwa tumemruhusu, si ndiyo jamani. Eeh, yeye ataweka utaratibu wake,

Iakini zile ambazo ni *Police Station* tuendelee na wale Polisi, hawa wengine waendelee kushirikiana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali hii tuachane nayo, iakini kwa dhana kwamba ile nilisema pale, hizi *cells* zitakazoanzishwa hata za mamlaka hii, taratibu zitawekwa vilevile *cell* zao kutumika hata na wahalifu ambao watafikishwa pale as long as wanaweza ku-accommodate.

**MWENYEKITI:** Sawa. Hilo limeeleweka kwa sababu pia zile bado hazitaitwa *Police Station*, zitaitwa kitu kingine. Sijui wataziitaje, iakini police wataruhusiwa kuzitumia.

Kwa hiyo, hili nadhani, ili kifungu chetu kiendelee kuwa na maana, kiendelee kuwepo na neno “*the Commissioner General*”, ambaye tunajua ni nani kwa sababu yupo defined or a *Police Officer In charge of a Police Station*, kwa sababu tukiondoa hapa, Polisi tutakuwa tunawapa wakati mgumu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hilo limeeleweka.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. (*Makofij*)

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge, kifungu kinaafikiwa?

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

Kifungu cha 19

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

**14 SEPTEMBER, 2022**

Kifungu cha 20

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

(Bunge lilirejea)

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (Na. 2) Bill, 2022*) ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Bill, 2022*) kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2022 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022  
Ulipitishwa na Bunge)

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuondoa Upungufu ambao umejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (A Bill for an Act to amend certain Written laws in order to keep the laws updated with some challenges observed in its Implementation)

(Kusomwa Mara Tatu)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa Mara ya Tatu.

Waheshimiwa Wabunge kwa kusoma Muswada kwa mara ya tatu tumemaliza kazi yetu ya kutunga sheria. Kwa hiyo, kwa muktadha wa kile tulichokuwa tukikifanya leo, tumefanya marekebisho ya sheria mbalimbali ambazo tulizitunga huko mwanzo, lakini katika utekelezaji wake zimeonekana changamoto na maeneo mengine imeonekana kwa yale maendeleo yanayoendelea hapa nchini na huko kwengine duniani, basi kuna marekebisho ambayo ni lazima tufanye. Kwa hiyo, kwa sehemu yetu kama Bunge, tumeshamaliza kutunga sheria hizi. Kwa hiyo, tutampelekea Mheshimiwa Rais naye afanye kwa sehemu yake kwa namna Katiba yetu inavyotuelekeza.

Hivyo nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuleta marekebisho haya kwa wakati. Wakati huu tulionao Watanzania, marekebisho haya ni ya muhimu sana ikiwa ni pamoja na kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama dhidi ya madawa ya kulevyia, pia kuhakikisha wale watuhumiwa wanatendewa inavyostahili; kama ni adhabu, wanapewa inavyostahili. (Makofii)

Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wasaidizi wako wote na msaidizi wa hiyari uliyempata leo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Tunawapongeza sana. (Makofii)

Pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Katiba na Sheria, mambo mengi mmeyasikia hapa ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasikiliza watu wa Kamati, mengine yameondolewa na mengine yameboreshwa. Kwa hiyo, Kamati yetu imefanya kazi nzuri sana. Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, tunawapongeza sana na tunawashukuru sana kwa kufanya kazi hii nzuri ambayo sote siku ya leo hapa tumeweza kuihitimisha. Tunawatachia kila la heri katika majukumu mengine yaliyo mbele yenu, tunaamini mtaendelea kuyafanya vizuri kama mlivyo yafanya haya.

Wabunge wengine pia tunawashukuru kwa kazi nzuri mliyoifanya, mmepitia huu Muswada, mmetoa michango mizuri. Yale ambayo hayataweza kuingia kwenye haya marekebisho kwa ajili ya mipaka ya kanuni zetu, Serikali imeyasikia, mengine itaenda kuyafanyia kazi kwa maana ya utekelezaji wa sheria hii na mengine, pengine huko baadaye wanaweza kutazama mazingira ya kuleta merekebisho siyo ya sheria hizi tu, pengine na nyingine ambazo zitakuwa zinaathiriwa na utekelezaji wa yale ambayo leo hapa tumeyapitisha. Kwa hiyo, tujipongeze Bunge zima kwa kazi nzuri. (Makofij)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza, ninayo mambo mawili. La kwanza, tunapokea ushauri, lakini pia huko tunakoenda na sisi kujifunza hapa na pale, leo nataka kutoa katazo la msingi sana.

Waheshimiwa Wabunge, sisi tunakatazwa tayari lakini hawa wasaidizi wetu walikuwa wao hawana hilo katazo la kupita mbele ya Siwa. Hili eneo ambalo Siwa imewekwa, huku ambako huwa tunaenda kujifunza hapa na pale, watu hawaruhusiwi kupita pita kwa sababu Siwa ni kuonesha Mamlaka ya Bunge. Sasa kwa sababu lengo lake hasa ni kuonesha Mamlaka ya nyumba hii, basi hilo eneo ambalo inakuwa imekaa, ikae yenyewe, badala ya mtu amepitapita, mara kaigusa huku, kapita hivi, aah.

Maana yake ni nini? Tutakapokuwa tunawatuma Wajumbe, wana sehemu ya kupita huko nyuma na hata hapa kwangu wanaruhusiwa kupita Mimi siyo Siwa. Kwa hiyo, wanaruhusiwa kupita hapa na huko, wazunguke, wapite huku. Hata sisi Wabunge, unapoleta hoja kama unatoka Kambi ya Walio Wachache, ni sahihi kukaa huku, kwa sababu utapitiliza mbele hapo, utakuwa hujazunguka.

Pia tunaotoka upande wa walio wengi na viongozi wa Kamati tunaotumia upande huu, lazima utokee upande huu. Hauruhisi kupita kwenye huu mzunguko wa Siwa hapa katikati. Nadhani nimeeleweka. Kwa hiyo, usitokee ukasema naenda kusoma pale mbele, kwa hiyo, ukakatiza hapo kama anavyoingia Spika, hapana. Hili eneo liachiwe Siwa kwa sababu ndiyo inaonesha Mamlaka yetu sisi wote kama Bunge. Nadhani hilo limeeleweka, na wahudumu nadhani wamenielewa vizuri. Hilo lilikuwa ni jambo la kwanza. (Makofij)

Jambo la pili, jana, niliombwa Mwongozo na mwingine sikuombwa Mwongozo lakini nikasema nitatoa mwenyewe. Ule wa Mheshimiwa Maige bado unafanyiwa kazi, lakini Mwongozo alioomba Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi kuhusu kutokujibiwa swali lake kikamilifu nitautoa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 13 Septemba, 2022 katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Jimbo la Mahonda aliomba mwongozo wa Spika chini ya kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwezi Juni, 2020.

Wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Mwinyi aliuliza swali la msingi Namba 20 kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwamba: Je, Serikali imechukua hatua gani kutatua changamoto zinazolezwa, za ukiritimba zilizopelekea kampuni ya Uber kusitisha shughuli zake nchini Tanzania?

Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi kama ifuatavyo; “Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianza kudhibiti huduma za Taxi Mtandao mwezi Mei, 2020. Kwa kutumia Sheria ya Madereva na Wamiliki wa Mifumo ya Taxi ambayo ni pamoja na kampuni ya Uber; kutokana na hatua ya LATRA kuweka tozo katika huduma za Taxi Mtandao, Kampuni ya Uber iliamua kusitisha kutoa baadhi ya huduma hapa nchini mwezi Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia LATRA inaendelea na mazungumzo na kampuni ya Uber kwa lengo la kuhakikisha inarejesha huduma za Taxi Mtandao.” Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwinyi alipata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambayo aliuliza, nanukuu; “Swali la kwanza, kwa kuwa Uber inachangia kwa kiasi kikubwa sana ajira nyingi za vijana; je, Serikali haioni kwamba ajira ya vijana ina mchango chanya zaidi kushinda hizi tozo ndogo ambazo Serikali imeziweka?

Swali la pili; Kwa kuwa Uber ni kampuni ya teknolojia na siyo kampuni ya usafiri, Uber ulimwengu mzima haina gari hata moja; inawezesha watu wenye magari kuweza kufanya biashara ya usafiri wa taxi kirahisi na kwa gharama nafuu; je, taasisi ya LATRA, mdhibiti wa magari ya ardhini ni taasisi sahihi kufanya majadiliano na kampuni ya Uber?”

Naibu Waziri alijibu maswali haya ya nyongeza pamoja na mambo mengine alisema, nanukuu: “Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Mahonda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Uber pamoja na mashirika mengine ambayo yalikuwa yanatoa huduma za Taxi Mtando yanayotoa ajira kubwa kwa vijana, lakini pia yanatoa huduma kwa wasafiri. Kilichopelekea kusitisha huduma kwa kampuni hii ya Uber na Bolt ilikuwa ni baada ya LATRA kuona uwezekano wa wao kupunguza kamisheni ambapo walikuwa wanatoa zaidi ya asilimia 25 na kukawa kuna malalamiko ya wamiliki wa taxi ambapo waliona kamisheni ile sasa hawafanyi kazi vizuri ndio maana wakasimama.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 mpaka 8 Septemba, 2022 LATRA, wamiliki wa hizi taxi pamoja na wasafirishaji wengine wamekaa na wamekubaliana kupata muafaka na kabla ya mwisho wa mwezi huu, Serikali itatoa taarifa, maana kumekuwa na mazungumzo mazuri ya kuwa na *win win situation* kwa msafiri, mwenye taxi na kampuni hizi ambazo zinasimamia huu usafiri wa taxi mtando." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo, Mheshimiwa Mwinyi aliomba mwongozo wa Spika akieleza kuwa katika maswali ya nyongeza mawili aliyouliza, moja lilijibiwa vizuri, la pili halikujibiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotolea ufanuzi kuhusiana na mwongozo huo kuwa kanuni zetu zinataka maswali yote yajibie kikamilifu; na kwa kuwa sikuwa na uhakika kama swali hilo la nyongeza lilijibiwa ama halikujibiwa, niliahidi kutazama Taarifa Rasmi za Bunge, maswali aliyouliza na majibu aliyyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ili swali hilo kama limesahafulika tumpe fursa ya kujibu wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kuhusu majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri hususan majibu ya swali la pili la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Mwinyi lilitaka kujua kuhusu iwapo ni halali kwa LATRA kufanya majadiliano na kampuni ya Uber.

Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika kufafanua jambo hilo, alieleza Bunge kwamba yalikuwepo malalamiko ya wamiliki wa taxi ambayo yaliifiki LATRA kuhusu mapato katika biashara ya Taxi Mtando. Alieleza zaidi kuwa LATRA ndiye msimamizi wa vyombo vya usafiri ardhini, aliwaita wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri, yaani taxi na wasafirishaji wengine akiwemo Uber ili kupata muafaka wa malalamiko hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia Hansard, nimebaini na kuridhika kuwa maswali yote mawili ya nyongeza yalijibiwa kwa pamoja na kwa ukamilifu. (Makof)

Swali la pili, lilijibiwa kikamilifu kwamba ilikuwa muhimu kwa LATRA kuwakutanisha wamiliki wa taxi na Uber ili kupata muafaka wa malalamiko yaliyowasilishwa na wamiliki wa taxi ili kupata muafaka.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo basi, kwa kuzingatia Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020 inayosimamia swali kujibiwa kikamilifu, nimeridhika kuwa swali la pili la nyongeza lilipata majibu kikamilifu. Huo ndiyo mwongozo wangu. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 7.54 mchana Bunge lilahirishwa hadi siku ya Alhamisi,  
Tarehe 15 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)